# Watiwa Mafuta Katika Wakati Wa Mwisho

Jeffersonville, Indiana USA

Julai 25, 1965A

1 Habari za asubuhi, wasikilizaji. Hebu na tuzungumze na Bwana wetu sasa. Mungu Mkuu, Muumba wa mbingu na nchi, Ambaye kwa Uungu umetupangia wakati huu asubuhi ya leo, ya kukuabudu Wewe. Na jalia sisi, Bwana, mioyoni mwetu tujisalimishe kabisa kwa mapenzi Yako ya Kiungu na kutenda kazi kwa Roho Mtakatifu ndani yetu, kuleta kile ambacho ungetaka tujue. Shauku yetu ni kuwa Wakristo bora na wawakilishi Wako walio wazuri zaidi. Tujalie jambo hili asubuhi ya leo, tunapokungojea Wewe, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ketini. [Mtu fulani anasema, "Unataka kuondoa vitambaa vyako vya maombi?"—Mh.] Ndiyo.

2 Tuna furaha sana kuwa hapa asubuhi ya leo tena, katika—katika kumtumikia Mfalme mkuu. Nasi tunasikitika, sisi, tena, ya kwamba hatuna nafasi kwa ajili ya watu, bali tuna … Tutajaribu na kujitahidi tuwezavyo, chini ya hali hizi.

Sasa, wengi wana leso na haja za maombi zimewekwa hapa ili kuombewa. Nami naziweka tu kando; si kwamba ninazipuuza, bali mimi hasa huziombea baada…kama vile, na usiku wa leo. Nitafanya hivyo asubuhi ya leo, halafu usiku wa leo tena, wakati … Kisha nitaomba na kumngoja Roho wa Mungu kwa ajili ya kuponya, na hapo ndipo ambapo napenda kuombea le—leso na kadhalika.

3 Na juu ya maombi maalum, Billy aliziwasilisha, kila moja, kwangu. Kuna kama mia tatu, na ndiyo kwanza niondoke vyumbani mle wakati huo. Mnaona, ninazichukua tu kwa haraka sana, na kila moja, ambazo ninaweza kuzifikia. Nami nitazishughulikia upesi tu niwezavyo. Sitaweza kuzishughulikia zote. Ninanyosha mkono tu na kuchukua moja, na kusema, "Bwana, hivi itakuwa *huyu* ndiye, na itakuwa ni *huyu*?" Namna hiyo tu, kwa sababu wao, kila mmoja, ni mhitaji, haja za kweli; kitu fulani, hapana shaka, ambacho hatuna budi kukizungumzia pamoja. Nami … Kidogo, mwajua, wakati mwingine Roho Mtakatifu anaweza kusema jambo fulani moja nililosoma, ambalo hudumu moyoni mwangu; narudia jambo hilo tena, na kulitafuta humo ndani hata nitakapolipata. La sivyo, mimi huziokota vyo vyote tu.

4 Sasa, tunataka pia kusema, asubuhi ya leo, na kuwasalimu wale walio huko nje katika sehemu zingine za nchi. Tunataka kuwasalimia watu asubuhi ya leo kwa njia hii ya mawasiliano ya simu, kwenye Jiji la New York; Beaumont, Texas; Prescott, Arizona; Tucson, Arizona; San Jose, California; Connecticut; Gainesville, Georgia; na New Albany, Indiana; kote nchini. Tunakusalimu katika Jina la Bwana Yesu.

Asubuhi ya leo, huko Indiana, ni asubuhi nzuri. Tulipata mvua jana usiku ambayo ilipoza hali ya hewa. Nasi tunaninii … Maskani yamejaa, na kila mtu anangojea, kwa matarajio makubwa, kwa ajili ya somo la shule ya Jumapili. Nami ninatumaini ya kwamba baraka nyingi sana za Mungu zitakuwa juu yenu huko nje.

Nasi tunatumaini, upesi iwezekanavyo, kufanya—njia ambayo tunaweza kuwa nayo, mahali ambapo tunaweza kuja sote pamoja, labda chini ya hema kubwa, ambapo ninajisikia kabisa kuongozwa kuhubiri juu ya Vitasa hivi Saba vya mwisho katika Biblia.

5 Kwa hiyo sasa, ili kwamba tusichukue muda mrefu sana kwenye somo kuu asubuhi hii … Nimemtafuta Bwana, nikiwaza, "Ningesema nini?" tukijua ya kwamba huenda hii ikawa ndiyo ibada yetu ya mwisho tutakayopata kuwa nayo. Kuja kwa Bwana kumekaribia sana!

Ninaona, baada ya utabiri huo uliofanywa huko California, kuna nyumba huko nje, na mahali, zikizama kwa kiwango cha inchi thelathini kwa saa, mbao zikipasuka na kuvunjika. Nao hawajui kinachofanya jambo hilo. Tuko mwishoni. Nyumba za dola laki moja, zinazama. Nina vichwa vikubwa vya maneno katika gazeti, picha, ambazo ninatumainia kuzileta usiku huu, kwa kuwa nataka kuzungumzia jambo fulani juu ya hilo usiku wa leo.

6 Na, basi, usiku wa leo tuna maombi kwa ajili ya wagonjwa. Njoo alasiri ya leo, saa tano, saa sita, ama wakati wowote. Tutaanza mapema, nadhani, ili watu waweze kuondoka mapema, na kupokea kadi zenu za maombi. Nasi tutakuwa tukiwaombea wagonjwa usiku wa leo, Bwana akipenda.

7 Sasa, baada ya kuwaza kwa maombi, "Nifanye nini?" nikijua ya kwamba siku moja sina budi kujibu kwa yale ninayosema hapa … Nami nimeamua, ama nimejisikia kuongozwa na Roho Mtakatifu kuzungumza asubuhi ya leo juu ya unabii, kwa namna fulani kutufahamisha. Mnaona? Ni kitu ambacho sisi … Kama hatujafahamishwa, na jambo lo lote likitukia kawaida tu, tunapaswa kujua kuhusu jambo hili. Roho Mtakatifu ametupa, kuwaonya watu juu ya kuja. Mnajua, Biblia ilisema, ya kwamba, "Mungu hatafanya jambo lo lote isipokuwa kwanza awaonyeshe watumishi Wake, manabii." Na—na namna ambavyo Yesu aliwaonya watu, ni kitu gani kingetukia; namna manabii walivyowaonya watu, yale yangetukia. Na inatupasa sasa, katika ile saa kuu tunayoishi, kuona ni wakati gani tunaoishi, na kile kinachotukia, kile kitakachotukia katika wakati huu. Kwa hiyo moja ya masomo haya ya ajabu ambayo labda tumesoma mara nyingi, liliinijia moyoni mwangu ku—kuzungumza na watu juu yake asubuhi ya leo.

8 Sasa hebu na tufungue katika Biblia zetu katika Mathayo sura ya 24 na tusome sehemu ya Neno.

[Ndugu Branham anasafisha koo lake — Mh.] Samahani. Kwa njia ya—ya kupata yaliyomo kwa fungu letu la maneno na somo letu.

Sasa, kumbukeni tutafundisha hili kama darasa la Biblia, polepole. Chukueni penseli zenu na karatasi. Nina Maandiko mengi yaliyoandikwa hapa, ambayo—ili mweze kuyaandika haya. Kisha mwende nyumbani mkayasome, kwa maana hili ni kama tu darasa la shule ya Jumapili, tupate kujua, na kuonywa na kutayarishwa kwa ajili ya saa tunazoishi.

9 Katika Kitabu cha Mathayo Mtakatifu. [Ndugu Branham anasafisha koo lake — Mh.] Samahani. Kifungu cha 24 … Ama, mlango wa 24, hasa, kuanzia kifungu cha 15, ninataka kusoma sehemu ya Neno Lake.

> *Basi hapo mtakapoliona chukizo la uharibifu, lile lililonenwa na nabii Danieli, limesimama katika patakatifu (asomaye na afahamu),*
>
> *Ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani.*
>
> *Naye aliye juu ya dari—juu ya dari asishuke kuvichukua vitu vilivyomo nyumbani mwake;*
>
> *Wala aliye shambani asirudi nyuma kuichukua nguo yake.*
>
> *Ole wao wenye mimba na wanyonyeshao siku hizo!*
>
> *Ombeni, ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi, wala siku ya sabato.*
>
> *Kwa kuwa wakati huo kutakuwapo dhiki kubwa, ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa, wala haitakuwapo kamwe.*
>
> *Na kama siku hizo zisingalifupizwa, asingeokoka mtu ye yote; lakini kwa ajili ya wateule zitafupizwa siku hizo.*
>
> *Wakati huo mtu akiwaambia, Tazama, Kristo yupo hapa, au yuko kule msisadiki.*
>
> *Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule.*
>
> *Tazama, nimekwisha kuwaonya mbele.*
>
> *Basi wakiwaambia, Yuko jangwani, msitoke; yumo nyumbani, msisadiki.*
>
> *Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.*
>
> *Kwa kuwa po pote ulipo mzoga, ndipo watakapokusanyika tai …*

10 Sasa, kwa ajili ya somo, ningetaka kuchukua kifungu cha 24, kusisitiza juu ya kifungu hiki kwa ajili ya somo letu la shule ya Jumapili asubuhi ya leo. Na sikilizeni kwa makini ninaposoma hili tena.

> *Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule.*

Sasa kwa ajili ya somo asubuhi hii, ama fungu la maneno, hasa, nataka kuchukua: *Watiwa Mafuta Katika Wakati Wa Mwisho.* Hilo ndilo somo ninalotaka kuzungumzia, ama fungu la maneno: *Watiwa Mafuta Katika Wakati Wa Mwisho.*

11 Ninaamini ya kwamba tunaishi katika wakati wa mwisho. Nafikiri karibu kila mtu ambaye … Msomaji wa Maandiko, ama hata mwa—mwamini, anajua ya kwamba sasa tuko kwenye mwisho wa historia ya ulimwengu. Hakutakuwa na haja ya kuiandika, kwa maana hakutakuwa na mtu wa kuisoma. Ni mwishoni mwa wakati. Ni lini tu, sijui. Ni muda gani tu utakaokuwa, hata Malaika wa Mbinguni hawajui dakika hiyo au saa. Lakini tumekwishaambiwa na Bwana Yesu, ya kwamba, wakati mambo haya tunayoona sasa yanapoanza kutukia, basi kuinua vichwa vyetu kwa maana ukombozi wetu unakaribia. Sasa, maana ya "kukaribia", sijui. Inaweza kumaanisha …

12 Kama vile wale wanasayansi walivyosema juzijuzi, kwenye televisheni, wakizungumzia juu ya ule mwanya mkuu wa maelfu ya maili ardhini ambao utazama. Aliulizwa swali, "Ungewezaje kuzama pale?" Hiyo ni Los Angeles, Pwani ya Magharibi. Na wengi wenu mmeona namna walivyolifuatilia jambo hilo kwa rada, na kupitia katika…ukakatiza kule chini ya San Jose, ukaenda hadi ukaingia Alaska, huko nje kupitia kwanye Visiwa vya Aleutia, yapata maili mia mbili huko baharini, kisha ukarudi ukaingia San Diego, ukazunguka nyuma ya Los Angeles, kisha ukaja kule, shimo kuu.

Na matetemeko haya yote ya ardhi ambayo tumekuwa nayo ni volkeno ikipiga kata hii kubwa tupu, inavyoonekana, kule ndani. Siwezi kukumbuka jina ambalo wao—wao waliliita. Hata hivyo, wakati hilo

linapotikisika, hilo linatoa matetemeko haya ya nchi ambayo tumekuwa nayo kwa miaka mingi kwenye Pwani ya Magharibi. Sasa limepasuka nyufa kila mahali. Nao wanasayansi wakasema, mmoja …

13 Yule mtu akamwambia yule mwingine, "Hiyo ingeweza kuzama?"

Yeye alisema, "Si 'ingeweza,' bali itazama."

Kasema, "Lakini si katika kizazi chetu, labda?"

Kasema, "Katika dakika tano zifuatazo, ama miaka mitano ijayo. Hatujui ni lini."

Juma hili, nilitumiwa kichwa cha maneno kwenye gazeti, juu ya manyumba makubwa ya dola laki moja elfu zikiatuka na kupasuka, watu wakihama. Nao hawajui namna ya kulikomesha. Hakuna njia ya kukomesha jambo hilo. Mnaona, Mungu anaweza kufanya lo lote atakalo, na hakuna mtu anayeweza kumwambia namna ya kulifanya.

Mnajenga nyumba, mnaweza kutengeneza vitu vya kisayansi, na Mungu ndiye Muumba wa sayansi. Mtamkomeshaje? Anaweza kuiangamiza dunia asubuhi ya leo kwa viroboto kama akitaka. Je! Mnatambua, Yeye angeweza kusema viroboto wawepo, nao wangekuwa na kina cha maili arobaini katika muda wa nusu saa, Mnaona, hakuna … na kula watu na wawamalize ardhini. Yeye ni Mungu. Yeye hufanya tu apendavyo. Yeye ni mwenye mamlaka, Mwenyewe.

14 Sasa, tunapoona hili ongezeko lote la ushuhuda, ya kwamba saa tunayoishi sasa, nafikiri ni jambo zuri kuyarudia mambo haya na kuyafafanua, kwa kuwa ile Mihuri imekwisha funguliwa, na tutafute ukweli wa mambo haya, kwa kuwa Mungu amekuwa mwaminifu sana kwetu, kwa neema yake, kutuonesha mambo haya.

Nawatakeni muone hapa katika Mathayo 24, Yesu alitumia neno "Makristo," M-a-k-r-i-s-t-o, "Makristo." Si Kristo, bali "Makristo," wingi, si umoja. "Makristo." Kwa hiyo, neno *Kristo* linamaanisha "aliyetiwa mafuta." Na halafu kama ni "aliyepakwa mafuta," hakutakuwa na mmoja tu, bali wengi, waliotiwa mafuta, "waliotiwa mafuta." Mnaona?

La sivyo, kama Yeye angetaka kulichambua ili kwa namna fulani tupate kulifahamu vizuri zaidi, Yeye angesema, "Katika siku za mwisho watainuka watiwa mafuta wa uongo." Sasa, hilo linaonekana karibu haliwezekani, mnaona, masharti ya "aliyetiwa mafuta." Lakini angalia maneno yanayofuata, "na manabii wa uongo," m-a-n-a-b-i-i, wingi.

15 Sasa, aliyetiwa mafuta, ni, "mmoja mwenye ujumbe." Na njia pekee ambayo ujumbe unaweza kutolewa ni kwa yule aliyetiwa mafuta, na huyo angekuwa ni nabii, aliyetiwa mafuta. "Watatokea waalimu wa uongo, waliotiwa mafuta." Nabii hufundisha ujumbe wake ni nini. Walimu waliotiwa mafuta, bali watu waliotiwa mafuta na mafundisho ya uongo. Waliotiwa mafuta, "Makristo," wingi; "Manabii," wingi. Na kama kuna kitu kama Ki—Kristo, umoja, basi hawa ingewabidi kuwa "waliotiwa mafuta," kwamba unabii wao wa yale waliyokuwa wakifundisha ungekuwa tofauti, kwa sababu wao ni watiwa mafuta, waliotiwa mafuta.

16 Sasa, ni somo la shule ya Jumapili, tunataka ku—kujaribu kuleta hili kwenye shindano la kweli, kwa Maandiko, si kwa yale mtu mwingine amesema juu yake, bali ni kusoma tu Maandiko.

Mnaweza kusema, "Hili linawezekanaje? Hivi watiwa mafuta …"

Walikuwa nini? "Makristo," M-a-k-r-i-t-o, watiwa mafuta. "Makristo, na manabii wa uongo." Waliotiwa mafuta, bali manabii wa uongo!

Yesu alisema, ya kwamba, "Mvua huwanyeshea wenye haki na wasio haki."

Sasa, mtu fulani anaweza kuniambia, "Je! Unaamini ya kwamba upako huo juu ya watu hao unamaanisha kwamba ni upako wa Roho Mtakatifu?" Naam, bwana, Roho Mtakatifu halisi wa Mungu juu ya mtu, na hata hivyo ni uongo.

Sasa sikilizeni kwa makini na mwone Yeye alivyosema. "Nao wataonyesha ishara na maajabu, hata ingewapoteza walio Wateule kama yamkini." Nao wametiwa mafuta na Roho Mtakatifu halisi. Ninajua hili linasikika ni la kipumbavu sana, bali tutachukua wakati na kulielezea kwa Neno, ya kwamba hiyo ni HIVI BWANA ASEMA kabisa, ile Kweli.

17 Sasa hebu na tufungue katika Biblia zetu, kwa dakika moja, kwenye Mathayo sura ya 5, na tuanzie kwenye aya ya—ya 45, na tuone sasa tunaposoma kwa muda mfupi juu ya Maandiko haya. Halafu basi, baada ya sisi kufika hapa, mbona, tutawapa … Kwa hiyo ninyi, kama tukishindwa kuyasoma yote, basi chukua Biblia yako; na—na pia unaweza kuyasoma baada ya sisi kuondoka hapa na wewe uende nyumbani, na—na usome kile Biblia inachosema kuhusu jambo hilo.

18 Sasa kuchukua wakati wetu, kupata jambo la—la msingi, kwa sababu ninatoa tamshi hapa ambalo ni

la kushangaza. Roho Mtakatifu anawezaje kumpaka mafuta mwalimu wa uongo? Lakini hilo ndilo Yesu alilosema lingetukia.

Sasa, Mathayo, mlango wa 5, kifungu cha 45, hebu na tusome sasa. Hebu na tupate, tuanze ninii—kidogo nyuma yake, ya 44.

> *Lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, na kuwabariki wale wanaowalaani, na kuwatendea mema wale wanaowachukia, … waombeeni wale wanaowadhulumu, na kuwatesa;*
>
> *Ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki;* (Mvua hujiliaa walio waovu sawasawa na walio wema.)

19 Sasa kufuatilia jambo hili, kwenye unabii mwingine unaohusu jambo hili, jalia tufungue sasa katika Waebrania sura ya 6, kwa ajili ya kifungu kinachofuata cha jambo hili, ambapo Paulo akikumbusha jambo lile lile alilosema Yesu. Paulo, akinena sasa. Wakati mnapotafuta … Na ninyi huko nje kwenye matangazo, chukueni Biblia zenu karibu nanyi na kipande cha karatasi, na mwangalie jambo hili sasa. Waebrania, mlango wa 6, Paulo akiwaandikia Waebrania, akiwaonyesha vivuli na mifano, akiwaleta kutoka chini ya Uyahudi akawaingiza katika Ukristo, akiwaonyesha jinsi ambavyo mambo yote ya kale yalionyesha tu kivuli cha mambo yaliyokuja. Paulo akinena sasa, Waebrania 6.

> *Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo* (K-r-i-s-t-o), *tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu; tusiweke msingi tena wa kuzitubia ... kazi zisizo na uhai, na wa kuwa na imani kwa Mungu,*
>
> *Na ... wa mafundisho ya mabatizo, na kuwekea mikono, na kufufuliwa wafu, na hukumu ya milele.*
>
> *Na hayo tutafanya Mungu akitujalia.*
>
> *Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu,*

Nataka mnisikilize kwa dakika moja tu. Mliona, hiyo ni "karama"; na si "karama," washiriki wa "karama za mbinguni"? Lakini, "karama ya mbinguni," umoja; "Kristo," umoja; "Karama," umoja.

> *… Kipawa chaa mbinguni, na … kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu,*
>
> *Na kulionja neno zuri la Mungu …* (nimeonja kitu gani?) … *Neno la Mungu, na nguvu za zamani zijazo,*
>
> *Wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsulibisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri.*
>
> *Maana,* (sikilizeni) *nchi ... inayoinywa mvua inayoinyeshea mara kwa mara, na kuzaa mboga zenye manufaa kwa hao ambao kwa ajili yao yalimwa, hushiriki baraka zitokazo kwa Mungu;*
>
> *Bali ikitoa miiba ... na magugu hukataliwa na kuwa karibu na laana; ambayo mwisho wake ni kuteketezwa.*

20 Sasa linganisha hilo na Mathayo 5:24 tena. Angalia, Yesu alisema mvua na jua huja juu ya nchi, kwamba Mungu huituma kuandaa chakula na vitu kwa ajili ya watu wa duniani. Na mvua hutumwa kwa ajili ya chakula, mboga. Lakini magugu, kwekwe, vikiwa shambani, yanapokea kitu kile kile. Mvua ile ile inayoifanya ngano ikue ni mvua ile ile inayofanya magugu kukua.

21 Namna nilivyokuwa na somo juu ya jambo hilo wakati mmoja, wakati nilipokutana na Wapentekoste kwa mara ya kwanza! Na lilikuwa ni somo kubwa kwangu. Niliona watu wawili, mmoja … Kamwe sijawahi kusikia kunena kwa lugha hapo kabla. Mmoja alinena kwa lugha, huyo mwingine alifasiri, na mwingine vivyo. Na angesema kweli, aseme ya kwamba, "Kuna wengi humu ndani wanaopaswa kutubu usiku wa leo. Kuna wanawake na wanaume, wote wawili." Na watu wangeinuka na kwenda madhabahuni.

Nikawaza, "Ni la utukufu iliyoje!"

22 Na ndipo nikiwa na kipawa kidogo cha Roho Mtakatifu, nilizungumza na watu hao, tu, mnajua namna, katika utambuzi, njia ndogo tu ya kujua. Na mmoja wao alikuwa Mkristo halisi, naye alikuwa mtumishi halisi wa Kristo, na huyo mwingine alikuwa mnafiki. Na mmoja wao, yule aliyekuwa mnafiki, alikuwa akiishi na mwanamke mwenye nywele nyeusi, akizurura na mwanamke mwenye nywele za shaba na kuzaa naye watoto. Vema, ilikuwa papo hapo katika ono; isingeweza kukanushwa. Nami nikazungumza naye kuhusu

jambo hilo. Akanitazama na kuzunguka jengo hilo.

23 Sasa nilikuwa nimechanganyikiwa, hakika kabisa. Nilifikiri nilikuwa nimekutana na malaika, kisha nikashangaa kama sikuwa kati ya pepo. Hili lingewezekanaje? Nisingeweza kufahamu jambo hilo. Na kwa miaka mingi nikajiepusha nalo, mpaka siku moja wakati…

George Smith, yule mvulana anayetembea na binti yangu, tulienda jana, huko kwenye kinu cha kale ambako mimi huenda kuomba.

Na baada ya kuwa mle ndani siku chache, Roho Mtakatifu alinirudishia Andiko hili. "Kwa maana mvua huinyeshea mara kwa mara na kuzaa mboga, bali michongoma na miiba huishi kwa mvua ile ile, ambayo mwisho wake ni kuteketezwa." Kuishi kwa njia ile ile inayotoa uhai ya Mungu. Ndipo nikafahamu jambo hilo. "Kwa …" Yesu alisema, "Kwa matunda yao wanajulikana."

24 Naam, kwa hiyo, mvua ikishuka juu uoto wa asili wa nchi, ni mfano wa mvua ya Kiroho ambayo inatoa Uzima wa Milele, ikishuka juu ya Kanisa, kwa kuwa tunaiita mvua za masika na mvua za vuli. Na ni mvua, ikimwagika kutoka kwa Roho wa Mungu, juu ya Kanisa Lake.

25 Angalia, ni jambo la ajabu sana hapa. Mnaona? Wakati mbegu hizo zilipoingia ardhini, vyo vyote zilivyoingia pale, zilikuwa ni miiba kwanza. Lakini hapo ngano ile ambayo iliingia ardhini, na mboga, zilikuwa mboga kwanza. Na kila mimea ikijizaa, tena, ilionyesha ya kwamba ilikuwa katika mwanzo wa asili.

Nao watawapoteza Walioteuliwa kama yamkini,‟ maana wao wanapata mvua ile ile, baraka zile zile, wakionyesha ishara zile zile, maajabu yale yale Mnaona? ″Watawapoteza, ama watawadanganya walio Wateule kama yamkini.‟ Sasa, mchongoma hauwezi kujizuia kuwa mchongoma, wala ngano haiwezi kujizuia kuwa ngano; ni kile Muumba wa kila kimoja alichokusudia hapo mwanzo. Hao ni Wateule. Mvua ile ile!

26 Jua huchomoza asubuhi na kuenea kote duniani, kama lilivyofanya na dunia hii na siku tunayoishi. Na jua, jua lile lile linalochomoza Mashariki ni jua lile lile linalotua Magharibi. Na jua hilo linatumwa kuivisha punje juu ya nchi, ambayo miili yetu imefanywa kwa hizo.

27 Tunaishi kwa vitu vilivyokufa. Hiyo ndiyo njia pekee unayoweza kuishi. Na kama kitu fulani hakina budi kufa kila siku ili uishi, kawaida, basi si ni kweli kwamba kama ninii yako … Mwili wako hauna budi kuishi kwa vitu vilivyokufa, kwa ajili ya uhai wa kawaida, ndipo huna budi kitu fulani kufa, kiroho, kuokoa maisha yako ya kiroho. Naye Mungu, akafanyika mwili, nyama, na akafa tupate kuishi. Hakuna kanisa, hakuna kitu kingine ulimwenguni kinachoweza kukuokoa ila Mungu. Hicho ndicho kitu pekee wanachoishi kwacho.

Sasa yafuatilie Maandiko. Yesu ni Neno. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu. Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, na Yeye aliyeishi, akakaa kwetu." "Na mtu hataishi kwa mkate tu," kwa ajili ya mwili, "bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Halafu, unaona, tunaishi kwa Neno, na huyo ni Mungu.

28 Sasa jua huja na kuipevusha punje. Naam, haliwezi kuipevusha yote mara moja. Inapoendelea, ikikomaa, inaendelea kukomaa mpaka unapofikia kwenye suke kamili.

Ndivyo ilivyo, leo, pamoja na Kanisa. Lilianza katika uchanga wake, huko nyuma katika wakati wa giza, ambapo lilikuwa chini ya ardhi. Limekua sasa hata kukomaa. Nasi tunaweza kuona jambo hilo, kikamilifu, namna ambavyo Mungu kwa maumbile daima …

Huwezi kuvuruga maumbile. Hiyo ndiyo shida ya siku hizi. Tunarusha mabomu, na huko nje katika bahari hiyo, tukivunja na kuvuruga kwa mabomu ya atomiki. Unaendelea tu kuvunjavunja zaidi na zaidi takataka hizo za wakati wote, unaziangusha mle ndani. Unakata miti; tufani zitakupata. Unauzuia mto kwa kujenga bwawa; utafurika.

Huna budi kupata njia ya Mungu ya kufanya mambo na kukaa ndani yake. Tumewafanya watu madhehebu katika makanisa na mashirika; angalia tulichopata! Kaa katika njia iliyoandaliwa na Mungu.

29 Lakini, mnaona, "Yeye huituma mvua," tukirudi kwenye somo letu, "juu ya wenye haki na wasio haki." Yesu anakwambia hapa sasa, katika Mathayo 24, ingekuwa ni ishara katika wakati wa mwisho.

Sasa, kama ishara hii itajulikana tu wakati wa mwisho, basi itabidi iwe ni baada ya kufunguliwa kwa Mihuri hiyo. Mnaona? Ni ishara ya mwisho. Hiyo ingekuwa, wakati mambo haya yatakapotukia, itakuwa katika wakati wa mwisho. Na itakuwa ni ishara, sasa, kwa hiyo Wateule hawatachanganyikiwa katika mambo haya. Mnaona jambo hilo? Halafu, halina budi kufunuliwa, kuwekwa wazi.

30 Angalia, ngano na magugu yote yanaishi kwa Upako ule ule kutoka Mbinguni. Wote wawili wanafurahia jambo Hilo.

Ninakumbuka jambo hili, nikirejea kwenye tukio hili juu hapa siku ile kwenye Kinu cha Green. Ni—niliona ono hilo likitokea. Na kulikuwako na dunia kubwa, nayo yote ilikuwa imelimwa. Na hapo Mpanzi akatoka, kwanza. Ninataka kuweka hilo mbele yenu. Angalia kile kinachotoka kwanza, halafu kile kinachofuata. Na wakati Mtu huyu aliyevalia mavazi meupe alipokuja kote duniani, akipanda mbegu, ndipo nyuma Yake akaja mtu, amevaa nguo nyeusi, alionekana mjanja sana, akinyemelea nyuma Yake, akipanda magugu. Na wakati hili lilipotukia, ndipo nikaona mimea yote miwili ikikua. Na ilipokua, mmoja ulikuwa ni ngano na mwingine ulikuwa ni magugu.

Kisha kukatokea ukame, hapo ambapo, ilionekana kwamba, yote miwili ilikuwa imeviinamisha vichwa vyao ikililia mvua. Ndipo likatokea wingu kubwa juu ya nchi, nayo ikanyesha. Nayo ngano ikainuka na kusema, "Bwana asifiwe! Bwana asifiwe!" Na magugu yakainuka na kupiga makelele, "Bwana asifiwe! Bwana asifiwe!" Matokeo yale yale. Wote wawili wakiangamia, wote wawili wanaondoka. Na halafu ngano inainuka na kuona kiu. Na kwa sababu ilikuwa katika shamba lile lile, bustani ile ile, mahali pale pale, chini ya bubujiko lile lile la maji, ngano ikainuka kisha magugu yakainuka kwa kitu kile kile. Angalia, maji yale yale ya upako huzaa ngano, huzaa magugu.

31 Roho Mtakatifu yeye yule anayelitia mafuta Kanisa, ambaye huwapa shauku ya kuziokoa nafsi, ambaye huwapa nguvu za kufanya miujiza, Yeye huwashukia wasio haki kama wale wenye haki. Roho yeye yule! Sasa, huwezi kufanya jambo lingine na kuelewa Mathayo 24:24. Yeye alisema, "Watatokea Makristo wa uongo," watiwa mafuta, wa uongo. Waliotiwa mafuta kwa Kitu kilicho halisi, bali wawe manabii wa uongo wa Kitu hicho, waalimu wa uongo wa Kitu hicho.

Ni kitu gani kingemfanya mtu atake kuwa mwalimu wa uongo wa kitu ambacho ni Kweli? Sasa tutafikia alama ya mnyama katika dakika chache, nanyi mtaona ni madhehebu. Mnaona? Walimu wa uongo; wa uongo, waliotiwa mafuta. Makristo waliotiwa mafuta, bali ni walimu wa uongo. Ndiyo njia pekee unayoweza kuona jambo hilo.

32 Kama tu hapa wakati fulani uliopita, nimenukuu jambo hili. Huenda nikalinukuu kwa maana tumeunganishwa kwa simu nchini kote. Siku moja nilikuwa nikizungumza na rafiki yangu, ambapo hii inakuja asubuhi ya leo, huko Arizona. Naye alikuwa na shamba la—la machungwa. Naye alikuwa na mti pale ambao ulikuwa ni mchungwa uliokuwa ukizaa matunda ya balungi, na limao, chenza, kangaja. Nami ninasahau ni matunda mangapi mbalimbali yaliyokuwa kwenye huo mti mmoja. Nami nikamwambia yule—yule—yule mtu, nikasema, "Imekuwaje? Ni mti wa aina gani huo?"

Yeye alisema, "Mti, wenyewe, ni mchungwa."

Nikasema, "Mbona una matunda ya zabibu juu yake? Kwa nini una malimao?"

Yeye alisema, "Yamepandikizwa kwake."

Nikasema, "Ninaona. Vema, sasa," nikasema, "sasa, mwaka ujao wakati mti huo utakapozaa mazao mengine ya matunda," ambapo yote huiva karibu wakati mmoja, nikasema, "basi utazaa machungwa kabisa. Kama ni mchungwa kitovu, utazaa machungwa ya kitovu, sivyo, bwana?"

Akasema, "La, bwana. Kila tawi lililopandikizwa litazaa kwa jinsi yake."

Nikasema, "Unamaanisha ya kwamba tawi la limao litazaa limao kutoka kwenye mti huo wa chungwa?"

Akasema, "Naam, bwana."

"Je! Mbalungi itazaa balungi kutoka kwenye huo mchungwa?"

Akasema, "Naam, bwana. Hiyo ndiyo asili ya tawi lililopandikizwa kwake."

Nikasema, "Mungu asifiwe!"

Akasema, "Unamaanisha nini?"

Nikasema, "Swali moja zaidi. Sasa, je, mti huo wa chungwa utazaa machungwa tena?"

Yeye alisema, "Wakati utakapotoa tawi jingine." Utakapotoa tawi lingine, si wakati lingine litakapopandikizwa kwake. Lakini, yote ni matunda ya jamii ya mchungwa, nayo yanaishi kutokana na maisha ya jamii ya mchungwa yaliyo katika mti huo wa jamii ya mchungwa.

33 Nikasema, "Haya basi! Mmethodisti itazaa Wamethodisti, kila wakati. Baptisti itazaa Wabaptisti, kila wakati. Katoliki itazaa wakatoliki, kila wakati. Bali Kanisa la Mungu aliye hai litamzaa Kristo kutoka kwenye shina, Neno kila wakati, kama litawahi kutoa tawi lingine Lake."

34 Sasa, mnaweza kulipandikiza mle ndani, mnaona. Kila balungi, limao, kangaja, chenza, hata liwe jamii ya mibalungi gani, kila moja ya hiyo linaweza kuishi kwenye mti huo; bali likitoa ushuhuda wa uongo juu

ya huo mti, likiishi kwa mti huo. Mnaona jambo hilo? Yanaishi na kustawi kwa uhai halisi ulio katika mti huo.

Sasa, kuna Mathayo 24:24, wakiishi kwa Uhai ule ule, bali hawakuwa sahihi, hapo mwanzo. Wanatoa ushuhuda wa uongo wa Mti huo! Ni mchungwa, hata hivyo ni jamii ya mchungwa. Nao wanasema, "Kanisa hili, dhehebu hili linamshuhudia Kristo," nao wana ubatizo wa uongo, ushuhuda wa uongo wa Neno, wakijaribu kusema ya kwamba nguvu za Mungu zilikuwa kwa ajili ya wanafunzi tu.

Yesu, Mwenyewe, alisema, "Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili kwa kila tawi ambalo litawahi…mti ambao utawahi kuzaa, tawi lo lote litakalowahi kuwa kwenye huo mti. Na ishara hizi zitafuatana na matawi halisi." Wapi? Mradi tu ni Mti, mradi tu unatoa matawi, hata ukamilifu wa dahari. "Katika Jina Langu watatoa pepo; kunena kwa lugha mpya; shika nyoka; kunywa vitu vya kufisha; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa nao watapata afya." Mnaona saa tunayoishi? Mnaona yale Yesu aliyosema?

35 Kumbukeni, hii ilikuwa katika wakati wa mwisho, si kule nyuma chini ya Wesley na kule nyuma. Sasa, katika wakati wa mwisho, hili lilikuwa litukie.

Sasa angalia Maandiko; waache washuhudie. Yesu alisema, "Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnafikiri, ama mnaamini, ya kwamba mna Uzima wa Milele, na Hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Kwa maneno mengine, kama mti huu ukiwahi kuzaa tawi… "Mimi ni Mzabibu, ule Mti; ninyi ni matawi. Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya,"Yohana Mtakatifu 14:12.

36 Sasa, "Yeye akaaye ndani Yangu, yeye … yeye aliyekuwa katika shina Langu hapo mwanzo."

Hiyo ndiyo sababu Yesu alikuwa ni Shina na Mzao wa Daudi pia. Yeye alikuwepo kabla ya Daudi, alikuwa ndani ya Daudi, na alikuwa baada ya Daudi, Shina na Mzao wa Daudi pia; Nyota ya Asubuhi, Ua la Uwandani, Ninyoro ya Mabondeni, Alfa na Omega; Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. "Katika Yeye unakaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili." Wote wawili ni Shina na Mzao wa Daudi!

"Yeye aliye Uzima uliochaguliwa, Uzima uliochaguliwa tangu asili, ulio ndani Yangu," Naye ni Neno, "tangu mwanzo; atakapokuja, atazaa matunda Yangu." Yohana Mtakatifu 14:12.

Lakini wengine wataishi kwa jambo lile lile, wakijiita Wakristo na waaminio. "Si wote wasemao, 'Bwana, Bwana,' watakaoingia."

Sasa, hili litatukia na kudhihirishwa katika siku za mwisho, "wakati siri za Mungu zitakapotimizwa," kama tutakavyofikia baadaye kidogo.

37 Miti hii, mzabibu wa kweli na mzabibu wa uongo! Mmenisikia nikihubiri juu ya jambo hilo tangu, tangu miaka mingi iliyopita, namna ilivyokua pamoja. Nikawaleta hao watu mmoja mmoja na kuonyesha ya kwamba, tokea Kaini na Habili, ile mizabibu miwili iliyokutana madhabahuni; wote wawili ni wa kidini, wote wawili wametiwa mafuta, wote wawili wakiwa na shauku ya uzima, na wakimwabudu Mungu yule yule. Na mmoja alikataliwa na mwingine akapokelewa.

Na njia pekee ambayo yule aliyepokelewa angaliweza kufanya jambo lolote tofauti na ndugu yake, lilikuwa limefunuliwa kwake. Kwa kuwa Biblia ilisema, "Kwa imani …" Waebrania, sura ya 11, "Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko ya Kaini, ambaye Mungu alishuhudia ya kwamba alikuwa mwenye haki."

Yesu, alisema, ufunuo wa kiroho wa kwamba Yeye alikuwa ni Nani! "Watu husema Mimi Mwana wa Adamu ni nani?"

Yeye alisema, Petro alisema, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

"Heri wewe, Simoni—Simoni, mwana wa Yona; mwili na damu kamwe havikukufunulia jambo hili. Baba Yangu aliye Mbinguni amelifunua hilo. Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu,"(nini?) Ufunuo wa kweli wa Neno. Huo hapo Mzabibu wa kweli tena. "Habili, kwa imani!"

Ulisema, "Haikuwa ni ufunuo."

38 Imani ni nini? Imani ni kitu ambacho kimefunuliwa kwako; ambacho bado hakipo, lakini unaamini kitakuwepo. Imani ni ufunuo wa mapenzi ya Mungu. Kwa hiyo, kwa ufunuo!

Na makanisa siku hizi hata hayaamini katika ufunuo wa kiroho. Wao wanaamini katika kanuni za mafundisho ya sharti ya madhehebu fulani. "Kwa ufunuo Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko ya Kaini, ambayo Mungu alishuhudia kwamba alikuwa mwenye haki." Amina. Natumaini mnaona jambo hilo. Mnaona mahali tunapoishi? Mnaona wakati?

Nilikuwa nikizungumza na mu—muungwana si muda mrefu uliopita, msomi Mkristo na muungwana. Akasema, "Bw. Branham, tunakataa mafunuo yote."

39 Nikasema, "Basi inakubidi kumkataa Yesu Kristo, kwa kuwa Yeye ni ufunuo wa Mungu, Mungu aliyefunuliwa katika mwili wa kibinadamu." Msipoliona jambo hilo, mmepotea.

Yesu alisema, "Msipoamini ya kwamba Mimi Ndiye, mtakufa katika dhambi zenu." Yeye ni ufunuo wa Mungu, Roho wa Mungu aliyefunuliwa katika umbo la mwanadamu. Kama huwezi kuamini jambo hilo, umepotea. Ukimweka kuwa mtu wa tatu, mtu wa pili, ama mtu ye yote mbali na Mungu, umepotea. "Msipoamini ya kwamba Mimi Ndiye, mtakufa katika dhambi zenu." Ufunuo!

40 Si ajabu hawakuweza kumwona. "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba," katika yale mashina, "watakuja Kwangu." Mnaona? Mnalipata? Loo, namna tunavyopaswa kumpenda, kumwabudu, kumsifu; kuona tunda la Roho katika siku za mwisho, na Mti wa Bibi -arusi ukikomaa kwenye kilele cha wakati!

41 Mzabibu wa kweli na mzabibu wa uongo, yote miwili ilikuwa na upako ule ule. Maji yaliiangukia yote miwili. Si ajabu Yeye alituonya, "Ingewapoteza walio Wateule kama yamkini."

Angalia, wanafanana. Wamepakwa mafuta vivyo hivyo. Lakini angalia, "Kwa matunda yao …" Unaujuaje?

Unajuaje huo si mchungwa? Kwa sababu unazaa balungi. Huo mzabibu ni sawa, unaishi kwenye ule mti, bali unazaa balungi. Si kama ule wa kwanza.

Na kama kanisa linasema wao "wanaamini Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele," na wanakana Uwezo Wake, kukana kazi Zake, kukana Neno Lake; kama—kama… Kanisa linalomwamini Yesu Kristo, litafanya kazi za Yesu Kristo, litakuwa na Uzima wa Yesu Kristo. Na kama halina, haidhuru kama Uhai unatiririkia ndani yake; kama haukuchaguliwa tangu asili, kutoka kwenye yale mashina, utazaa balungi kila wakati, ama kitu kingine. Lakini kama ni Uzima uliochaguliwa tangu asili, katika mizizi, utamzaa Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, kama ni Neno likichipuka kupitia kwenye Shina. Ambapo, Yeye ni Shina, mwanzo wa wakati.

42 Angalia, lakini kile wanachotoa ndicho kinachokuonyesha tofauti yake. "Kwa matunda yao," Yesu alisema, "mtawatambua." "Mtu hachumi zabibu katika miiba," ingawa miiba kweli iko kwenye mzabibu. Hiyo ingewezekana, bali tunda litaonyesha.

Tunda ni nini? Neno, kwa ajili ya tunda la wakati. Hivyo ndivyo ilivyo, mafundisho yao. Mafundisho ya nini? Mafundisho ya wakati, ni wakati gani. Mafundisho ya mwanadamu, mafundisho ya kimadhehebu, lakini, ama Neno la Mungu kwa huo wakati?

Sasa, wakati unaenda upesi sana, hata tungeshikilia jambo hilo kwa muda mrefu. Lakini nina hakika ya kwamba ninyi mliopo hapa, na nina hakika ninyi mlioko kote nchini, mnaweza kuona ninalojaribu kuwaambia, kwa kuwa hatuna muda mrefu zaidi wa kudumu katika jambo hilo.

43 Lakini ili kwamba muone ya kwamba Upako unakuja juu ya wasio haki, walimu wa uongo, na kuwafanya wafanye yale hasa Mungu aliyowaambia wasifanye; bali wao watalifanya, haidhuru. Kwa nini? Hawawezi kujizuia. Mwiba unawezaje kuwa kitu kingine ila mwiba? Haidhuru ni utanyunyiziwa mvua nzuri namna gani, hauna budi kuwa ni mwiba. Hiyo ndiyo sababu Yesu alisema, "Zitafanana sana zingewapoteza Walioteuliwa," ambao ni mashina, "kama yamkini," bali haiwezekani. Ngano haiwezi kufanya kitu ila kuzaa ngano; hivyo tu ndivyo inavyoweza kuvumilia.

44 Angalia. Kumbuka, Mungu si mwanzilishi wa madhehebu. Ibilisi ndiye mwanzilishi wa madhehebu. Nimethibitisha jambo hilo kwa Neno, kwa kila hali, na tena na tena; haitatulazimu kuingilia jambo hilo asubuhi ya leo. Tunajua ya kwamba Mungu kamwe hakuwapanga watu pamoja namna hiyo, kuunda madhehebu. Mamia ya miaka baada ya kifo cha yule mwanafunzi wa mwisho, kabla hawajapata kuwa na madhehebu ya kwanza. Daima yameonyesha kushindwa. Kama hayajashindwa, mbona hatuko pamoja sasa katika upendo leo, Methodisti, Batisti, Presbiteri, Katoliki na wote? Kwa nini kazi za Mungu hazitufuati, basi, kila kanisa kwenye jambo lile lile, Neno? Mambo hayo yanayowatenganisha watu, undugu … Tuko mbali sana na Mungu kuliko tulivyowahi kuwa, makanisa, tukinena habari zake.

45 Sasa, tunaambiwa, ya kwamba, "Mambo yote ya kale yalitukia kwa mifano, kwa mafundisho yetu, yatukemee, maonyo." Kwamba, mambo yote ya kale ya Agano la Kale yalitukia, yakawa kivuli, kuona yale yangekuwa katika Agano Jipya, katika siku zetu.

Ni kama tu hujapata kuuona mkono wako, halafu ukaangalia kuona kivuli ukutani, kama vile mkono wangu ungekuwa kutoka kwenye nuru, kama una vidole vitano hapa kwenye kivuli, wakati ile negativu; nawe uusogeze mkono wako kuelekea, ukiwa halisi, kuelekea—kuelekea kwenye negativu, huna budi utokee na vidole vitano.

Kama vile Biblia inavyotuambia, ya kwamba, "Agano la Kale likiwa kivuli, mfano wa mambo mapya, ama mambo yaliyokuwa yaje; si mambo yaliyopo, bali ni kivuli, mfano wa mambo yatakayokuja."

46 Hebu na turudi nyuma tuone kama jambo hili liliwahi kuwa katika wakati mwingine wo wote. Mnakubali? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Kwa hiyo tutajua, kuthibitisha jambo hili, huku na huko, kwa Neno; si kwa wazo la mtu fulani, nadharia fulani.

Sijali yeye ni nani; mtu mwingine ye yote, mimi mwenyewe au mtu mwingine ye yote, "Kama haneni kulingana na torati na manabii, hamna Nuru ndani yake." Mnaona? Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. "Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu liwe kweli," haidhuru ni nani.

47 Sasa hebu turudi nyuma tuone kama jambo hili liliwahi kutukia, kutuonyesha mfano.

Tungeweza kurudi nyuma sasa katika Kitabu cha Kutoka na kunena juu ya mtu aliyeitwa Musa, ambaye alikuwa nabii aliyetiwa mafuta aliyetumwa na Mungu, akiwa na Neno la Mungu na mapenzi ya Mungu kwa ajili ya kizazi chake. Kama vile Neno la Mungu daima linavyoendelea, Yeye alisema, "Yeye hakufanya lo lote mpaka alipowafunulia manabii Wake kwanza." Ndipo akafanya hivyo. A-ha.

Sasa, Yeye hawezi kusema uongo. Hawezi kusema uongo na awe Mungu. La, bwana. Hana budi kudumu kweli. Hakuna uongo ndani Yake. Yeye ni …

Na Yeye hawezi kulibadilisha. Kama akifanya hivyo, basi Yeye si Mungu; Alifanya kosa. Hana budi kuwa asiye na kikomo. Na asiye na kikomo hawezi kufanya kosa. Mnaona? Kwa hiyo yale Mungu anayosema, hayo ni kweli Milele. Mnaona? Naye aliahidi jambo hilo. Kwa hiyo, angalieni, hakuna mahali katika Biblia isipokuwa pale panapofuata mwendeleo wa moja kwa moja mle.

48 Sasa, Mungu alikuwa amemwahidi Ibrahimu ya kwamba uzao wake ungekuwa mgeni katika—katika nchi ya kigeni kwa muda wa miaka mia nne, ndipo Yeye angemtoa kwa mkono mkuu wa uweza na nguvu, kuonyesha ishara Zake na maajabu miongoni mwa watu ambao walikaa nao. Wakati wa ile ahadi ulikaribia. Watu walikuwa wamesahau jambo hilo. Walikuwa na Mafarisayo na Masadukayo, na kadhalika, madhehebu. Lakini, ghafla, huyu hapa Mungu peke yake na kujiondoa, kutoka, mbali na ye yote wao.

Mungu kamwe, katika siku yoyote au wakati wowote, hajawahi kumwita nabii kutoka kwenye madhehebu. La, bwana. Yeye amechanganyikiwa sana, asingeweza kufanya jambo hilo; angepaswa kukaa na madhehebu hayo.

49 Musa, mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu, akiwa na Neno la Mungu, na akiwa safarini akiwapeleka Israeli katika nchi ya ahadi, akishika kabisa amri ya Mungu, alikutana na nabii mwingine, mpakwa mafuta mwingine aliyekuwa na upako halisi wa Roho Mtakatifu yule yule aliyekuwa juu ya Musa. Hiyo ni kweli. Yeye alikuwa ni nabii. Roho Mtakatifu alikuwa juu ya mtu huyu. Jina lake lilikuwa Balaamu. Sote tunamfahamu. Vema, mambo yale yale, jambo lile lile, mambo—mambo aliyosema mtu huyo, yangali yanatendeka, yapata miaka elfu mbili mia nane iliyopita. "Wewe ni kama nyati, Ee Israeli. Ye yote akubarikiye atabarikiwa. Ye yote akulaaniye atalaaniwa. Nguvu zako, na nguvu zako, jinsi hema zako zilivyo za haki, Ee Yakobo!" Mnaona, asingeweza kujizuia. Yeye alikuja pale akikusudia moyoni mwake kuwalaani watu hao.

50 Loo, ninyi walimu wa uongo mkisikiliza kanda hizi miaka hii yote, na mkimwona Mungu akithibitisha yale hasa aliyosema, na mnaketi katika vyumba vyenu vya kusomea na kujua ya kwamba ni Kweli; na kwa sababu ya tofauti zenu za kimadhehebu, mnaupinga na kuwaambia watu wenu si kweli. Ole wenu! Wakati wako umekaribia.

51 Balaamu, aliyetiwa mafuta na Roho yeye yule aliyekuwa juu ya Musa. Tofauti ilikuwa nini? Mafundisho ya Musa yalikuwa makamilifu. Biblia ilisema hapa katika Petro wa Pili, ya kwamba ilikuwa ni "mafundisho ya Balaamu" ambalo Israeli walipokea, ambayo Mungu kamwe hakusamehe. Dhambi isiyosameheka! Hakuna hata mmoja wao aliyeokolewa, ingawa walikuwa wamekuja chini ya baraka za Mungu, na kuuona mkono wa Mungu ukimtumia nabii huyu mkuu, na kuuona ukithibitishwa kikamilifu na Mungu. Na, kwa sababu, nabii mwingine alikuja na fundisho, kinyume, na kubishana na Musa, na kujaribu kuwathibitishia watu ya kwamba Musa alikuwa amekosea. Na Dathani, Kora, na wengi wao, walikubaliana naye na kuwafundisha wana wa Israeli kufanya uasherati, kufuata shirika lake, kwamba, "Sisi sote ni sawa."

"Kama sisi ni Wamethodisti, Wabatisti, Wapresbiteri, ama Wapentekoste, na kadhalika, sote ni sawa."

Sisi si kitu kimoja! Ninyi ni watu waliotengwa, watakatifu kwa Bwana, waliowekwa wakfu kwa Neno na Roho wa Mungu, kuzaa matunda ya ahadi Yake ya siku hii. Wala wewe si mmoja wao! Ninajua hilo ni kali sana, bali hiyo ni Kweli hata hivyo. Waliowekwa wakfu kwa ajili ya utumishi katika siku hizi za mwisho! "Tokeni kati yao."

52 Sasa, "mafundisho ya Balaamu," si unabii wa Balaamu. Huo ulikuwa sawa. Huyo alikuwa ni Mungu. Ni wangapi wanaoamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Unabii wa Balaamu ulikuwa sahihi kabisa, maana asingeweza kunena kitu kingine. Upako wa Mungu usingalinena kitu kingine cho chote, naye Mungu aliuhakikisha kwa kuthibitisha ulikuwa Kweli. Lakini ilikuwa ni "mafundisho ya Balaamu."

Sasa linganisha hilo na Mathayo 24:24. Waliotiwa mafuta, bali mafundisho yao ni ya uongo. Wa utatu, na mambo yote kama hayo; makosa, upinga Kristo!

Natumaini hamtaumia hisia zenu. Wala msizime hizo, hizo simu zinazima. Wala msisimame na kutoka. Tulieni tu, na hebu tuone kama Roho Mtakatifu hatatufunulia jambo hilo, na kututhibitishia. Mnasema, "Lakini hilo …" Chochote tu unachoamini, tulia tu na usikilize. Na umwombe Mungu afungue moyo wako, ndipo utaona kama wewe ni gugu, ama mwiba, ama po pote unaposimama. Mnaona?

53 Sasa, hata Yuda, "aliyejulikana tangu zamani apate kulaaniwa," alikaa pale mbele ya Yesu. Naye Yesu akamwambia, "Wewe ndiwe. Lo lote unaloenda kufanya, na lo lote linakubidi kufanya, nenda ukalifanye upesi." Yeye akijua alichokuwa anafanya, lakini, kwa ajili ya vipande hivyo thelathini vya fedha, na kupendwa na watu, alimuuza Bwana Yesu Kristo. Mmoja wa wanafunzi Wake, mweka hazina wa kanisa, Yesu alimwita "rafiki" Yake. Mnaona? Biblia ilisema, "Yeye alizaliwa mwana wa upotevu," kama tu vile Yesu alivyozaliwa Mwana wa Mungu. "Kuwapoteza walioteuliwa kama yamkini."

54 Angalia kwa makini tunapoendelea kusoma. Tutachukua mfano mwingine, katika Kitabu cha Wafalme. Kulikuwa na na—nabii, na jina lake lilikuwa Mikaya. Yeye alikuwa mwana wa Imla, naye alikuwa nabii. Alikuwa nabii.

Kisha kulikuwa na nabii mwingine, mkuu wa shirika la manabii, waliotiwa mafuta. Biblia ilisema wao walikuwa "manabii," kama tu vile Yeye alivyosema Balaamu alikuwa ni nabii, waliotiwa mafuta.

Na kulikuwa na mmoja wao jina lake Mikaya, ambaye alitiwa mafuta na Mungu na kutumwa na Mungu, pamoja na Neno la Mungu.

Kulikuwako na mmoja, Zedekia, ambaye alidhani alitumwa na Mungu. Alikuwa ametiwa mafuta na Mungu, bali mafundisho yake yalikuwa kinyume cha Neno la Mungu. "Amkeni, enyi Makristo wa uongo, muonyeshe ishara kuu, mngewapoteza Wateule kama yamkini."

55 Angalia, wote wawili, wote wawili wametiwa mafuta. Sasa, ungewezaje kujua ni nani aliyekuwa wa kweli, na wa uongo? Angalia kile Neno lilichomwahidi Ahabu. Nabii aliyemtangulia, ambaye alikuwa ni Eliya, mmoja wa manabii walio wakuu sana wa wakati huo, huyo alikuwa ni nabii aliyethibitishwa. Huyo nabii aliyethibitishwa alisema, ya kwamba, "Kwa sababu Ahabu alikuwa amefanya uovu huu, ya kwamba mbwa watairamba damu yake; alimuua Nabothi. Na kwamba mbwa wangemla Yezebeli, na … mwili wake ungekuwa mavi mashambani." Sasa, unawezaje kubariki kile Mungu alicholaani? Ama wawezaje kulaani, kama Balaamu alivyosema, alichobariki Mungu? Mnaona?

Lakini manabii hawa walikuwa waaminifu. Hakukuwa na shaka ila walikuwa watu wazuri, watu waheshimiwa. Kwa kuwa, kuwa nabii katika Israeli, huna budi kuwa mtu mwenye heshima, ama hata kuwa Mwisraeli. Ulipigwa mawe, la sivyo. Walikuwa watu waheshimiwa. Walikuwa ni watu werevu. Walikuwa ni watu wenye elimu. Walikuwa wameteuliwa na Ahabu, kutoka taifani. (Unaona jambo hilo, Dada Wright?) Walioteuliwa wa taifa, walistahili kwa ajili ya ninii …

56 Na sasa, wakati Mikaya alipoona ono lake, alijua moyoni mwake vile Neno lilivyokuwa limesema, bali alitaka kuona yale Roho aliyekuwa ndani yake angesema.

Kwa hiyo wakamwambia, wakasema, "Useme jambo lile lile hawa manabii wengine wanalosema. Na utakapofanya hivyo, mbona, utakuwa, tutakupeleka kwenye ushirika, hapana shaka, tena. Mnaona? Tutakufanya mmoja wetu. Tutakurudisha kwenye dhehebu letu. Wewe ni … Tunajua wewe ni nabii, bali daima unasema mambo ya kulaani. Daima unamlaani Ahabu. Sasa, Zedekia, mtu mkuu, papa, ama ninii … chochote kile alichokuwa. "Sasa amembariki Ahabu, na kusema, 'Nenda kafanye hivyo.' Sasa wewe sema jambo lile lile, Imlah. Mbona, wewe ni mtu maskini tu. Huna kusanyiko lo lote, karibu huna, kabisa. Na watu hawa wana mamilioni. Taifa zima liko upande wao. Sasa wewe sema vile vile wanavyosema, uone utakavyofanya, uta—wewe kula utajiri wa nchi." Yeye anazungumza na mtu asiye sahihi pale!

57 Vipi kama ingalikuwa imesemwa, "Mikaya, waweza kupata kosa lo lote kwake Zedekia?" "La." "Je! Ulipata kumshika katika dhambi?" "La." "Umeishawahi kumsikia akimlaani mtu ye yote?" "La." Ulipata kumshika amelewa?" "La." "Unaweza kuitilia shaka elimu yake?" "La." "Unaamini digrii yake ya udaktari ni ya uongo?" "La." "Unaamini Ph —D. ni sawa?"

"Hakika. Kwa halmashauri ya Sanhedrin; nafikiri ni halmashauri yote, nafikiri ni sawa."

"Vema, basi, kwa nini usijiunge naye?"

"Kwa sababu yeye ameacha Neno!"

Vema, tutakuwa na shindano la jambo hilo, basi, kama nabii Eliya kabla ya hapo. Na kama wewe ni mwana wa Mungu, utadumu na nabii wa Biblia hii. Ni Neno. Angalia ile saa, huo wakati.

58 Vema, vipi kama Zedekia alisema, "Loo, najua nabii alisema jambo hilo, bali hilo ni kwa ajili ya kizazi

cha usoni. Hiyo ni kwa muda mrefu tangu sasa”?

Akasema, “Ngojeni hata nitakapoona ono kutoka kwa Mungu, ndipo nitawaambia.”

Kasema, “Basi unasema jambo lile lile?”

Yeye alisema, “Nitasema tu yale Mungu asemayo; si kitu kingine, hakuna kingine. Siwezi kuongeza neno moja Kwake, ama kuondoa Neno moja Kwake.”

Kwa hiyo usiku huo, katika maombi, Bwana alimjia katika ono. Akatoka akaenda asubuhi yake, akasema…

Kuna manabii wawili!

59 Mtu mkuu kuliko wote katika taifa, katika jeshi na macho ya taifa, alikuwa Zedekia. Yeye alikuwa ni nabii mkuu, kwa mfalme. Yeye alikuwa kiongozi wa manabii wengine wote, kwa madhehebu. Alifanywa, na madhehebu yake, kiongozi wa hao wote; labda waliosoma vizuri zaidi, wenye elimu zaidi, wanaostahili zaidi kupata kazi hiyo. Naye alitiwa mafuta na Roho Mtakatifu, kwa kuwa anaitwa “nabii.” Hakika, si nabii wa kawaida tu, yeye alikuwa nabii wa Kiebrania. Sasa mwangalie.

60 Zedekia akasema, “Bwana alinena nami, 'Tengeneza hizi pembe mbili za chuma,' mfano.” Nabii kwa kawaida hutoa mifano. “Akasema, 'Tengeneza pembe hizi za chuma.' Roho Mtakatifu aliniambia, 'Chukua hizi,' kule Kutiwa mafuta kulikonibariki.” Usifikiri jambo hilo kama kitu cha kafara, bali ni kuelezea jambo fulani. “Roho Mtakatifu anayenena kwa lugha kupitia kwangu, Yeye aliyenithibitisha, Yeye alisema, 'Chukua pembe hizi, na, kwa hizi, umwambie mfalme ya kwamba ataisukuma Shamu moja kwa moja kutoka nchini. Nami nitamrudishia ile nchi ambayo ni haki ya Israeli, kanisa.'”

Ndugu, hilo ni la kimsingi kabisa, ni kama tu Balaamu alivyokuwa hapa juu. Balaamu alikuwa akinena kimsingi tu kama Musa alivyokuwa. Musa … Nambari sahihi ya Mungu ni saba. Ndipo Balaamu akasema, “Nijengeeni madhabahu saba; dhabihu saba safi, maksai na kondoo dume saba.” Huko ni kunena juu ya kuja kwa Mwana wa Mungu. Kimsingi, alikuwa sawa tu kama ye yote wao.

61 Na huyu hapa Zedekia, sawa tu kimsingi, “Kwa maana nchi hii ni yetu. Sasa, hao Waashuri na Wafilisti kule wakijaza matumbo yao, ya watoto wao na kadhalika, adui yetu, na chakula ambacho watoto wetu wanakosa! Wakati, Mungu alitupa nchi hii!”

Ndugu, hiyo ni hoja nzuri. Nafikiri yeye angalilipazia jambo hilo sauti mbele ya Israeli, nao wangalipiga kelele kwa nguvu walivyoweza. Sasa, ninazungumzia habari za leo sasa. Natumaini mnanifuata. Kupiga mayowe yote, kupiga makelele!

62 Mnakumbuka Daudi Jumapili iliyopita? Mnaona? Ninyi huko nje kwenye redio, ama mahali palipo na mawasiliano haya ya simu; hamkupata Ujumbe wa Jumapili iliyopita, hakikisheni mmeupata. *Kujaribu Kumfanyia Mungu Kazi Bila Kuchaguliwa Kuifanya*, haidhuru inafanywa kwa uaminifu jinsi gani, nzuri, haipokelewi kabisa na Mungu. Mnaona?

Sasa, huyu hapa Zedekia, akidhani yuko sahihi.

63 Mikaya akasema, “Hebu nimwombe Mungu.” Kwa hiyo akashuka asubuhi iliyofuata akiwa na BWANA ASEMA HIVI. Alichunguza ono lake kwa Neno.

Sasa kama angalimwambia Zedekia, “Unajua yale nabii wa Biblia hapa alisema kingempata jamaa huyu?”

“Lakini si wakati huu, kwa sababu mtu huyu ni mtu mwenye heshima. Yeye anajaribu.” Usikose kulipata hili. “Yeye anajaribu kurudisha kwa kanisa mambo ambayo ni mali ya kanisa. ”Yeye anajaribu kulirudishia kanisa mali ya kanisa. Anajaribu kulirudishia mali yake,“ si mambo ya Kiroho; kama angejaribu kurudisha hayo, yeye angalilitikisa taifa hilo lote kama alivyofanya Eliya. Lakini, akijaribu kuwapa vitu vya kimwili, ”Tunamiliki mali. Sisi ni dhehebu kubwa. Sisi ni wafuasi wake. Sisi sote, ninyi watu wote, ninyi Waprotestanti, wote mnapaswa kujiunga nasi.“ A-ha.

Tunalifikia hilo katika muda kidogo. “Yote ni ndugu na dada, hata hivyo.” Sivyo! Hawajapata kuwa wala hawatapata kuwa, kwa Kanisa halisi na la Kweli la Mungu. Haiwezekani!

64 Angalia, yeye aliona lile ono. Na kwa hiyo akasema, “Mungu alinena nami.” Sasa, angalia, mtu huyo alikuwa mwaminifu. Yeye alisema, “Yeye alisema, 'Tengeneza pembe hizi, na uende kule mbele ya mfalme na usukume upande wa magharibi,'” ama mahali popote nchi ilipo kutoka mahali walipokuwa wamesimama. “'Sukuma, na hiyo itakuwa ni BWANA ASEMA HIVI, ya kwamba atashinda vita na kurudi, ushindi kwa ajili ya kanisa.' Mtawasukumia mbali!” Hilo liko karibu sana, sivyo? Kulikuwa na nini?

Huyu hapa Mikaya anashuka. Kasema, “Sasa wewe toa unabii wako.”

"Kwea! Lakini niliwaona Israeli kama kondoo, wametawanyika, hawana mchungaji." Whiu! Kinyume kabisa.

65 Sasa, ninyi ni kusanyiko. Sasa ni yupi yuko sahihi? Wote wawili, manabii. Njia pekee unayoweza kujua tofauti yao, ni, kulichunguza kwa Neno.

Kasema, "Unapataje jambo hili?"

Yeye alisema, "Nilimwona Mungu ameketi juu ya Kiti cha Enzi." Kasema, "Niliona baraza lote lililomzunguka."

Sasa kumbuka, Zedekia alisema tu kwamba alimwona Mungu, pia, na Roho yule yule. "Nilimwona Mungu. Yeye aliniambia nitengeneze pembe hizi kwa—kwa chuma. Nenda huko nje na kuyasukuma mataifa yatoke hapa, kwa maana hii ni yetu. Hao wengine hawana haki ndani yake." Wangefanya hivyo kama wangalikaa sawa na Mungu. Wangaliipata hiyo, bali walimwacha Mungu.

Hivyo ndivyo dhehebu lilivyo, kanisa. Lina haki ya mambo haya, bali mmedanganywa mkaondoka kwake, kwa sababu mliliacha Neno la Mungu na Roho wa Mungu, kutiwa mafuta, ili kulithibitisha Neno la wakati huu. Msikose kuupata Ujumbe huu.

66 Angalia kilichotukia sasa. Yeye alisema, "Nilimwona Mungu," Mikaya alimwona, "ameketi juu ya Kiti cha Enzi Mbinguni. Baraza lake lilikuwa limekusanyika karibu Naye. Akasema, 'Tunaweza kumtuma nani ashuke aende akamdanganye Ahabu, kuyatimiza maneno ya Eliya; nabii Wangu aliyethibitishwa. Nilinena ya kwamba angekuja. Naye Eliya alikuwa na Neno Langu. Na mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa. Sijali wanakuwa wa kisasa iliyoje, ama wanakuwa wema iliyoje, ama wanakuwa na elimu iliyoje, ama ni wakubwa iliyoje, Maneno Yangu hayatashindwa kamwe.'

"Na pepo wa uongo akatoka kuzimu, akaanguka magotini mwake, na kusema, 'Kama utaniruhusu tu, ninaweza kuwapa upako wangu, kuwafanya wafanye ishara ya aina yoyote ama maajabu, mradi tu Ninawaondoa kwenye Neno. Hata hatajua ya kwamba Hilo ni Neno Lako. Yeye atalipuuza, kwa ajili ya kupendwa na watu.'" Ndugu, nyakati hazijabadilika. Ndugu Neville, hiyo ni kweli. Mnakumbuka, hiyo ni kweli. "'Nitampata, nitamfanya afanye mambo yale yale wengine wao wanafanya. Nitamfanya atabiri, na kusema uongo.'" Ingewezekanaje kuwa ni uongo? Kwa sababu ilikuwa ni kinyume cha Neno.

67 Hebu chukua yo yote ya mabatizo haya ya uongo,*fulani na fulani na fulani* za uongo, sijali linavyosikika likiwa halisi, namna wanavyojaribu kuiga, ni uongo kama ni kinyume cha Neno la Mungu la wakati huu. Hiyo ni kweli kabisa.

Unasema, "Vema, yetu, vema, tulifanya *hivi*, na tunafanya *hivi*, na kanisa letu liko *hivi* na *vile*."

Sijali ni kitu gani. Kama ni kinyume na Neno lililoandikwa kwa ajili ya wakati huu, ni uongo. Mungu hatakuwa na uhusiano wo wote nalo, haidhuru ni aminifu iliyoje, ni la kielimu iliyoje, ni la akili iliyoje, linasikika la kweli iliyoje, linasikika ni zuri iliyoje, iwapo ni kinyume cha Neno la wakati huu. Tutaingilia jambo hilo ndani zaidi katika dakika chache, wakati ukituruhusu. Tusipofanya hivyo, tutalichukua tena usiku wa leo.

68 Angalia, yeye alikuwa mwaminifu, mtu mzuri, hapana shaka. Naye akasema … Halafu, vinginevyo, Mikaya alimwambia, si moja kwa moja mbele yake, bali kwa maneno mengine, "Umetiwa mafuta kwa roho wa uongo." Hilo si lingekuwa ni jambo la kumwambia askofu? Lakini yeye alifanya jambo hilo.

Na kwa hiyo askofu huyu akaja na kusema, "Hutakuwa na ushirika tena," na kumpiga kofi usoni. Kasema, "Unajua ya kwamba mimi ni mtu aliyethibitishwa. Kanisa langu lilinifanya kiongozi wa wake, jambo hili. Kura ya watu wengi wa Mungu ilinifanya hivi. Dhehebu langu lilinifanya hivi. Na Mungu alitupa nchi hii, Naye anakusudia iwe ni yetu. Nami nina BWANA ASEMA HIVI." Akampiga kofi, akasema, "Roho wa Mungu alienda upande gani aliponiacha?"

Mikaya alisema, "Utaona, moja ya siku hizi," wakati California iko chini ya bahari huko, na mambo haya yote. Mnaona? "Utaona ilipitia njia gani, wakati unaketi kwenye magereza ya ndani."

69 Sasa, Ahabu, utasema nini? "Ninaamini nabii wangu," akasema. Vipi kama alilichunguza tu Neno? Mnaona, yeye hakutaka kujiona amelaaniwa. Nisikilizeni! Hakutaka kujiona amelaaniwa. Hakuna mtu anayetaka.

Na dhehe … ndugu wa kidhehebu, hiyo ndiyo shida yako. Unataka kuwazia ya kwamba uko sahihi, wakati, unajua moyoni mwako, unapobatiza kwa kutumia jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," unasema uongo. Unajua wakati unapo- … unasema mambo hayo unayofanya, na kuchukua ushahidi wa kwanza, na mambo yote kama hayo, umekosea. Ushahidi wa kwanza unawezaje kuwa ni kunena kwa lugha, halafu unanena kinyume cha ahadi ya Mungu ya wakati huu? Inawezekanaje? Hutaki laana, sivyo? Lakini Hapa imeandikwa, ndivyo itakavyokuwa. Hiyo ndiyo ile alama ya mnyama, inafanana sana hata ingewapoteza Walioteuliwa kama yamkini.

70 Kila ishara, kila ajabu, mtu aliyetiwa mafuta, unabii, mambo ya kila namna yakiendelea; kila namna ya ishara, kila namna ya maajabu, utajuaje tofauti yake? Angalia Neno la wakati huu. Hivyo ndivyo unavyochukua …

Mwangalie Musa, jinsi ambavyo angalimwambia Balaamu. Mwangalie Mikaya hapa, tulijuaje alikuwa sahihi? Neno, kabla yake, lilikuwa limetabiri jambo hilo kwa ajili ya Ahabu.

Na Neno, mbele yetu, lilitabiri madhehebu haya kwa ajili ya siku hii, na laana hii juu yao. Na mambo ambayo yangetukia kwa Kanisa Lake lililotiwa mafuta kweli kweli, litakuwa na Neno, Bibi -arusi Neno. Tuko hapa. Hili hapa, leo, sawasawa tu na ilivyokuwa wakati huo.

71 Biblia ilisema, "Kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitishwe." Nilinena juu ya Balaamu, nilinena juu ya Balaamu na juu ya Musa. Nami nimenena sasa juu ya Mikaya na Zedekia. Sasa nitatoa moja zaidi. Ambapo, kuna mamia ya hao, bali mmoja zaidi, kuwafanya mashahidi watatu. Nina mfuatano mzima wao ulioandikwa hapa; bali kuokoa wakati.

Yeremia ambaye alikuwa amethibitishwa, amekataliwa, bali nabii wa Mungu aliyethibitishwa. Walimchukia mtu huyo. Walimtupia yasiyo...matunda yaliyooza, na kila kitu kingine. Naye akaweka laana juu yao. Na mambo aliyofanya, na akalala huko nje kwa ubavu wake, na kadhalika, na kutoa ishara ya kwamba Israeli ilikuwa imekosea.

Kila nabii, nabii wa kweli aliyewahi kuinuka ulimwenguni, alilaani mashirika hayo ya madhehebu ya kanisa. Yangewezaje kubadilika, kwa Mungu asiyebadilika?

Roho Mtakatifu ndiye Nabii wa wakati huu; Yeye analihakikisha Neno Lake, akilithibitisha. Roho Mtakatifu alikuwa ndiye Nabii wa wakati wa Musa. Roho Mtakatifu alikuwa ndiy Nabii wa wakati wa Mikaya. Roho Mtakatifu, ambaye aliliandika Neno, huja na kulithibitisha Neno.

72 Sasa ni jambo gani lililotukia katika wakati wa Mikaya? Ahabu aliuawa, na mbwa wakairamba damu yake, kulingana na Neno la Mungu.

Enyi walimu wa uongo nyote, ndivyo anavyosema Mungu, siku moja mtavuna mnayopanda, enyi viongozi vipofu wa vipofu! Sina hasira. Ninawaambia tu Kweli. Na nisingelisema jambo hili kama hapa, kwenye kile chumba, kama Roho Mtakatifu hakusema, "Liseme kwa namna hiyo." Je! nimepata kuwaambia jambo lo lote lisilo kweli ila lile Mungu alilothibitisha kuwa ni kweli? Amkeni, ndugu zangu, kabla ya kuchelewa sana!

73 Lakini hebu niseme jambo hili. Bali hebu niseme jambo hili. Mwiba ungewezaje kuamka kisha uwe mchongoma, wakati ulikusudiwa tangu asili kuwa hivyo? Wateule wangewezaje kutoliona jambo hilo? Kwa sababu, mmechaguliwa kuliona. "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu," alisema Yesu, "lakini hakuna mmoja wao anayeweza kuja isipokuwa Yeye amenipa Mimi huyo tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, hapo majina yao yalipowekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo," si kwenye kasisi wa mtaa wa kanisa, bali kwenye Kitabu, Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo.

74 Angalia, Yeremia alisimama, alithibitishwa mbele ya watu, hata hivyo walimchukia.

Na kwa hiyo wakaondoka wakatengeneza nira, yeye aliitengeneza, na kuiweka shingoni mwake, akaondoka akaenda mbele za watu. Walisema, "Loo, sisi ni watu wakuu wa Mungu. Mbona, sisi ni Israeli. Sisi ni waaminifu sana kwenye sinagogi letu! Tunahudhuria kila Jumapili, sisi, tunatoa dhabihu, na tunalipa pesa zetu. Nebukadreza anawezaje kushikilia mambo matakatifu ya Mungu?" A -ha! Dhambi zako zilikuwa zimefanya jambo hilo.

Mungu alisema, "Kama mtazishika amri Zangu, sitafanya hili. Lakini, msipozishika, linawajia." Hiyo ni kweli kabisa. Bado ni vile vile. Shika amri Zake, Neno Lake kwa ajili ya wakati huu, yale aliyoahidi.

75 Sasa angalia. Sasa, Yeremia, kwa mapenzi ya Mungu, nabii aliyethibitishwa, ingawa alichukiwa … Kila mmoja wao alichukiwa katika siku zao. Walifanya mambo hayo ya ajabu sana kinyume na madhehebu ya siku hiyo, kila mmoja alimchukia, hata wafalme na chochote kile. Kwa hiyo akaweka nira shingoni mwake, na kusema, "BWANA ASEMA HIVI. Mtakaa huko miaka sabini," maana yeye alifahamu kutokana na Neno la Mungu. "Miaka sabini!"

76 Ndipo Hanania, Hanania, nadhani mnalitamka, H-a-n-a-n-i-a. Hanania, nabii miongoni mwa hao watu, akatokea, akaiondoa ile nira hiyo shingoni mwa Yeremia, na kuivunja. Kisha akasema, awe mtu mkubwa miongoni mwa watu, unaona, wakati alipokuwa akinena kinyume cha Neno la Mungu. Naye akasema, "Miaka miwili watarudi. BWANA ASEMA HIVI."

Manabii wawili waliopakwa mafuta. Tofauti yao ilikuwaje? Mmoja alikuwa ananena Neno, na huyo mwingine hakunena Neno. Yeremia akasema, "Amina."

77 Mbele ya wazee wote na kusanyiko, Israeli wote, mnaona, alitaka kuonyesha angeweza kuwa

mkubwa tu kama Yeremia. "Unajua hawakupendi, kwa vyo vyote. Kwa hiyo mimi ni nabii, pia. Mimi ni nabii zaidi ya ulivyo wewe, kwa maana wewe unatabiri uongo. Unaniambia watu wa Mungu watakuwa chini ya kitu *hiki* na *hiki?*"

Hivyo ndivyo wanavyosema leo, bali mtakuwa huko hata hivyo, kama kanisa. Mmelaaniwa kwa laana. Ninyi makanisa yote, madhehebu yanashikilia mapokeo yao ya mwanadamu badala ya Neno la Mungu, mmelaaniwa na Mungu.

78 Sasa angalia, huyu hapa anakuja. Hanania anatoa kwa nguvu nira hii kutoka kwenye shingo yake, ishara ya Mungu, akaivunja, akasema, "BWANA ASEMA HIVI. Miaka miwili watarudi." Ni kwa kujionyesha tu, "Mimi ni Fulani." Kwa sababu alisimama ndani, yeye alikuwa nabii wa kimadhehebu.

Yeremia alikuwa mtu wa jangwani aliyeishi peke yake. Yeye alitabiri mabaya dhidi yao wakati wote, maana walikuwa waovu.

Na mtu huyu alikuwa akiwaambia, "Loo, mko sawa mradi tu mu wafuasi. Mradi tu wewe ni Israeli, hilo tu ndilo muhimu. Mnaona, ninyi, sisi … Mungu hatafanya jambo hilo. Najua kuna kitu kidogo kilichotendeka hapa, lakini msiwe na hofu, msiogope."

Loo, ndugu, wangali wanaishi leo. "Msijali, kila kitu ni sawa. Tumedhibiti kila kitu. Sisi ni Kanisa." Msiwazie hayo. Naam.

79 Kwa hiyo akasema, "Kila kitu ni sawa. Watarudi baada ya miaka miwili. Hilo ni jambo dogo lililotukia. Si jambo lisilo la kawaida. Tuna jambo hilo. Ni Nebukadreza tu aliyekuja hapa, bali Mungu wetu atashughulikia haya yote."

Bali Neno lilisema wao watakuwa huko miaka sabini; hata kizazi hicho kiwe kimepita, na kizazi kingine. Miaka arobaini ni kizazi kimoja. "Hii ni karibu vizazi viwili mtakuwa huko chini." Naye Yeremia alisema jambo hilo kulingana na Neno la Mungu.

Hanania alivunja hilo! Yeremia alisema, "Vema. Amina. Lakini, Hanania, hebu na tukumbuke jambo hili, sisi sote wawili ni manabii. Sisi ni wahudumu."

Nami ninawaambia jambo hili, ndugu yangu. Hebu na tukumbuke kumekuwa na manabii waliotutangulia, nao walitabiri juu ya falme, tena wakatabiri dhidi ya mambo fulani Lakini, kumbukeni, wakati nabii aliposema jambo lo lote, hana budi kutabiri kulingana na Neno. Kama vile Mikaya, na Musa, na hao wengine wote. Haina budi kuwa kulingana na Neno. Kama sivyo, basi kumbukeni kilichotukia.

80 Ndipo, Hanania, hasira yake ya haki ikainuka. "Mimi ni Hanania" (hapana shaka), "nabii wa Bwana, nami ninasema, 'Miaka miwili.'" Kwa maneno mengine, "Sijali Neno linasema nini." Upako wake mafuta, "Ninasema, 'Miaka miwili, watarudi.'"

Yeremia akaondoka mbele yake, akatoka nje akasema, "Bwana, Sijali alisema nini, ningali ninaamini na kujua ya kwamba Neno hilo linasema hivyo. Nitadumu mwaminifu Kwako. Sitadanganywa naye."

Mungu alisema, "Nenda ukamwambie Hanania, 'Nitaitengeneza kwa chuma, nira inayofuata.'" Kwa sababu alifanya jambo hilo, aliondolewa kwenye uso wa nchi, Hanania alichukuliwa, mwaka uo huo.

Hiyo hapo mifano yetu, wote wawili manabii. Wengi sana wangeweza kusemwa na kuzungumziwa wakati huu.

81 Lakini angalia. Yesu alisema, ya kwamba, katika wakati huu wa mwisho, tena, hizo roho mbili zingefanana sana tena. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Sasa angalia. Zitafanana sana kuliko hizo zilivyokuwa. Huu ni wakati wa mwisho. Loo, enyi watoto! Mungu na uturehemu! Mpaka, "Hata ingefanana sana hata ingewapoteza hata Walioteuliwa kama yamkini." Sasa utalitambuaje, tulilitambuaje katika siku hizo? Utaliambiaje leo? Namna ile ile, dumu na Neno. "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele."

Sasa jali Ujumbe huu wote. Na wakati mtakaposikiliza kanda, hata labda nitakuwa nimeondoka siku moja wakati Bwana atakapomaliza nami hapa duniani, mtarejea kwenye jambo hili. Sikilizeni sauti yangu, yale ninayowaambia. Kama akinichukua kabla ya Kuja Kwake, kumbuka tu, nimezungumza nawe katika Jina la Bwana, kwa Neno la Bwana. Ndiyo.

82 Angalia, "Kuwa karibu sana hata ingewapoteza walio Wateule kama yamkini," wangefanya ishara zile zile, miujiza ile ile, kwa Roho yule yule. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Kama vile wale manabii walivyokuwa ambao ndiyo kwanza tuzungumze habari zao, manabii. Sasa, pia imeandikwa …

Hebu tufungue, kwa ajili ya hili, kama mkitaka, Timotheo wa pili 3 Hebu na tusiliache hili. Nami sitaki kuninii …

Ninaiangalia ile saa ya ukutani pale, nami na—nataka kuacha mengi sana yake, nami sifikiri

tunapaswa kufanya jambo hilo sasa. Mnaona? Angalia. Ninii tu … Kama nimesimama hapa, nikitokwa na jasho, mnaona, lakini nina furaha. Nami ninajua ya kwamba hii ni kweli. Timotheo wa Pili 3:8.

83 Paulo, yule mtu aliyesema, "Kama Malaika akija kutoka Mbinguni na kunena neno lingine lo lote kwenu kuliko lile nililosema, na alaaniwe," naam, Malaika ashuke aje. Hiyo ni Wathesalonike wa Pili … Loo, samahani.

Angalia katika Timotheo wa Pili 3:8. Mwangalie Paulo akinena sasa. Hebu tuanze na karibu … Hebu tuanzie kwenye aya ya kwanza, na sikilizeni sasa kwa makini sana. Ninyi mlio na Biblia zenu, soma pamoja nami. Ninyi msio na Biblia zenu, sikilizeni kwa makini. Ninii …

*Lakini ufahamu neno hili, ya kuwa siku za mwisho ...*

Pigia hilo mstari, *"siku za mwisho."* Hapo ndipo litakapotukia.

*... kutakuwako nyakati za hatari.* (Tuko ndani yake.)

*Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi,*

84 Angalia kundi hili tulilo nalo leo, limeoza. Hata watu barabarani, vijana wanaume, wakizivuta nywele zao chini kwenye vipaji vya nyuso zao, kama vile kuzikata kukingama uso kama mwanamke. Upotovu! Wasodoma!

Je! Ulisoma katika mwaka huu, Reader's Digest ya mwezi huu? Imesema, "Wamarekani kwenye umri," ambao nafikiri ulikuwa, "kati ya ishirini na ishirini na mitano, tayari wako katika hali yao ya umri wa makamu." Wamekwisha! Wameoza! Sayansi inasema ya kwamba, ya kwamba mwanamume yuko katika umri wake wa makamu, na mwanamke, wakati wangali bado kwenye umri wa miaka ya mwanzoni ya ishirini na kitu. Miili yao imeoza sana na imetolewa kwa uchafu.

85 Loo, Marekani, ni mara ngapi Mungu angewafunika, bali sasa saa yenu imewadia! Mnauongoza ulimwengu kwa uchafu.

*... wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi,*

*Wasiowapenda wa kwao,…*

Hawana upendo wa kweli hata mmoja kwa mwingine, mwanamume kwa mwanamke, mwanamke kwa mwanamume. "Hata hawawapendi wa kwao." Wachafu, kujuana kimwili!

*…wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wakali na wasiopenda mema,*

Kwa maneno mengine, tuseme, "Enyi kundi la watakatifu wanaojifingirisha." Mtu fulani aliuliza hivi majuzi kuhusu kuja hapa kanisani. Kasema, "Usiende kule. Yote kwa jumla ni kundi la makelele na lisilo na adabu."

"wasiowapenda wa kwao"

wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu;

Mnasema, "Ndugu Branham, hao ni wakomunisti." Kifungu kinachofuata kinasema nini?

*wenye mfano wa utauwa, lakini* (nini?) *wakikana nguvu zake:* (Neno, Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, amedhihirishwa, ile ahadi ya siku hii) …

Ni kama tu vile Hanania, hasa kabisa kama Zedekia, kama hasa Balaamu, kurudi nyuma, manabii wengine wa uongo.

*Wenye mfano wa utauwa,* waliotiwa mafuta … Mnaona?

*Wenye mfano,* waliotiwa mafuta, wahudumu waliowekwa wakfu …

*Wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana* ya kwamba ni yeye yule jana, leo … Wakilikataa Neno Lake!

Wao walimkataaje Yesu katika siku hiyo? Walimkana nani walipomkataa Yesu? Lile Neno. Walikuwa wa kidini. Walifundisha kutoka kwenye Biblia yao, bali walikana Neno la siku hii.

Wao ni nini leo? Kitu kile kile, wametiwa mafuta, wakihubiri Injili ya Pentekoste, bali wakiikana ahadi ya siku hii ya Neno kuthibitishwa, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Mnaliona? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

*Kwa maana katika hao wamo wale wajiingizao katika nyumba za watu, na kuchukua*

*mateka wanawake wajinga wenye mizigo ya dhambi, waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi;*

"Karamu zetu za kushona na fulani-na-fulani wetu." Mtu fulani anakuja akijaribu kufasiri Neno vibaya, na kusema jambo hili, "Ni sawa, dada, kwako kuwa na nywele fupi. Usimjali mpumbavu yule. Mnaona? Ama, kama u—unavaa hii; si kwamba, 'kile kinachotoka moyoni mwa mtu ndicho kinachomtia unajisi.'" Mnaona? Basi unatambua ya kwamba umetiwa mafuta na roho mwovu wa tamaa mbaya na mchafu? Tahadhari, huenda ukaimba kwenye kwaya, ukiwa na nywele fupi, bali una pepo mchafu. Hilo ni kinyume na Neno. Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Nawe unasema, "Vema, ninavaa kaptura. Hainihukumu."

"Mtu ye yote, mwanamke akivaa vazi linalompasa mwanamume, ni chukizo mbele za Mungu." Mungu asiyebadilika alisema hivyo.

86 Loo, mambo mengi sana, tungewezaje kuyapitia; wakati wetu ungekuwa umekwisha. Lakini unajua vya kutosha kujua lililo jema na baya. Na ninawezaje kuwafanya wafanye hivyo? Ninawezaje kufanya jambo hilo? Kusema, "Vema, mnafanya nini?" Mimi ni shahidi dhidi yenu. Siku moja, katika Siku ya Hukumu, hamtakuwa na kona ya kuingia.

87 Mikaya angewezaje kukomesha jambo hilo? Musa anawezaje; akipiga makelele, akijaribu kulikomesha, huku Yoshua na hao wengine wakikimbia miongoni mwa watu, halafu Lawi akauvuta upanga wake akawaua, hata hivyo? Waliendelea vivyo hivyo.

Imetabiriwa ya kwamba watafanya jambo hilo. Nao watalifanya, kwa maana ni BWANA ASEMA HIVI watafanya hivyo. Unafikiri hayo madhehebu yatavunjika kamwe, madhehebu yao yalirudie Neno? Ni BWANA ASEMA HIVI, hawatafanya hivyo! Wataingia katika mpinga -Kristo? Kweli kabisa. Ni BWANA ASEMA HIVI, wataingia! "Kwa hiyo unasema nini?" Sina budi kuwa shahidi, na vivyo hivyo nanyi, waamini wote. Angalia.

*… wanawake wajinga waliochukuliwa na … tamaa za namna nyingi,*

88 "Vema, wanawake wengine wote hufanya jambo hilo." Manabii wa uongo! Sasa sikilizeni. Manabii wa uongo, ninaowazungumzia. Sasa watafanya nini katika siku ya mwisho?

*… kuchukua mateka wanawake wajinga wenye mizigo ya … waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi,*

"Vema, ninajua wanawake wengine wote …" Vema, endelea.

Nilisema nini kabla tu ya tukio hili kubwa hapa California? "Ninyi watu hapa Los Angeles, kila mwaka ninaporudi kuna wanawake wengi zaidi waliokata nywele zao na wanaume dondoadume kuliko waliokuwemo kwanza, wahubiri wengi zaidi wakiingia katika madhehebu. Hamna udhuru! Kama zile kazi kuu zilikuwa zimefanywa katika Sodoma na Gomora zilifanywa kwenu, ungekuwa umesimama hata leo. Loo, Kapernaumu, wewe unayejiita kwa jina la malaika, Los Angeles!" Mnaona kile kinachotendeka? Unazama moja kwa moja kwenye kilindi cha bahari. Lini? Sijui utazama lini, bali unazama. Enyi vijana, kama nisipoliona katika siku yangu, angalieni. Ameondoka!

*wakijifunza siku zote, ... ila wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa kweli.*

Sasa hili hapa jambo la kustusha sana, hii hapa sehemu ya kustusha sana. Sikilizeni hili.

Na kama vile Yane na Yambre walivyopingana na Musa, vivyo hivyo na hawa wanapingana na ile kweli; ni watu walioharibika akili zao, wamekataliwa kwa mambo ya imani *waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu, bila shaka.*

"Kuhusu Imani." "Naye ataigeuza Imani ya baba, ama watoto, iwarudie baba zao."

89 "Wamekataliwa kwa mambo ya Imani." A -ha! Mnajua maana ya waliokataliwa? Kama una Biblia ya Scofield, kuna "h" pale. Papo hapo, inasema, "ukengeufu." Ukengeufu, hivyo ndivyo ilivyo.

90 Sasa, hebu kidogo. Ninataka kuangalia kitu fulani hapa. Nafikiri niliandika jambo hili vizuri. Sina hakika, bali nataka kusema jambo hilo, na niliangalie kabla si—sijalisema. Sasa, dakika moja tu. [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] Wamekataliwa kwa mambo ya Ukweli, kwa mambo ya Imani." "Imani," kuna Imani moja tu. Hiyo ni kweli. "Kwa mambo ya Imani, wamekataliwa!"

Sasa nataka kusoma Luka 18. Hebu kidogo. Huna … Unaweza kuliandika; haikubidi kusoma.

*Akawaambia mfano, ya kwamba imewapasa kumwomba Mungu sikuzote, wala wasikate tamaa.*

*Akasema—akasema, Palikuwa na kadhi katika mji fulani, hamchi Mungu, wala hajali watu.*

*Na katika mji huo palikuwa na mwanamke mjane, aliyekuwa akimwendea-endea, akisema, Nipatie haki na adui wangu.*

*Naye—naye kwa muda alikataa; halafu akasema moyoni mwake, Ijapokuwa simchi Mungu wala sijali watu,*

*Lakini, kwa kuwa mjane huyu ananiudhi, nitampatia haki yake, asije ... akanichosha kwa kunijia daima.*

*Bwana akasema, Sikilizeni asemayo yule hakimu dhalimu.*

*Na Mungu, je! Hatawapatia haki wateule wake ... wanaomlilia mchana na usiku, naye ni mvumilivu kwao?*

*Nawaambia, atawapatia haki upesi; walakini, atakapokuja Mwana wa Adamu, je! Ataiona imani duniani?*

91 Sasa hilo ndilo swali. Hapa ndipo nilipotaka kufika, katika Ufunuo 10. Tutalifikia katika dakika chache, kwenye aya nyingine ya Maandiko. Yeye alisema, "Katika siku za Ujumbe wa malaika wa saba, siri za Mungu zinapaswa kutimizwa." Swali ndilo hili, ni, kama ukifuatia kwenye mstari huo katika saa hii itatimizwa? "Nitaiona Imani?" Malaki 4 itatimizwa katika wakati huu, "Kuirudisha Imani ya watoto, ielekee Imani ya baba zao, ile ya asili, lile Neno"? Mnaona?

92 "Waliokataliwa, Yane na Yambre, waliposhindana." Sasa, pia, sikilizeni, 2 Timotheo 3:8. "Kama vile Yan-…walivyoshindana na Musa, pia katika siku za mwisho wawa hawa waliokataliwa wangekuja," sasa angalieni mahali linaposema hapa, "wakiwa na mfano wa utauwa," waliotiwa mafuta. Sasa hebu na tu … Rudini m—mkasome hilo mtakaporudi nyumbani, ili kwamba niweze kuumaliza huu, asubuhi ya leo, nikiweza. "Waliokataliwa kwa mambo…" Si waliokataliwa katika—katika—katika maisha; wao ni sawa, watu wastaarabu.

93 Sasa angalia wakati Musa aliposhuka kwenda Misri, akiwa na Ujumbe wa BWANA ASEMA HIVI, naye alithibitishwa; akawaita Israeli, waliokuwa ni watu, si kanisa. Israeli walikuwa ni watu; kamwe hawakuwa kanisa. Maana, neno *kanisa* linamaanisha "walioitwa watoke." Walikuwa ni watu wa Mungu. Ndipo walipotiwa mafuta chini ya Neno, na kuitwa watoke, wakawa kanisa la Mungu. Ndipo wakarudi nyuma, kwa maana hawakuamini Neno la Mungu, na wakamsikiliza nabii wa uongo. Natunaimini hilo linazama ndani.

Israeli, wakiwa ni watu wa Mungu, walitoka chini ya mkono wa Mungu, wamepakwa mafuta na Neno … kwa Nguvu za Mungu, waliona ishara na maajabu ya Mungu. Na wakati Mungu alipokuwa akiendelea pamoja nao, nabii wa uongo akaingia, ametiwa mafuta, akawafundisha jambo fulani kinyume cha Neno la Mungu la asili walilokuwa wamesikia; kisha kila mmoja wao akaangamia jangwani, ila watu watatu. Sasa lishikilia jambo hilo.

94 "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ambapo watu wanane waliokolewa kwa maji, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ambapo watatu walitoka Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika wakati atakapofunuliwa Mwana wa Adamu." Mimi ninanukuu tu Maandiko, Neno la Bwana, ambalo, "Mbingu na nchi zitapita …" Itakuwa ni wachache!

95 Angalia hapa. Musa anashuka kwenda kwa Haruni. Musa alipaswa kuwa Mungu. Mungu alimwambia awe Mungu, akasema, "Wewe uwe Mungu, na hebu Haruni ndugu yako awe nabii wako. Weka maneno yako katika kinywa chake kama huwezi kuzungumza vizuri." Kasema, "Lakini ni nani aliyemfanya mwanadamu bubu? Ni nani aliyemfanya mwanadamu kunena?" Bwana alifanya hivyo.

Ndipo akashuka akaenda kule. Alifanya nini? Alifanya muujiza wa kweli na wa haki ambao Mungu alimwambia afanye. Mungu alimwambia aafanye, "Nenda ukatupe fimbo yako chini." Akaichukua, nayo ilikuwa nyoka. Akaiokota, kisha akageuka ikawa fimbo. Kasema, "Nenda ukafanye hivyo mbele ya Farao, na useme, 'BWANA ASEMA HIVI.'"

Basi Farao alipoona jambo hili, tunasema, "Naam, ni ujanja duni vipi wa kiganga." Kasema, "Hakuna kitu. Ni kuwasiliana kimawazo ama kitu fulani, mwajua. Tuna watu katika madhehebu yetu wanaoweza kufanya jambo lile lile. 'Njoo hapa, Askofu Fulani. Na, wewe, njoo hapa.' Tunao wanaoweza kufanya jambo lile lile." Huyo alikuwa ni Shetani akinena kupitia kwa Farao.

Huyo alikuwa ni Mungu akinena kupitia kwa Musa.

96 Lakini mwangalie jamaa huyu akitoka. Yane na Yambre wakatoka wakaja mbele ya Musa, na hadharani mbele ya watu, na kufanya kila muujiza ambao Musa angeweza kufanya. "Watawapoteza Walio Wateule kama yamkini." Hiyo ni kweli? Wakafanya jambo lile lile alilofanya Musa. Mnalipata? Sasa kumbuka, ni MAANDIKO YASEMA HIVI, ya kwamba jambo hilo litajirudia tena katika siku za mwisho.

Kulikuwa na tofauti gani kati ya Musa na Yambre?

Musa alisema, "Damu na ije katika maji."

Nao hawa manabii wa uongo wakasema, "Bila shaka, sisi hutia damu katika maji, pia." Nalo likatukia.

Kwa hiyo Musa akasema, "Viroboto na waje." Alikuwa akilitoa wapi? Moja kwa moja kutoka kwa Mungu. Mnaona?

Naye alifanya nini? Akasema, "Vema, hakika, tunaweza kuleta viroboto, pia." Nao walifanya hivyo. Muujiza wo wote ambao Musa angeweza kufanya, wao wangeweza kufanya, pia!

Kumbukeni, wekeni hilo moyoni mwenu, tutalifikia, baada ya kitambo kidogo. Wao wanaweza kufanya jambo lo lote wale wengine wanaloweza kufanya, bali wao hawawezi kudumu na Neno. Hawawezi kudumu na Neno.

97 Sasa angalia, wao walifanya jambo hilo. Lakini Musa, nabii wa kweli aliyetumwa kutoka kwa Mungu, aliyeagizwa na Mungu, yeye kamwe hakushindana nao, kasema, "Hapa, huwezi kufanya jambo hilo! Huwezi!" Yeye aliwaacha tu peke yao, aliwaacha tu waendelee. Wao ni manabii wa kimadhehebu, bali waendelee tu.

Musa aliendelea tu moja kwa moja, akamsikiliza Mungu. Chochote Mungu alichosema, "Sasa fanya jambo *hili*," Musa alienda na kulifanya. Yeye alifanya jambo jipya. Walipofanya hivyo, kila mmoja wao alikuwa na msisimko ama kitu fulani, hawa hapa wanakuja. Walifanya hivyo, pia, kama vile tu Musa alivyofanya.

98 Sasa angalia. Watu hawa walitokea … Loo, enyi watu, msikose jambo hili! Hawa wadanganyifu, waigaji, walitokea baada ya yule wa kweli kutokea kwanza. Mnaona? Walikuja kuiga. Mnaona, hawana budi kufanya hivyo. Ibilisi hawezi kuumba chochote; yeye ni mpotoshaji tu wa asili.

Na dhambi ni nini? Ni haki iliyopotoshwa. Uzinzi ni nini? Tendo sahihi lililopotoshwa. Uongo ni nini? Ukweli ulioelezewa vibaya. Upotovu!

Mwangalie Hanania, upotovu wa Neno la asili. Mwangalie Balaamu, upotovu wa Neno la asili. Mwangalie Zedekia, upotovu wa Neno la asili.

Na Biblia ilisema ya kwamba jamaa hawa wangetokea, baada ya, yule mpotoshaji, ... kupotosha Neno la asili, lililothibitishwa na kuhakikishwa kwamba ni Kweli.

99 "Fanya kazi ya mhubiri wa Injili," pembeni kule, "timiliza huduma yako. Kwa maana utakuja wakati watakapoyakataa Mafundisho yenye uzima, ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana maskio ya utafiti; na waendelee na kufanya lo lote wanalotaka, na, 'Ni sawa, tuna ishara zile zile na maajabu.' Nao watajiepusha wasisikie yaliyo Kweli, na waingizwe katika hadithi za uongo, mafundisho ya sharti."

100 Loo, kule kumhisi Roho Mtakatifu, ule uchaji unaoigusa nafsi ya mwanadamu wakati anaposimama ili kuwazia jinsi lilivyo halisi na dhahiri moja kwa moja mbele zetu! Chimbueni lile jiwe la pembeni hapa nje na msome kipande cha karatasi kilichowekwa kule miaka thelathini na mitatu iliyopita. Tazama alilosema Yeye kule kwenye—kwenye Barabara ya Saba, asubuhi hiyo wakati lilipowekwa hili jiwe la pembeni. Sasa angalieni. Sasa liangalieni. Angalieni hapa chini mtoni, wakati Malaika wa Mungu aliposhuka katika mfano wa Mwali wa Moto, mamia ya makanisa, ama watu wa kanisa, wakisimama ukingoni; yale Yeye aliyosema, angalieni kama yametimia. Angalia kilichotukia.

Ni vigumu sana. Ninajua inaonekana ni vigumu, ndugu, huko nje. Lakini ni … Biblia ilisema, Yesu alisema Mwenyewe, "Ingewapoteza walio Wateule kama yamkini." Hakuna njia ya kulizunguka. Wao hawataweza kuliona kamwe. Kama ingaliwezekana, Walioteuliwa wangepotezwa nayo.

101 Angalia, jamaa hawa walitokea baada ya mtiwa mafuta wa kweli wa Mungu kutumwa; kwa nabii Wake wa kweli, Musa. Na kila Musa alipofanya jambo lo lote, wao wangeliiga hilo.

102 Sasa, ndugu, dada, mimi … Hili ni kanisa langu mwenyewe. Nina haki ya kuhubiri ninalotaka, mradi tu linatoka katika Neno la Mungu. Nami siwahukumu ninyi watu, bali hebu tuchunguze hilo kwa wakati na saa tunayoishi sasa.

Salamu kwa Ndugu Ruddell, kwa Junior Jackson, na wengineo hapa nje, makanisa yetu ndugu. Niliwasahau, muda mfupi uliopita. Nafikiri wameunganishwa asubuhi hii, pia, kwa sababu hakuna—hakuna nafasi kanisani.

103 Hebu wazia tu jambo hilo sasa, kwa dakika moja tu. Walifanya miujiza ile ile ambayo Musa alifanya. Musa alileta viroboto; waliigiza na kuleta viroboto. Mnaona?

Mungu alisema, "Siku utakayokula, siku hiyo utakufa."

Shetani alikuja na kusema, "Hakika, humtakufa. Mtakuwa na hekima zaidi. Mtakuwa na madhehebu bora, bora…" Mnajua. "Unajua, kila kitu kitakuwa bora kwako, mtakuwa na Nuru zaidi." Mnaona, upotovu tu. Inapaswa …

Kisha kumbukeni, BWANA ASEMA HIVI, kulingana na Timotheo wa Pili 3:18, ya kwamba, "Katika siku za mwisho, ya kwamba hawa Yane na Yambre wangekuwa duniani." Sasa, ninawatakeni mwone kuna wawili wao, mnaona, waigaji.

Sasa tutarudi Sodoma, baada ya kitambo kidogo, hao watatu, tuwaone hao Malaika watatu walioshuka wakaja, na tuone kule kuigiza, na kadhalika, mnaona, tuone ni nani wa kweli na ni nani wa uongo. Mnaona? Mnaona?

104 Angalia, walifanya miujiza ile ile. Lakini, angalieni, wao waliigiza baada ya Neno la Kweli kutiwa mafuta, na yule wa kweli aliyetumwa na Mungu; wakafuata, ni wa pili.

Sijui kama tungeweza kuwazia kwa dakika moja. Kule kuwashika watu kwa mkono, si muda mrefu uliopita, yapata miaka ishirini iliyopita, na ishara ikaonyeshwa. Jamani, kulikuwa na ishara nyingi zaidi katika vitu vyote, na kila mtu… Mmoja anayo kwenye mkono wake wa kulia; mmoja anayo kwenye mkono wake wa kushoto; yule mwingine huisikia harufu. Mnaona, kila namna ya … Nami nashangaa … Mungu hataniruhusu niwaambieni katika wakati huu lililokuwa kweli, bali siku moja mtatambua. Hiyo ilikuwa tu ni kufanya upumbavu wao udhihirike. Hilo halikuwa sahihi, hapo mwanzo. Nitawaambia, siku moja, Bwana akiruhusu.

105 Angalia, walifanya miujiza ile ile, bali hawakuninii … Angalia, hawakufanya hivyo mpaka baada ya Neno la asili kutoka, kwanza. Hivyo ndivyo Shetani alivyofanya katika bustani ya Edeni. Hivyo ndivyo alivyofanya wakati wote. Ni nani aliyetabiri kwanza? Musa. Ni nani aliyejitokeza kwenye tukio kwanza, Musa ama Balaamu? Musa. Ni nani aliyejitokeza kwenye sehemu ya tukio kwanza, Yeremia ama Hanania? Mnaona ninalomaanisha? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

Angalia, waliiga. Waigaji wa kimwili, waaminifu, wakifikiri walikuwa "wanamfanyia kazi Mungu," kama Daudi alivyofanya, juma lililopita, lakini ni kuiga kimwili. Ninangojea tu kwa dakika moja. Ninawatakeni mfikirie katikati ya mahali hapa. Kama silisemi, bila shaka Roho Mtakatifu atawafunulia, hasa kwa walioteuliwa. Mnaona?

106 Dhehebu la Farao linasema, "Tuna mtu anayeweza kufanya jambo hilo hilo," nao walililifanya. Mnaona? Kwa nini Farao alifanya jambo hili? Kwa nini Mungu aliruhusu jambo hilo? Kwa nini Mungu akamtuma nabii wa kweli na aliyetiwa mafuta kule kufanya ishara mbele za Farao, halafu aiache nakala ya kimadhehebu ije na kuinakili mbele za watu? Kwa nini amwache mwigaji ainuke afanye jambo hilo, na kufanya jambo lile lile hasa ambalo Roho halisi wa Mungu alifanya? Mnaona, Maandiko hayana budi kutimizwa.

107 Angalia, Yeye alifanya jambo hili kusudi apate kuufanya mgumu moyo wa Farao na Wamisri, kuthibitisha ya kwamba Musa hakuwa ndiye tu aliyekuwa na Neno. Wangeweza kufanya kila kitu kama vile tu Musa angeweza kufanya.

Na kwa nini Mungu aliruhusu jambo hili litukie katika siku za mwisho? Kwa hiyo, jambo lile lile kama roho wa uongo alivyomwambia Zedekia, "Tutamtoaje Ahabu huko nje, kuyafanya mambo haya kutimia?" Yeye atawapataje watu hawa, wanaoyatumaini makanisa yao, kutoka hapa na kuyafanya mambo haya yatimie, ambayo Yeye aliyabashiri? Wao, katika Wakati huu wa Kanisa la Laodikia, "Kwa maana unasema ya kwamba u 'tajiri, na huna haja na kitu.' Niliketi kama malkia.' Huna kitu! Hujui ya kwamba u mwenye mashaka, mnyonge, kipofu? Nami nakushauri uje ununue Kwangu,"Yeye alisema,"mafuta na dhahabu." Kwa nini alifanya hivyo?

Kwa nini akaruhusu kuiga huku kutokee katika siku za mwisho, wakati mambo haya yanakuja kutimia kwa Neno la kweli la Mungu; kisha akawaacha waigaji wainuke na kufanya jambo lile lile, na kulikana Neno la kweli la Mungu? Yeye alifanya hivyo kwa ajili ya Musa. Naye Farao akafanya jambo hilo dhidi ya Musa; na hao, Yane na Yambre, walifanya jambo hilo dhidi ya Musa. Na Biblia ilisema ya kwamba jambo litarudia tena katika siku za mwisho. Tuko hapa. Naam, kama hayo si Maandiko yakitimizwa, liko wapi?

108 Je! Musa aliwapigia makelele na kusema, "Hapa! Hapa! Hamuwezi kufanya jambo hilo. Mimi ndiye pekee niliyechaguliwa kufanya jambo hilo. Hapa! Ninyi acheni jambo hilo, sasa hivi"? Aliwaacha tu waendelee.

Acha waendelee. Kumbuka, Biblia ilisema, "Kama vile upumbavu wao ulivyodhihirishwa, ndivyo hawa nao katika siku ya mwisho watakavyodhihirishwa," wakati Bibi-arusi atakaponyakuliwa na kuchukuliwa mbinguni. Angalia.

109 Musa, Neno la kweli lililodhihirishwa, hakusema kitu, aliliacha tu. Lakini Yeye alifanya hivyo kusudi

apate kuufanya mgumu moyo wa Farao, kumdanganya Farao.

Yeye alifanya jambo lile lile kusudi apate kumdanganya Ahabu. Na maskini jamaa huyo mdogo amesimama pale peke yake, maskini Mikaya, akiwaambia, "BWANA ASEMA HIVI." Hapa amesimama mwingine, ametiwa mafuta, "BWANA ASEMA HIVI." Na ni kinyume, mmoja kwa mwingine.

110 Tunasimama leo tukiwa na BWANA ASEMA HIVI, ya kwamba ubatizo wa maji katika siku za mwisho unapaswa kuwa katika Jina la Yesu Kristo. Na mtu mwingine anasimama na kufanya miujiza, na, ni wa utatu.

Nionyeshe neno *utatu* katika Biblia. Nionyeshe ambapo kuna Miungu watatu. Nionyeshe ambapo kuna mambo kama hayo. Hayamo katika Neno la Mungu. Hakuna kitu kama mtu ye yote aliyewahi kubatizwa katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," kutumia vyeo hivyo. Mambo haya yote, "Loo, ni sawa, akina dada. Hiyo ni sawa, kuwa na ndefu tu … nywele zako fupi. Hilo ni sawa, si lazima mfanye jambo *hili*, *lile*, ama *lile jingine*. Loo, huo ni upuzi, mzee wa mtindo wa kale."

Lakini Biblia ilisema! Naye aliahidi, "Katika siku za mwisho, Yeye angemtuma Roho Wake wa Eliya, naye angewaita watu, watoto wa Mungu, wairudie ile Imani ya asili kama ilivyokuwa hapo mwanzo, ya lile Neno." Hilo Neno lilithibitishwa, Mwana wa Adamu katika siku za mwisho, kama vile ilivyokuwa huko Sodoma; jana, leo, na hata milele. Yeye aliahidi kufanya jambo hilo. Ni ahadi ya Mungu. Ni BWANA ASEMA HIVI.

111 Tazama walifanya jambo lile lile, kama tu vile Musa alivyofanya, hata Mungu akachoshwa nalo.

Sasa kumbuka, ni BWANA ASEMA HIVI, litatimia katika siku hii. Naam, chunguza dunia nzima; chukua kila dhehebu, chukua kila ukoo, mchukue kila mtu, chukua kila kanisa! Ninawaagiza, katika Jina la Kristo, kufanya jambo hili, ninyi wahubiri. Nawaagiza msome magazeti ama mwangalie kila mahali mnapotaka kwenda, muone kama haiko duniani sasa hivi. Mnaona?

Halafu, Mathayo 24:24 ni kweli kabisa. "Waliotiwa mafuta wa uongo watainuka katika siku za mwisho, nao watakuwa manabii wa uongo, nao watawapoteza wengi." Liangalie katika mifano sasa, inapokuja sasa, mnaona, "Watawapoteza wengi." "Manabii," wingi; "Makristo," waliotiwa mafuta, wingi; wengi mbalimbali, Wamethodisti, mnajua, na Wabatisti, na Wapentekoste, na kadhalika. Mnaona?

Lakini kuna Kristo mmoja halisi, Roho, na huyo ni Neno lililofanyika mwili kama alivyoahidi kulifanya.

Sasa tutaendelea mbele kidogo, kwenye Maandiko mengine zaidi.

Mpaka, Mungu akachoshwa nalo, ndipo lilikuwa limekwisha. Upumbavu wao ulidhihirishwa.

112 Angalia. Kumbuka, kapi linafanana kabisa na punje ya ngano. Mnaona? Sasa, usingeweza kusema, huko nyuma katika wakati wa Kilutheri, "shina lilikuwa ni ngano," hata hivyo lina Uhai ndani yake. Ubua ni sawa, Uhai uliokuwemo katika ubua ulikuwa sawa, lakini, kumbukeni, Uhai uliendelea kusonga mbele; ukatoka kutoka kwa Elisha ukaingia katika Eliya. Uzima unaendelea kusonga mbele. Lakini, kumbukeni, ni katika hatua nyingine. Hauwezi kubaki katika hatua hiyo. Hatuwezi kula mzoga uliooza wa wakati mwingine. Hatuwezi kula mzoga uliooza wa Kipentekoste, Mmethodisti, ama Mbatisti. Mnaona, umekuwa mzoga. Tuna Chakula kipya, Neno la wakati huu, na kadhalika.

113 Kumbuka, kapi linafanana kabisa na punje ya ngano. Huwezi … Haikufanana nayo katika jani, haikufanana nayo katika kishada, bali kweli ilifanana nayo katika kapi. Haikufanana nayo katika…Yesu Kristo yeye yule jana, katika Lutha; haikufanana nayo katika Wesley; bali hakika inafanana nayo katika Pentekoste, "ingaliwapoteza Walioteuliwa kama yamkini." Mnaona? Hizo hapo nyakati zenu.

114 Lakini kumbuka, kanisa hilo la Kipentekoste, katika siku za mwisho, lilikuwa ni Laodikia; naye Kristo akatolewa nje, kiini, Ngano, Yenyewe. Alipojaribu … Kumbukeni, wakati alipojaribu kujidhihirisha Mwenyewe kanisani, alitolewa nje. Lilikuwa bado ni kanisa, lililodaiwa kuwa; lililotiwa mafuta.

Lakini *hili* hapa Neno, Kristo Mwenyewe, hilo ni Neno lililotiwa mafuta ambalo litakuja kwa ajili ya Mwili Wake uliosalia, Bibi -arusi. Aliyetiwa mafuta, wa maji yale yale yaliyotia maji ile ngano, kama tulivyozungumzia, pia huyatia magugu maji, waliotiwa mafuta. Ni Wateule tu, ama waliochaguliwa tangu asili, wataweza kutambua tofauti kati yao. Sasa, Waefeso 5:1 inakwambia hivyo, na namna ilivyokuwa.

115 Wao ni watiwa mafuta. Kila mtu aseme, "Utukufu kwa Mungu! Tuna uhuru hapa chini. Haleluya! Sisi … Loo, haleluya! Tunanena kwa lugha, na kuruka. Tuna uhuru wa wanawake; ninyi watu mnajaribu kuwaweka chini ya mambo haya yote." Mnaona? Endelea. Hakuna kitu mnachoweza kufanya. Sema, "Vema, tunanena kwa lugha. Tunapaza sauti. Tunacheza katika Roho. Tunalihubiri Neno." Kabisa. Hakuna jambo la kusema dhidi yake. Vivyo hivyo na watu hawa hapa nyuma katika Biblia.

Yesu alisema, "Itawapoteza walio Wateule kama yamkini, Walioteuliwa."

116 Sasa angalia kapi. Kutoka kwenye Punje ya asili, Punje iliyoingia ardhini, haikuwa madhehebu. Ilikuwa ni punje moja, yenyewe. Lakini wakati ilipojitokeza, haikuwa Punje; ilikuwa madhehebu, mnaona, majani, mahindi.

Ndipo ikaingia katika hatua nyingine, ambayo ilikuwa kishada. Bado haikuwa kama mwanzo. Ilikuwa ni dhehebu.

Iliingia katika kapi, majani mengi, Pentekoste, karibu kufanana sasa. Iangalie. Iangalie. Inachukua umbo wakati wote, karibu kufanana kabisa, inafanana na Punje ya ngano kabisa unapoona maskini ganda hilo pale.

Lakini hatimaye inadhihirishwa, wala hakuna dhehebu. Hakuna wabebaji wengine. Dhehebu ni mbebaji tu. Hakuna wabebaji tena; ubua hauna budi kufa, kapi halina budi kufa, kila kitu kingine hakina budi kufa, bali ngano inaendelea kuishi. Huo ni mwili wa ufufuo, unaoshuka moja kwa moja na kuwachukua. "Wale walio wa mwisho watakuwa wa kwanza, na hao walio wa kwanza watakuwa wa mwisho." Mnaona, huwachukua moja kwa moja kwenye ufufuo. Je! Mnafuatilia jambo hili? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Vema. Angalia, punje ni …

117 Kapi linafanana kabisa na punje. Na mtu anayelima shamba la ngano, ama kitu kingine, angeangalia na kusema, "Mungu asifiwe, nina mmea wa ngano," wakati hana hata punje moja ya ngano. Linafanana kabisa na ngano, bali ni kapi.

118 Sasa, enyi marafiki, rudini nyuma pamoja nami. Ni mahali gani ambapo ufufuo wa kwanza ulipokuja, baada ya (kifo) siku zile ambazo ile punje ya ngano ilipopaswa kuanguka ardhini, ule Mwili, Bibi-arusi wa Kristo? Kristo alimpanga Bibi -arusi Wake, hilo ni kweli, Kanisa Lake? Yeye kamwe hakuliundia madhehebu; Yeye aliweka tu mitume, na manabii, na kadhalika, Kanisani, kuliweka safi. Lakini huko Nikea, Rumi, miaka mia tatu na sita baadaye, waliiundia madhehebu na kuunda madhehebu kutokana nayo. Hiyo ni kweli? Nalo likafa. Kila kitu kisichokubaliana na kanisa hilo kiliuawa. Nalo likatulia, kwa miaka mia kadha, mavumbini.

Lakini, baada ya kitambo kidogo, likatokea katika Luther. Majani madogo ya kwanza ya mahindi yalichipuka. Ya pili, yalichipuka kutoka hapo. Waliendelea, walikuwa na Zwingli na kadhalika, na madhehebu mengine na kadhalika. Ndipo, baada ya kitambo kidogo, akaja Mwanglikana.

Halafu basi ni jambo gani lililotukia? Huyu hapa Wesley anakuja pamoja na uamsho mpya, kishada, ambacho kinafanana zaidi na Ngano. Basi ni kitu gani kilichotukia kwenye jambo hilo? Kiliunda madhehebu, na kikakauka na kikafa.

Uhai huo uliingia moja kwa moja kwenye kapi, nalo kapi likaja karibu kabisa kama Ngano. Lakini, hatimaye, upumbavu wake ulidhihirishwa katika miaka minane au kumi iliyopita, hasa katika miaka mitatu iliyopita. Sasa linafanya nini? Linajiondoa kwenye Ngano.

119 Sasa mbona hapajakuwepo na madhehebu yaliyozuka katika miaka hii ishirini iliyopita ya ufufuo huu mkuu; ni manabii waliotiwa mafuta, waalimu waliotiwa mafuta, na kadhalika, lakini kwa nini hakuna? Hakuna kitu baada ya Punje. Mnaona, Hiyo imerudi, bila madhehebu. Loo, jamani, kipofu angeweza kuona jambo hilo. Haliwezi kuunda madhehebu; linayapinga kwa dhati. Ni punje ya Ngano, Yenyewe. Mwana wa Adamu atadhihirishwa. Ile punje ya Ngano itajirudia Yenyewe tena, Mwana wa Adamu katika siku za mwisho.

"Na kutakuja kuigiza Kwake kwa uongo, katika siku za mwisho, ambako karibu kutawadanganya Wateule kama yamkini." Angalia makapi yao ya kimadhehebu yakiondoka sasa.

120 Linaifanya Ngano tu ijulikane, kwa Wateule, ambao ni sehemu Yake. Angalia jinsi hili linavyoelezwa hapa vizuri sasa. Ni ninii tu … Angalia, waliotiwa mafuta wataweza; Wateule wa kweli na waliochaguliwa tangu zamani, Waefeso 5:1, ama 1:5, hasa, watachaguliwa, watateuliwa. Hao ndio pekee ambao hautawadanganya.

Angalia, manabii waliotiwa mafuta watakuwa wa uongo, na miongoni mwao kutakuwa na watiwa mafuta wa kweli. Utawajuaje? Kwa Neno. Kama, tunalo katika kivuli. Mnaona jambo hilo? Sema, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Mnaona?

121 Angalia, wale waliotiwa mafuta, ni Neno pekee litakalowatenganisha, si ishara. Loo, la. Watafanya ishara zile zile, bali Neno ndilo lililowatenganisha. Hakika. Wote walitabiri. Wote walifanya *hivi*, *vile*, na *vinginevyo*, hakika, vivyo hivyo tu. Yesu alisema wangefanya jambo lile lile. Lakini Neno ndilo lililowatenganisha, angalia, si ishara.

Mliona? Yesu alisema hapa, katika Mathayo 24. Yeye hakusema, "Watatokea Yesu wa uongo katika siku za mwisho." Loo, la, wao hawangalistahimili jambo hilo. La. Umpate Mpentekoste ambaye ni Mpentekoste halisi, aseme, yeye mwenyewe, yeye ni "Yesu"? Mnaona? Unampata Mmethodisti wa

uongo, ama Mbatisti, ama mtu kama huyo, ama moja ya madhehebu, aseme, "Sisi ni Yesu"? Wanajua vizuri zaidi ya hayo. Hawatafanya hivyo. Lakini Biblia ilisema wangekuwa "Makristo wa uongo," si Yesu, bali, "Makristo wa uongo." Wasingeweza kutambua, waseme, "Mimi ni Yesu." Loo, la.

122 Lakini wao ni "Makristo wa uongo," wala hawajui, kwa sababu wao ni kinyume cha Neno. Naye Mungu huthibitisha jambo lile lile. Sasa, ninaleta tu hili moja kwa moja kwenye mashindano ya kuamua sasa, maana mmeona jambo lile lile likifanywa na watu hawa ambalo limefanywa na walio halisi. Naye Yesu alisema hivyo.

Sasa, kama nilivyosema, sasa kwenu watu mlio huko nje kwenye, mahali palipo na simu kule, mimi—mimi siwahukumu, bali hili ni kanisa langu na—na kundi langu ambalo Roho Mtakatifu ameniweka kuliangalia, nami sina budi kuwaambia Kweli. Wakati unachelewa.

123 Sasa, wasingeweza kustahimili hilo, bali, "Makristo wa uongo," wa uongo, waliotiwa mafuta, karibu kila ishara na kila herufi ya Neno. "Wanaamini ubatizo wa Roho Mtakatifu?" Kabisa. "Wanaamini yote haya?" Naam. "Wanaamini kunena kwa lugha?" Naam. "Wanaamini ishara na maajabu yanafuata, ishara zitafuatana nao?" Naam. Hao si Wamethodisti, hao si Wabaptisti. La, la. Hao ni Wapentekoste. Mnaona, hii ni siku ya mwisho.

Sasa, wakati wa kwanza wa kanisa kamwe haungeona jambo hilo. Wakati wa kanisa la Kimethodisti kamwe hawakuona jambo hilo; Wakati wa kanisa la Kibaptisti, hawakuona jambo hilo kamwe; Wakati wa kanisa la Kipresbiteri, hawakuona jambo hilo kamwe. Lakini, Wapentekoste, wanafanana sana na kilicho Halisi! Hapo ndipo ambapo, Ngano, kapi linafanana sana na Ngano. Wasingeliona kamwe. Mnaona? Wasingeweza. Lakini ni siku za mwisho, siku hii. Naam, bwana.

124 Angalia, kama tu ilivyokuwa hapo mwanzo, ndivyo itakavyokuwa mwishoni. Kama Hawa alivyolifasiri tu Neno moja vibaya, Shetani alifanya hivyo kwa Hawa, naye akaliamini. Yeye, si mwanamume; kanisa, si Yeye. Mnaona? Kanisa ndilo lililolichukua neno la uongo. Mnaona? Si Adamu; Hawa. Si Kristo; kanisa, bibi-arusi, waliotiwa mafuta, wanaodhaniwa wametiwa, wanaojiita Bibi-arusi, mnaona, yeye alipochukua neno la uongo.

Hivi hamwezi kuona jambo hilo? Naam, linafungamana pamoja kama kamba ya viatu, kama kope kwenye jicho lako. Mbona, kila utakachogeukia, Biblia, inalifungasha tu moja kwa moja pamoja. Hawa, si Adamu; Hawa aliamini jambo hilo, si Adamu. Bibi-arusi leo, anavyojiita, aliliamini; si Kristo. Bibi-arusi ana za kila namna, anayejiita bibi-arusi; ishara zile zile, maajabu yale yale, kila kitu kile kile; bali si Yule aliye halisi. "Kuwapoteza Walio Wateule kama yamkini."

Sasa upesi, kama tunaweza kumaliza jambo hili katika dakika kumi na tano, tutakuwa kwenye wakati. Angalia kwa makini sana sasa, ili usi—hutafahamu vibaya, wewe.

125 Sasa, la, wasingevumilia kuitwa "Yesu wa uongo." Wasingefanya jambo hilo, kuvumilia kuitwa, "Yesu." Bila shaka sivyo. Hilo ni dhahiri sana. Mtu ye yote angejua jambo hilo. Mtu yeyote angejua hawakuwa Yesu. Sijali kama walikuwa na mafuta mgongoni mwao, na damu mikononi mwao na juu na chini machoni mwao, wangali wanajua ni … Mtu ye yote aliye na akili timamu, alijua haikuwa Yesu. Mnaona? Wasingevumilia jambo hilo. Lakini wao wanajiita "waliotiwa mafuta." Nao wanafanya ishara na maajabu, "karibu kuwapoteza walio Wateule." "Bali Makristo wa uongo, waliotiwa mafuta, watatokea, nao watawapoteza walio Wateule kama yamkini."

126 Sasa angalia kwa makini. Usikose tamshi hili, kwa sababu linastahili kusikiliza.

Yeye anaweka tu utepe mdogo kwenye maikrofoni hii hapa, kuifanya isiruke. Nimekuwa nikitokwa na jasho; ilidondokea kwenye utepe, mnaona.

Na kwa hiyo litakuwa kama Hilo tu, Biblia, ilisema itakuwa hivyo. Mnaona?

127 Angalia, si Mayesu wa uongo. "Makristo wa uongo!" Wanaamini wametiwa mafuta, bali wanajua wao si Yesu. Mnaona, hilo ni dhahiri sana. Kama mtu angepanda juu na kusema, leo, "Angalia makovu yaliyo mkononi mwangu. Angalia kwenye uso wangu. Mimi ni Yesu." Vema, sasa, tunajua ya kwamba hilo ni kosa. Na, kumbukeni, Yesu hakusema ya kwamba hao jamaa wangetokea. Yeye alisema kungetokea "Makristo wa uongo." "Makristo," wingi, madhehebu, na kadhalika, *watiwa mafuta;* waliotiwa mafuta na roho ya kimadhehebu, wala si Neno. Mnalifuata? Si Yesu wa uongo. "Makristo wa uongo," watiwa mafuta, wa uongo. Mnaona? Loo, ni dhahiri iliyoje! Namna sisi … Hakika humtakosa hili!

128 Sasa, kumbukeni, daima nimewaambia kuna tabaka tatu za watu. Kuna jamii tatu za watu; Ham, Shemu, na Yafethi, jamii tatu. Matabaka matatu, nami nilisema, huyo ni mwamini, anayejifanya mwamini, na asiyeamini. Imekuwa hivyo daima, daima itakuwa hivyo. Mnaona? Kulikuwako na Musa, mwamini; kulikuwako na Yane na Yambre; wasioamini. Mnaona? Kulikuwako na Balaamu; Musa … Daima makundi hayo matatu ya watu, tabaka tatu; mwamini, anayejifanya mwamini, na asiyeamini.

Sasa kumbuka, asiyeamini, kanisa la kimadhehebu, haliamini katika ishara zo zote kamwe; baridi, rasmi, gumu, kanisa ulimwenguni, hayo madhehebu. Bali anayejifanya mwamini ni kapi hilo. Huyo ndiye jamaa anayejifanya kuamini. Na halafu kuna mwamini halisi ambaye ni wa kweli kwelikweli. Sasa, waangalie wanaposonga mbele sasa, kwa dakika moja tu.

129 Na angalia namna hawa wasioamini wana ujasiri, ama hawa wanaojifanya waamini na wasioamini. Jamani! Wao wana ujasiri, angalia, hata kama Shetani alisimama moja kwa moja katika Uwepo wa Neno la kweli, na kusema, "Imeandikwa!" Hiyo ni kweli?

Kwa nini Shetani alifanya hivyo? Ni kwa sababu hakujua Neno kwa ajili ya hilo … Yeye alijua hilo Neno lilikuwa la saa hiyo, bali alishuku maskini Mtu huyu mnyenyekevu kuwa ndiye Neno hilo. "Kama Wewe ni Mwana wa Mungu. Ninajua Mwana wa Mungu anakuja, kwa sababu Hilo lilisema angefanya hivyo. Na imeandikwa, 'Yeye atakuagizia Malaika Wake wakulinde.' Mnaona? Nithibitishie jambo hilo! Fanya muujiza! Hebu nikuone ukifanya hivyo." Mnaona? Mnaona?

Mnaona, asiyeamini, anayejifanya mwamini, mwigaji. Mwangalie Yuda moja kwa moja miongoni mwao, wakati ule ule, anayejifanya mwamini! Mnaona? Angalia, na kulikuwako na Neno la kweli.

130 Namna walivyo jasiri! "Sasa, msiujali upuzi huo. Hakuna kitu Kwake. Usiende huko juu. Ni kundi la makelele tu. Hakuna chochote kwa Hilo. Hayo yote ni hadithi tu za uongo. Hayo yamo niani mwako." Mnaona, mnaona ninalomaanisha? Simama moja kwa moja katika Uwepo wa Neno na uliseme.

Shetani aliingia moja kwa moja. Kama vile Biblia ilivyosema hapa katika Yuda, "Hata yule Malaika Mkuu, aliposhindana na Shetani, alisema, 'Bwana na akukemee.'" Dhidi ya Neno Lenyewe!

Na huyu hapa mpinga Kristo, mtiwa mafuta, amesimama papa hapa dhidi ya Neno halisi la siku hiyo, Yesu Kristo, kisha kasema, "Imeandikwa."

131 Angalia siku za mwisho. "Itafanana sana ingewapoteza Walio Wateule kama yamkini." Loo, jamani! Sababu ya Wateule kutodanganywa, mnajua ni kwa nini? Ni kwa sababu wao ni Neno. Mnaona? Ni kama tu Uhai ulio kwenye shina, nilisema muda mfupi uliopita, hauwezi kujikana. Mnaona, ni Neno na katika majira ya Neno. Hiyo ni kweli.

Kama tu vile Yeremia, yeye alijua. Haidhuru Hanania alisema nini, alijua mahali alipokuwa. Hivyo ndivyo hasa Musa alivyofanya, na—na hao wengine. Hiyo ni, yeye alijua, haidhuru manabii wa uongo walisema nini, Neno la Mungu lilikuwepo hapo. Ilikuwa imeandikwa.

Hiyo ndiyo sababu Mikaya angeweza kusema, "Vema, ngoja tu uone."

Ahabu alisema, "Ninaamini manabii wangu. Dhehebu langu ni sahihi. Nitakaporudi kwa amani … Mwekeni huyu jamaa huko gerezani. Nitamshughulikia! Mpe mkate wa huzuni. Mfukuzeni, msishiriki naye kamwe. Nitakaporudi kwa amani, tutamshughulikia jamaa huyo."

Mikaya akasema, "Kama ukirudi kamwe, Bwana hajanena nami." Yeye alijua alikuwa na BWANA ASEMA HIVI, na ono lake lilikuwa kulingana na BWANA ASEMA HIVI; si kwa majira mengine, bali kwa majira hayo. Amina! Haleluya! Majira hayo!

Wajasiri, kasimama na kushindana na Malaika Mkuu! Imesemwa, ya kwamba, "Wapumbavu hukanyaga kwa viatu vyenye misumari mahali ambapo Malaika wanaogopa kutembea." Hiyo ni kweli.

132 Sababu ya Walioteuliwa, Yesu alisema, hawatadanganywa, ni kwa sababu wao ndio Neno hilo. Hawawezi kuwa kitu kingine. Hawawezi kusikia kitu kingine. Hawajui kitu kingine. Hiyo ni kweli.

Kumbukeni, Musa hakuchukuliwa na maigizo yao yote. Sivyo! Musa alisema, "Sasa, ngoja kidogo, Farao. Wajua nini? Bwana aliniambia nifanye jambo hili, lakini, Mungu atukuzwe, ninaona ya kwamba wavulana wenu wanaweza kufanya jambo lile lile. Kwa hiyo, hebu nikwambie nitakalofanya, nitaungana nawe"? A -ha! Hiyo haisikiki kama nabii wa Mungu. La, hasha! Yeye alisimama imara tu kama ambavyo angeweza kusimama. Yeye alijua, barabara, Mungu angeshughulikia jambo hilo kwa namna fulani, maana Yeye aliahidi. "Nitakuwa pamoja nawe. Sitakuacha."

133 Alijua, kwa hiyo hakujiunga nao. Loo, la. Alikaa moja kwa moja pamoja nao. Hakutaka mojawapo ya madhehebu yao. Alikaa sawa na Mungu. Yeye hakuchukuliwa na mambo yote wangaliweza kufanya. Walipofanya jambo moja … Alileta chawa; wakaleta chawa. Alileta damu; walileta damu. Alileta kila kitu; walimwiga kwa kila hali, moja kwa moja. Alisimama tu kimya. Alijua barabara ni kitu gani. Mungu alikuwa kazini.

Mnaelewa sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Mnachukua mbili na mbili, na kufanya nne? ["Amina."] Hutaki kuunguza sana. Kwa hiyo, kwa hiyo mna—mnafahamu, mnaona.

Kwa nini? Wao hawatadanganywa nayo. Mwamini halisi, wao ni Mbegu iliyochaguliwa tangu zamani

ambayo inapaswa kusimama katika siku hiyo.

134 Ni kwamba tu, pia, Yesu alisema hivi, "Wengi watakuja katika siku hiyo, katika Jina Langu, na kusema, 'Bwana, sikutoa pepo katika Jina Lako?'" Yesu alisema, "Katika siku za mwisho, hapo wakati utakapokwisha na ule ufufuo mkuu uje, ya kwamba wengi watakuja na kuketi katika ule Ufalme." Ufalme wa Mungu umo ndani yenu.

Wengi, magugu watakuja na kuketi moja kwa moja pamoja na Ngano, yaseme, "Sasa, ngoja kidogo, Bwana! Nilinena kwa lugha. Nilipiga kelele. Nilicheza katika Roho. Ninawatoa pepo. Nilinena kwa lugha. Nimefanya mambo haya yote."

Yeye angesema nini? Angalia. "Ninyi mtendao maovu, hata sikuwajua."

135 Uovu ni nini? Mwuulize mtu fulani. Ni "kitu ambacho unajua unapaswa kufanya, nawe hutakifanya." Wanajua hilo Neno. Wanalisikia. Mnasikiliza kanda hii. Mnasikiliza Ujumbe huu. Unamwona Bwana Mungu akisema jambo hilo; unamwona akilithibitisha, kulifanya kweli. Nawe unajua Hili dhahiri tu kama vile jua linavyowaka huko nje, bali wewe utakayeshikilia madhehebu yako, kushikilia hayo mambo ya uongo; ewe utendaye maovu!

"Loo, naam, nilikuwa na mikutano mikubwa. Nilifanya jambo hili. Nilifanya hivyo."

Kasema, "Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu, Mimi sikuwajua kamwe."

"Vema, Roho Mtakatifu alishuka juu yangu." Sitilii shaka hata kidogo. "Nilinena kwa lugha. Niliimba katika Roho. Nimekwisha …" Sitilii shaka hata kidogo. Hakuna swali kwa hilo. Loo, ndugu, dada, ni hali ya namna gani!

Huu ni wakati wa kutetemeka. Tuko wapi? Neno hili linafufuka sasa. Angalia.

136 Naam, Yeye alisema wangefanya hivyo. Angalia, "Enyi watendao maovu." Nina Andiko lililoandikwa hapa. Sijui ilikuwa wapi hasa. Nimechukua wakati mwingi sana. Nitaliangalia, kwa dakika moja tu, na kuona ilikuwa ni nini. Nina—nina Mathayo 7:21. Si—sijui ni wapi. Mimi, wakati mwingine siandiki kitu chini kwake, vema, mi—mimi hukihubiri namna hii, ni—ninasahau nilichokuwa nikirejea kwenye Maandiko. Mathayo 7:21.

> *Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni.*
>
> Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii ...

Manabii, waliotiwa mafuta! Hiyo ni kweli? Sisi hatukuwa nabii? Si tulikuwa tumetiwa mafuta, tumetiwa mafuta? Si nilitabiri katika Jina Lako? Na katika Jina Lako sijatoa pepo?" Unawezaje kufanya hivyo, na kukataa kubatizwa katika Jina la Yesu? Mnaona? Loo, jamani! Mnaona ni danganyifu iliyoje? Karibu kabisa kufikia mahali hapo, halafu wanarudi nyuma. Wao wanaenda moja kwa moja mpaka kwenye Neno, kisha wanarudi nyuma. Sasa angalia jambo hili. Tunatoa hili nje, kwa dakika moja.

> *Wengi wataniambia … Bwana, Bwana, hatukutabiri, tumekuwa manabii*

… Naam, nilinena hayo katika Mathayo 24:24

> *… Na kwa jina lako … kutoa pepo? na kwa jina lako kufanya miujiza mingi* … kazi nyingi?
>
> *Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.*

"Wakati Hilo lilipowekwa moja kwa moja mbele zenu nanyi mkaliona jambo Hilo, na kuliona likitenda kazi, mkaona lilikuwa ni Neno; na kwa ajili ya madhehebu yenu, mkashikiliwa kwayo. Hata sikuwajua. Sijali mliwatoa pepo wangapi, ni wangapi mlifanya *hivi* na *vile;* sikujua kitu kuwahusu ninyi."

Balaamu alisema, "Nilitabiri vizuri, katika Jina Lako. Ilitimia."

"Hiyo ni kweli kabisa, lakini, ilipofikia kwenye Neno, ulilikataa."

Loo, ndugu, mnaona ile sehemu ya iliyodanganyifu? Si "nabii," hasa; bali ni kwa Neno, Neno la kweli, Neno lililothibitishwa likidhihirishwa. "Enyi mtendao maovu!"

137 Kujaribu, Shetani amejaribu katika nyakati zote kuliiga Neno la kweli. Tunajua jambo hilo, sivyo?

138 Angalia, wanakuja mpaka mpakani kisha wanaacha. Angalia hapa, Yeye alisema, katika Waebrania sura ya 6, sasa, tulikuwa tukisoma muda mfupi uliopita. Niliwaambia mrejee kwenye jambo hilo, nasi tutafanya hivyo kwa dakika chache zifuatazo. Akasema:

*… Bali miiba na michongoma … iliyo karibu na kukataliwa; ambaye mwisho wake ni kuteketezwa*. (Mpaka!)

*… Ninyi mlioionja … karama ya mbinguni, …*

"Kuonja," kwa maneno mengine, mmeiona! Huwezi [Ndugu Branham anapigapiga midomo yake — Mh.] onja tu kwa kinywa chako. Bali uliliona, nawe ulijua lilikuwa Kweli. Mlijua lilikuwa Kweli. "Mmekwisha onja kipawa cha Mbinguni."'

*… Na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu,* aliposhuka juu yako,

*… Kulionja neno zuri la Mungu,, …*

"Kuonja," umeona ilikuwa ni kweli. *"Na Roho Mtakatifu akiwashukia," magugu shambani.*

…kisha wakaanguka,…

"Kumkana Kristo yeye yule aliyekutakasa, na kukuita, na kuweka upako huo juu yako."

… haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu,kwa jambo hilo

Haisameheki! "Hawawezi kabisa kuufikia ujuzi wa ile Kweli."

Kwa maana haiwezekani kwa hao walikiokwisha… kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu,

Walianguka kwenye magugu, mnaona, "Walianza na Yesu, kisha, 'Bwana, ninapita,'" bali ulipolifikia Neno, unarudi. "Kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, na hata wakaonja, ama wakaona Neno Lenyewe likidhihirishwa." Kisha wanaliacha, "Haiwezekani kabisa kwao kuliona kamwe wala kulifikia."

Hilo ni BWANA ASEMA HIVI. Sasa, ninyi … "Mbingu na nchi zitapita, bali Hilo halitapita." Mnaona jambo hilo? "Haiwezekani kabisa." Biblia ilisema hivyo, na Roho anashuhudia jambo hilo.

139 Angalia, hebu niwape mfano mdogo. Angalia watu hao waliokuja chini ya unabii wa Musa, waliotoka katika madhehebu hayo, na wakatoka kutoka katika kila kitu, chini ya unabii, wakaona kazi kuu na maajabu, na mambo kama hayo, na wakafikia kwenye mpaka wa kuingilia.

Sasa, Lee, hilo hapo linakuja "jina lako kwenye kile Kitabu." Mnaona? Umekitengeneza. Nanyi ambao hamko hapa, na huko nje kwenye—kwenye mawasiliano ya simu, ni Daktari Lee Vayle aliyeketi hapa. Yeye anakitia sarufi kitabu hiki cha Nyakati Saba za Kanisa. Basi tatizo likatokea, ama swali, juu ya "jina kutolewa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo." Mnaona, limewatatiza wahudumu wengi sana. Bali subirini hata mtakapokipata hicho kitabu, mtalielewa jambo hili iwapo mna Nuru yo yote ndani yenu. Mnaona?

Angalia, sasa, utageuza kichwa chako na hata hutaliangalia Hilo endapo hutaki kuliona. Kama vile mama yangu alivyokuwa akisema, "Huwezi kupata damu kutoka kwenye mboga nyekundu, maana hakuna damu ndani yake."

140 Angalia, Nuru haina budi kuja; haiko gizani. Nuru huja gizani, na giza haliioni. Waangalie sasa waliotiwa mafuta katika siku hii.

Kama vile Musa alivyowatoa hao wana wa Israeli; nao wakasikiliza na kuchanganyikiwa kabisa na taifa hilo kuu kule juu. Sasa, Israeli walikuwa wa kidini. Hawakuwa na nchi, hawakuwa na makao. Walikuwa wanaelekea nyumbani.

Hatuna kanisa. Sisi si ninii … Tuna—tunaelekea kwenye Kanisa fulani, lile Kanisa la Mzaliwa wa Kwanza, Kanisa lililo Utukufuni; si kanisa lililo duniani, la mwanadamu. Kanisa lililo Utukufuni, wale walioitwa watoke, waliochaguliwa tangu zamani kwa ajili ya Uzima wa Milele, mnaona, wakienda Nyumbani mwao.

Na walipofikia mahali pa kuvuka, walilitilia shaka Neno, kisha wakarudi. Baada ya Yoshua na Kalebu na hao wengine kuvuka na kuleta kichala cha zabibu, kuwathibitishia ya kwamba ile nchi ilikuweko, Neno la ahadi ya Mungu, "Ni nchi nzuri, maziwa na asali." Nao wakayaleta, upande huu, kuwathibitishia. Nao wakaonja hayo, na kusema, "Loo, loo, hatuwezi kufanya jambo hilo, hata hivyo." Ni kitu gani kilichotukia? Waliangamia jangwani. Walikaa pale pale na kujiundia madhehebu, na wakafa, kila mmoja wao.

Bali hao waliovuka na kuleta, Yoshua na Kalebu; Musa aligeuzwa. Mfano wao kulingojea Kanisa; na ufufuo wa Agano la Kale, Agano Jipya; na Mwili ulionyakuliwa. Mnawaona hao watatu pale? Hamna budi kuwaweka hao watatu mstarini, mnaona, kwa hiyo, katika mwamini na asiyeamini. Mnaona?

141 Angalia namna ilivyokuwa "kabisa." Kumbuka, Mungu kamwe hakusamehe dhambi hiyo. Sasa wataingiaje? Kama ni miiba, kwanza, ni miiba mwishoni. Ni wale tu waliochaguliwa tangu asili ndio watakaoliona Hilo.

142 Angalia kwa makini sasa. Kama tu katika siku za Mtakatifu Martin, moja kwa moja kabla ya zile Nyakati za Giza; mtu mdogo mcha Mungu. Ni wangapi waliopata kusoma maandiko ya Mtakatifu Martin? Wengi wenu mmesikia. Tulishuka tukaenda kuchukua maandishi ya Mtakatifu Martin; yule kasisi alisema, "Lakini yeye hakuwa ameingizwa katika hesabu ya watakatifu." Hakika, hakuwa; si na hao, bali alikuwa ameingizwa na Mungu. Roho Mtakatifu alituambia tumweke pale kwenye ule wakati wa tatu wa kanisa. Mnaona?

143 Angalia namna alivyokuwa mtu mcha Mungu; kuitwa, kuchaguliwa tangu zamani. Wazazi wake, makafiri. Baba yake, askari. Hakika, hakuwa; si na hao, bali alikuwa ameingizwa na Mungu. Na, wakati alipofanya hivyo, na daima aliamini ya kwamba kulikuwa na Mungu mahali fulani; mtu wa mwituni, na angeweza kumwona Mungu. Siku moja alipitia karibu na mji fulani, na kulikuwa na mzee mwombaji amekaa pale, anakufa, akimwomba mtu fulani… Yeye alikuwa baridi usiku huo. "Loo," kasema, "nipe kitu cha kunifunika; Nitakufa usiku wa leo."

144 Hakuna mtu angefanya hivyo. Naye Martin akakaa kando na kumwangalia kwa muda kidogo. Hakuna mtu angefanya hivyo. Alikuwa na koti moja tu. Angeganda kwa baridi, yeye mwenyewe, alikuwa kazini, kama—kama alimpa koti hilo. Kwa hiyo akawaza, "Sote wawili tuna nafasi ya kuishi kama tukigawana." Kwa hiyo akachukua koti lake mwenyewe, na kuligawanya vipande viwili kwa upanga wake, na kumfunika kile kigae cha kale. Akamfunika koti lake mwenyewe.

Kila mtu alisema, "Angalia ni mlinzi wa kuchekesha iliyojei. Angalieni askari wa kuchekesha iliyoje, amejifunga nusu koti!"

145 Usiku wa pili, wakati alipokuwa ametoka kazini na amelala kitandani mwake, aliamshwa usingizini. Akaangalia, amesimama chumbani, na alisimama pale Yesu Kristo amejifunika kipande hicho kikuukuu cha nguo ambacho alimfunika nacho. Yeye alijua papo hapo, "Mnayomtendea mmoja wa walio Wangu wadogo hayo mmenitendea Mimi, kwa watiwa mafuta Wangu," wanaoketi pale.

Alikuwa ni mtumishi mkuu wa Mungu. Kanisa lilimdhihaki, likamtesa, likamfukuza, na cho chote kile, bali yeye alikuwa ni nabii wa Mungu. Yale aliyosema yalitimia. Kuna wengi waliomwamini katika wakati huo, pia.

146 Ninataka kuwaonyesha namna Shetani alivyo mdanganyifu. Siku moja alikuwa ameketi kwenye chumba chake cha kusomea. Akaja malaika mwenye nguvu, ana taji kichwani mwake, amevaa viatu vya dhahabu, kimia imeizunguka nguo yake ya dhahabu, kisha akasema, "Martin, unanijua mimi?" Yeye alisema, "Mimi ni Bwana na Mwokozi wako. Mimi Ndiye niliyekuokoa. Niabudu, Martin." Bali nabii huyo, akijua kulikuwa na kitu fulani kidogo kigeni hapo, akakaza kumwangalia. Yeye alisema, "Martin, mimi ni Mwokozi wako, Yesu Kristo. Niabudu! Hivi hunijui, Martin?"

Martin akaendelea kumwangalia, Maandiko yakipita haraka moyoni mwake. Akasema, "Shetani, ondoka kwangu." Yeye alisema, "Una taji kichwani mwako. Na Neno la Mungu linasema 'watakatifu Wake watamvika taji' mwishoni mwa wakati."

Je! Hilo lisingekuwa ni chambo cha Kipentekoste? Angalia Neno hilo, ndugu. Hapo ndipo linalipolipa.

147 Siku moja, tena, katika nyumba ya watawa, walikuwa na mtakatifu mzee kule, kundi la watawa vijana. Kuna mmoja wao aliyekuwa kwa namna anakera. Angalia jambo hili, huu hapa mfano m—mzuri leo. Alitaka kuwa kitu fulani juu ya hao wengine. Alitaka kujionyesha, mamlaka, kitu fulani kikubwa, kitu fulani bora zaidi, tabaka yote, mwajua, na kitu fulani kikubwa mno. Ilimbidi awe bora sana. Daima nilitaka ndugu wengine wasi … Mwajua, ilibidi awe tofauti. Mnaona? Yeye, haidhuru ilikuwa ni nini, alikuwa na kiburi sana. Yeye alikuwa ndiye kokoto pekee ufukoni. Hakuna mtu angaliweza kumgusa. Sasa angalia kilichotukia. Ilimbidi awe na kitu kikubwa. Ilimbidi kujilinganisha na watu wa ta—tabaka ya juu. Mnanifuata? Mnaona? Kwa hiyo, yeye alisema, alitabiri. Yeye alisema, "Bwana amenifanya nabii, pia. Mimi ni nabii."

Sasa, kulikuwa na nabii mmoja aliyedhibitishwa nchini, na huyo alikuwa ni Mtakatifu Martin; alizaliwa nabii.

148 Lakini mtoto huyu alisema, kijana huyo alisema, kijana mtawa mwenye umri wa miaka ishirini na mitano. Yeye alisema, "Bwana amenifanya nabii, nami nitawathibitishia." Kasema, "Usiku wa leo Bwana atanipa joho kubwa na zuri, anivalishe, joho jeupe, kisha nikae kati yenu. Ndipo ninyi nyote mtanijia, mnaona, nanyi mtashika amri zangu."

Sasa linganisha jambo hilo leo, mnaona, "Nitakuwa kiongozi wa madhehebu. Nitawashughulikia, enyi watawa wengine."

Basi kweli kabisa, "Usiku huo, nuru ziliingia kwenye jengo," ndivyo maandishi ya Mtakatifu Martin yanavyosema. Yasomeni. Na ni ya kweli. Ni historia. Ndipo nuru zikaingia, na hao wengine wote wakaangalia, na huyu hapa anakuja… Alikuwa amevaa joho jeupe, akisimama miongoni mwao. Akasema,

"Mnaona yale niliyowaambia?" Lakini hilo ni kinyume cha Neno.

149 Na wakati alipoenda akampata mzee mkuu wa chuo hicho, alitembea huku na huko kidogo, kasema, "Mwanangu, hilo halionekani kuwa sawa." Akasema, "Kuna njia moja tu." Hili hapa! "Kuna njia moja tu kwetu kujua. Ilionekana ya kimbinguni." Jamani, Pentekoste ingalinyakua hilo, shina, chubwi, ugwe, ndoana, na kadhalika! Yeye alisema, "Muujiza huenda ukaonekana ni sawa, bali hauonekani sawa kwa Neno. Sasa, tuna mtu kama huyo, nabii aliyetiwa mafuta, jina lake Martin. Njoo, panda uende mbele zake."

Jamaa huyo akasema, "La, la! Martin hana uhusiano wowote na jambo hili."

Kisha akasema, "Utaenda, hata hivyo." Nao wakamshika mkono, kumpeleka mbele ya Martin, na lile joho likamwacha.

150 Mnaona, "Itawadanganya walio Wateule kama yamkini." Mnaona, wanawajua. Yesu alisema, "Kondoo Wangu wanalijua Neno Langu."

"Loo," unasema, "'sikia "Sauti" Yangu."

Hilo ni Neno Lake. "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno." Mnaona? Waliochaguliwa tangu zamani wanajua jambo hili. "Neno geni, ama sauti ya kigeni, hawatafuata."

Hivyo ndivyo ilivyo na jamaa hao kule nyuma; wasingefuata. Walijua ya kwamba Martin alikuwa pale, nabii wa wakati huo, aliyetambulishwa na Mungu kupitia Neno, alijua Neno. Na mtu huyo asingesimama mbele Yake.

151 Yeye pia alisema, "Palipo na Mzoga," ama Neno, "hapo, katika majira yake, tai watakusanyika." Sasa hiyo ni Math- … Mnataka kuandika hilo, hiyo ni Mathayo 24:28. Kabla kidogo tu, Mathayo 24:24; aya nne chini yake, mnaona, kama unataka kuipata. "Palipo na Mzoga," palipo na Mana, palipo na Neno, "ndipo watakapokusanika tai."

152 Sasa sina budi kuharakisha. Niliangalia kule juu na kuona ni wakati gani … Ni—ni dakika saba ama dakika nane baada ya saa sita. Nitaharakisha upesi sana, ama tunaweza kuumaliza usiku wa leo, ama lo lote mnalotaka kufanya. Asubuhi hii au usiku wa leo? A -ha? Ni wangapi wanaopaswa kwenda nyumbani leo baada ya ibada, hebu tuone mkono wako, mnaona. Loo, jamani, afadhali endelea!

Ninasikitika kuwashikilia watu hao kwenye hizo simu huko nje namna hiyo, bali nitaharakisha. Huu una faida kuu kuliko pesa zenu. Ninaamini unafaida, kwangu mimi, mnaona. Pesa zenu zitakwisha. Huu hautakwisha; Ni Neno. Mnaona?

153 "Palipo na Mzoga, ndipo watakapokusanyika tai." Palipo na Mzoga, mahali pana—pana—panapochinjiwa, hapo ndipo tai watakusanyika. Palipo na Nyama mbichi, Neno la wakati huu, ndipo watapokusanyika tai.

Lakini baada ya kuoza, basi ndege wala mzoga watajazana kwake. Naam. Mnaona ninalomaanisha? Wakati mnyama amechinjwa, hawa hapa tai wanakuja; bali baada ya kukaa pale, akaoza, basi hawa hapa ndege wala mzoga wanakuja. Tai hawatakuwa na uhusiano wo wote nao. Mnaona?

Yesu alisema, "Palipo na Mzoga," pale ilipoanguka Mana, usiku ule Mana itakaposhuka mpya, "hapo ndipo tai watakusanyika kwa ajili Yake." Hiyo ndiyo Mana ya siku hiyo. Mnaona? Angalia.

154 Lakini baada ya kuoza, mabuu huingia ndani yake, ndipo hawa ndege wala mzoga wanakuja. Wao hawawezi kuisikia harufu mpaka imeoza. Si ajabu Yesu alisimama pale na kusema, "Yerusalemu, wewe uliyempiga mawe kila nabii!" Angalia hicho kiwakilishi nafsi, mnaona, "Yerusalemu, Yerusalemu, ni mara ngapi mimi …" Yeye alikuwa ni nani? "Ni mara ngapi ningekukusanya pamoja kama vile kuku avikusanyavyo vifaranga vyake, wewe uliyempiga mawe kila nabii niliyemtuma kwako," kanisa lile kuu, Yerusalemu.

155 Yerusalemu isiyo ya hapa duniani, "lakini sisi ni wa Yerusalemu itokayo Juu," mahali linapotoka Neno, kutoka kuchaguliwa tangu asili, mnaona. Si Yerusalemu ya kale inayoangamia; Yerusalemu Mpya isiyoweza kuangamia. Si Yerusalemu ya kale, iliyojengwa na mwanadamu; bali Yerusalemu Mpya iliyojengwa na Mungu, mnaona, Neno kule juu sasa likidhihirishwa. "Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi. Nitaenda na kuwaandalia ninyi,"Muumba akifanya barabara za dhahabu, na kadhalika. Huo Ndio yule usioweza kuangamia.

156 "Yerualemu, Yerusalemu, ni mara ngapi Mimi," tangu mwanzo wa wakati; si Nafsi ya tatu, mtu mwingine, lakini, "Ningewafunika kama kuku alivyofanya kwa vifaranga wake, bali hamkutaka. Lakini sasa saa yako imewadia." Mnaona?

"Palipo na Mzoga, tai watakusanyika." Lakini baada ya mzoga kuoza, ndipo kengewe wanakusanyika. Mnaona?

157 Angalia. Musa, kamwe hakuwapa watoto wa Mungu … Musa alikuwa tai, wala hakuwapa watoto wa Mungu mabaki ya Nuhu. Mnaona? Alikuwa na Neno jipya la Mungu. "Bwana Mungu alikutana nami nyikani, na kulithibitisha Neno Lake, na kunituma hapa kuja kuwaita mtoke." Ndipo wakaja waigaji, wakaigiza. Mnaona? Lakini yeye alikuwa na Neno la wakati huo.

Maana, Mungu alimwambia Ibrahimu, yule aliyekuwa na ahadi, "Uzao wako utakuwa mgeni katika nchi ya kigeni, miaka mia nne, bali nitawazuru na kuwatoa kwa mkono wenye nguvu."

158 Musa alisema, "Sasa, Bwana Mungu atasema nami na kunionyesha, na ameniambia la kufanya, nami nitawaambia." Kasema, "'MIMI NIKO 'alinituma."

"MIMI NIKO!" Si "Nilikuwa, ama nitakuwa." "MIMI NIKO," wakati uliopo, Neno sasa. Si Neno lililokuwako, Neno litakalokuja; Neno lililopo sasa. Mnaona? Mnalipata? "MIMI NIKO!" "MIMI NIKO" ni Neno. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu." Hiyo ni kweli? "MIMI NIKO." "Mungu alinituma kama nabii Wake, kuthibitisha hili kuwa ni kweli. Mimi ni jibu la Neno hili, aliniambia nije hapa chini na kufanya jambo hili."

Na wakati alipofanya jambo hilo, Farao alisema, "Vema, tuna wavulana wengi katika kundi letu wanaoweza kufanya jambo hilo, pia," waigaji.

Yesu alisema, "Sasa, hilo litajirudia tena katika siku za mwisho," mnaona, wakidai jambo lile lile. Angalia ni nani aliyeshuka kwanza. Angalia ni nani aliyedumu na Neno. Hivyo ndivyo ilivyo. Hivyo ndivyo inavyojulikana, kwa hiyo mnaona.

159 Tunaona, Musa kamwe hakuwapa wakati wa Nuhu, "Tutajenga safina sasa, maana hilo ni Neno, mwajua. Nuhu alijenga safina siku moja." La, ndege wala mzoga walikuwa wakila hayo. La, la. La.

Hili ni Neno lililoahidiwa. Angalia, kwa ajili ya ujumbe wake aliokuwa nao kutoka kwa Mungu, alikuwa na Neno halisi la Mungu lililochaguliwa tangu asili kwa ajili ya saa hiyo.

Wala Yesu hakuwapa mabaki ya Musa. Musa alikuwa na Neno la wakati huo, bali Musa alikuwa ni nabii. Huyu hapa Mungu Mwenyewe, mnaona, kamwe hakuwapa mabaki ya Musa—Musa.

Lakini hebu waangalieni tu wale ndege wala mzoga kule kwenye madhehebu hayo, waliokuwa wakijishibisha. "Tunajua! Tuna Musa! Haitubidi kuwa na Wewe."

Yeye alisema, "Kama mngalimjua Musa, mngelinijua Mimi, kwa maana Musa alinena habari Zangu." Loo, jamani! Mnaona?

"Palipo na Mzoga, tai watakusanyika." Tai! Windo jipya la Neno, Neno ambalo limekwishakuzwa na kunona, na limedhihirishwa na kutolewa kama Chakula kwa watoto.

Sasa, mzoga wa kale uliolala pale kwa mamia ya miaka, utakuwa pale.

Vivyo hivyo sasa! Luther alikuwa na ujumbe wa toba; lakini, enyi kundi la kengewa wa Kiluteri! Wabatisti walikuwa na ujumbe; lakini, enyi kengewa wa Kibatisti! Mnaona? Pentekoste ilikuwa na ujumbe; tukija nyumbani sasa, kengewa wa Kipentekoste!

"Lakini palipo na Mzoga, ndipo watakapokusanyika tai."

160 Kumbukeni, msingeweza kumlisha Mlutheri, huko nyuma katika siku hizo (mnaweza sasa), mzoga uliooza wa Katoliki. La, bwana. Alikuwa na nyama mpyai. Huo ulikuwa ndio wakati wa kanisa.

Usingeweza kumlisha Methodisti, ujumbe wa Kiluteri. Loo, la, hakutaka huo mzoga. Umeoza. Mnaona, Uhai tayari ulikuwa umeuacha na kuingia kwenye kitu kingine. Huo ndio ubua wa kale uliokufa, huko nyuma. Uhai unaendelea mbele.

Wala huwezi kumlisha Bibi -arusi wa Yesu Kristo Upentekoste. La, hakika! Madhehebu yaliyojaa mabuu; hayafai kitu! La, la!

Kwa maana ahadi ni, "Na kabla haijaja ile siku kuu na ya kuogofya, nitawapelekea Eliya nabii. Yeye atairudisha mioyo ya watoto iwarudie Imani ya baba zao tena." "Ahadi hizi zote zilikuwa zimetolewa katika Biblia, nitazitimiza, na hapo ndipo watakapokusanyika tai." "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Mnaona?

161 Yesu kamwe hakujaribu jambo hilo. Bali Yesu alipokuja, Yeye aliwakuta hao makundi la ndege wala mzoga uliooza, "Tuna Musa na torati." Mnaona? Vema, hicho kilikuwa ni chakula kizuri huko nyuma wakati kilipouawa nao wakapewa. Mnaona, hilo lilikuwa sawa wakati huo.

Lakini jambo hili ndilo lililobashiriwa na Musa, mwenyewe, aliyechinja ile sadaka, kasema, "Bwana Mungu wako atawaondokeshea kati yenu, mmoja wa ndugu zenu wenyewe, Nabii. Itakuwa, ya kwamba

kila mtu asiyeshika ya Nabii huyo na yale anayosema, atakatiliwa mbali na watu." Na ilikuwa hivyo.

Angalia jinsi karibu nabii mbalimbali mia sita zilizotimizwa papo hapo, wa Agano la Kale, kwa Yesu Kristo. "Waliichoma mikono Yangu na miguu Yangu." Kiasi, nasahau ni ngapi zilitimizwa katika masaa saba ama manane ya mwisho wa maisha Yake, yote waliyosema manabii, kikamilifu.

162 Kama ningelitabiri leo ya kwamba jambo fulani lingetukia katika mwaka mmoja tangu sasa, labda nina —nina uwezekano wa asili mia ishirini kwamba lingetukia, liwe kweli liwe uongo. Na kama nilitabiri ya kwamba hilo lingetukia, wala sikusema ni lini, nina asilimia ndogo zaidi. Kama ningebashiri ni wakati gani lingetukia, linanipa kiasi kidogo zaidi. Kama nilibashiri mahali lingetukia, bado linatoa kiasi kidogo. Kama nilibashiri…itakuwa juu ya nani, basi ningali nina sehemu moja juu ya laki moja ya nafasi kwamba itatimia kamwe, kama si kweli.

Na kila Neno, haleluya, ambalo liliandikwa juu ya Masihi huyo, lilitimizwa kikamilifu. Hata hadi siku moja, akisoma Maandiko, Yeye alisimama moja kwa moja katikati ya sentensi, na kusema,"Roho wa Mungu yu juu Yangu kuihubiri Injili, na kuwaachia huru…" Naye akasimama papo hapo katikati ya sentensi, kwa sababu iliyobaki ni kule Kuja Kwake mara ya pili. Amina! "Mbingu na nchi zitapita; bali Maneno Yangu hayatapita." Mnaona?

163 Yeye alikuwa Neno wakati huo, lililokuwa likiwalisha wakati huo. Musa aliwaambia Kweli; lakini, Mnaona, wao daima hufanya madhehebu kutoka kwake, kwa ajili ya tai …

Kuna baadhi Yake yaliyosalia baada ya tai kula na kwenda nyumbani. Ndipo wanangojea kuona kitu kingine. "Neno," wao wanasema, "hapa linapaswa kuja. Tulikula kulungu jana; kesho tutakula kondoo." Mnaona ninalomaanisha? "Kuna mzoga wa kale uliooza wa kulungu pale, kushangilia, bali tuna kondoo anayekuja leo. Yuko wapi?" Mnaona ninalomaanisha? Chakula cha Malaika! Watu waliokula mana siku moja, kama walijaribu kuitunza kwa ajili ya siku inayofuata, iliambukizwa. Hivi hamwoni mifano yote, namna ilivyo kamilifu? Vivyo hivyo sasa!

164 Angalia, wale nderi wa siku za Yesu pia walikuwa wakiwatoa pepo; waliotiwa mafuta juu ya huo mzoga wa kale. Hiyo ni kweli? Walikuwa wakitoa pepo. Yesu alisema hivyo.

Pia kumbukeni, walikuwa na manabii katika siku hizo. Kayafa, kuhani mkuu, alitabiri. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Kayafa alitabiri. Angalia mahali pa magugu katika shamba; yanamwagiliwa maji kwa upako ule ule. Kwa nini Biblia ilisema alitabiri? "Kwa sababu alikuwa kuhani mkuu mwaka huo." Mla mizoga aliyeoza, magugu na mwiba, ikikaa kati ya Ngano; bali Roho alikuwa juu yake, Roho Mtakatifu halisi wa Mungu. Roho Mtakatifu wa Mungu alikuwa juu yake, kuhubiri, kutabiri, na kubashiri litimie; kisha akalikana na kulisulubisha Neno lile lile lililothibitishwa la wakati huo.

Loo, rehema, ndugu! Ni muda gani zaidi itatubidi kusema mambo haya, mnaona, ni zaidi sana vipi katika Maandiko? Nitaharakisha. Nina kama kurasa kumi hapa, za Maandiko, namna ya kuthibitisha mambo yote. "Jua juu ya wenye haki na wasio haki, vivyo hivyo."

165 Yesu alisema, kuthibitisha jambo hili. "Kama nikitoa pepo kwa kidole cha Mungu, wana wenu wanawatoa kwa nani?" Sasa, walikuwa wakitoa pepo. Walikuwa wakitabiri. Hiyo ni kweli? Lakini hawakumtambua Yeye kuwa Neno la wakati huo, (kwa nini?) kwa sababu Yeye hakushirikiana nao.

Sasa chukua Mathayo 24:24, "Makristo wa uongo," waliotiwa mafuta, "watainuka, na watakuweko manabii wa uongo wakitabiri," mnaona, "nao watawapoteza Walioteuliwa kama yamkini." Mmelipata sasa?

166 Angalia watoto. "Ni nani watoto … Kama nikitoa pepo kwa Neno la Mungu," ambalo, Yeye alikuwa Neno la Mungu,"watoto wenu wa kimadhehebu huwatoa kwa nani?" Sasa, na Mungu pekee ndiye anayeweza kumtoa pepo, tunajua jambo hilo, Mungu peke yake. Kwa maana, mtu mwenye nguvu hana budi kuwa na nguvu kuliko yule aliye nyumbani mwake. Walikuwa na nguvu za kufanya jambo hilo.

Mnajua, katika Ufunuo pale, alisema angemwamini … yule mpinga -Kristo aliyefufuka katika siku za mwisho, "Alifanya ishara na maajabu, ambaye hata aliwadanganya hao wakaao juu ya uso wa nchi, na kumdanganya kila mmoja wao, Wakristo na wote, ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana -Kondoo," jibu la Mathayo 24:24,"ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana -Kondoo tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu."

Huo Uhai uliokuwemo katika shina la mchungwa huo—huo halisi, ambao ulipitia katika hiyo jamii ya mibalungi na kadhalika, kisha ukapita na kuzaa tunda juu ya huo mti, juu ya mapandikizo yote ya kimadhehebu na matawi. Mmelipata? Nitaharakisha. Yule mtu mwenye nguvu …

167 Kumbukeni Daudi sasa, alikuwa mwaminifu, mwaminifu, akijaribu kumfanyia Mungu kazi, wala hakuamriwa kuifanya.

"Wao," waliotiwa mafuta; bali Yesu alisema, "Wanafundisha Mafundisho tafsiri (ya Maandiko) ya mwanadamu," mnaona, si Neno la Mungu, si Neno Lake lililothibitishwa; akifundisha Kristo wa kihistoria,

mnaona, jambo fulani lililokuwako.

Na Biblia ilisema, “Ndiye.” “MIMI NIKO,” si “Nilikuwa ama nitakuwa.” “MIMI NIKO, sasa hivi.” Yeye ni lile Neno linaloishi hapa.

Yeye alikuwa, hapo mwanzo, alikuwa katika … Yeye alikuwa katika yale—yale majani; Yeye alikuwa katika kishada; Alikuwa kwenye kapi; bali sasa Yeye yuko katika Punje.

168 Sasa, unarudi nyuma na kujaribu kuishi tena? Naam, unarudi nyuma na kujaribu kuishi tena? Vipi kama Uhai huo ungalirudi kule chini, unafikiri Uhai (uliosalia) huo ungalizungumza kamwe, urudi baada ya kapi hilo la kale kukauka, ungerudi kamwe na kuishi ndani yake tena? Haufanyi namna hiyokamwe. “Kwa maana haiwezekani kwa wale waliokwisha kupewa nuru,” nao hawakusonga mbele pamoja na Neno hapo lilipotimia, “wao wamekufa, wamekwisha; na miiba na michongoma ambayo huwa karibu kukataliwa, ambayo mwisho wake ni kuteketezwa.” Hiyo ni kweli?

Sasa kuharakisha upesi tu niwezavyo.

169 Angalia Maandiko sasa. Angalia Maandiko sasa. Kufundisha Mungu wa kihistoria, mnaona, kama tu wanavyojaribu kuishi katika wakati uliopita, kama vile, “Vema, Wesley alisema kitu fulani. ”Vema, Wesley alisema kitu fulani. Ama, Fulani alisema kitu fulani.“ Unakataa Neno lililoahidiwa la siku hiyo, Mana iliyotambulishwa dhahiri ya siku hiyo. Wanajaribu kuweka divai yao ya kale ya Kiluteri, Baptisti, Pentekoste katika chupa zetu mpya. Haifai kitu. Na Divai yetu mpya, katika chupa zao za kale, haitafaa kitu. Kama wakijaribu kuweka Divai hii mpya katika madhehebu, upumbavu wao unadhihirishwa. Hawawezi kufanya hivyo. Inaipasua.

“Sasa, ndugu, niliona Neno la Mungu, kikamilifu kwa Neno!”

“Sasa, angalia hapa, daktari, kama … Ha—hatuwezi kuchukua Hilo.” Ned, nafikiri umekuwa na baadhi ya hayo siku za hivi majuzi. “Sisi, hatuwezi kuwa na Hilo hapa sasa. Ni—ningependa labda wewe uendelee tu.” Mwajua. Mnaona, haifai kitu. Inapasuka.

“Huweki kitambaa kipya kwenye nguo kuukuu, maana utaifanya yote iraruke.” Mnaona? Je! Yesu hakusema hivyo? Huwezi kuweka Mvinyo mpya katika chupa za kale. Itazipasua. Divai mpya ina Uzima ndani yake. Vema.

170 Angalia hapa jambo fulani, upesi sana sasa, tunapomalizia … mazungumzo yetu. Angalia Ufunuo 16:13 hadi 14, kama unataka kuandika hilo. Sitakuwa na wakati labda wa kuliendea. Ninawatakeni muwe na hakika na muone jambo hilo. Sasa angalia, huku ni kupiga baragumu kati ya Kitasa cha Sita na cha Saba.

Sasa tunaninii … tutafunga kwa dakika moja, kama mnaweza tu kuvumilia kwa dakika chache zaidi. Tunafunga sasa.

Angalia. Ufunuo 16:13 hadi 14, kati ya Kitasa cha Sita na cha Saba, “Roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura” (mliona jambo hilo?) ?) “zikatoka katika kinywa cha mtu fulani.” Sasa angalia, upesi. Uko tayari? Sema, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.” — Mh.] Utatu wa roho!

171 Sasa ndugu wa kimadhehebu, kaeni kimya kwa dakika moja tu. Usisimame na kutoka chumbani, huko nje kwenye redio hii, mawasiliano ya simu. Usizime kinasa sauti chako. Keti kimya kwa dakika moja tu, na usikilize. Umezaliwa na Mungu, utafanya hivyo.

172 Utatu wa vyura! Chura ni mnyama ambaye daima hutazama nyuma. Yeye kamwe haangalii anakoenda; anaangalia alikotoka. Mnaona? Hivi hamwoni? Utatu ulizaliwa wapi? Kumbukeni, “pepo watatu wachafu,” roho binafsi. Je! Mnalipata? [Kusanyiko linasema, “Amina.” — Mh.]

Angalia, wanaangalia nyuma kwenye Baraza la Nikea ambako fundisho la utatu lilizaliwa, si katika Biblia. Hakuna kitu kama hicho. Wanaangalia nyuma kwenye Baraza la Nikea huko Nikea, Rumi, ambako utatu ulizaliwa.

Angalia walikotoka. Angalia. Na utatu wa vyura ulitoka kwenye utatu wa kale, ukazaa utatu mpya, mama yao. Ulitoka wapi? Utatu, “yule joka,” unaona, “yule mnyama,” na “nabii wa uongo.” Utatu, mpya. Kwani vyura hawa walitoka lini? Walitoka lini? Angalia, walikuwepo sikuzote, bali hilo halikudhibitishwa mpaka kati ya Kitasa cha Sita na cha Saba, kabla tu ya zile Muhuri kufunguliwa na kulifunua.

“Kwa maana katika Ujumbe wa malaika wa saba, siri za Mungu zingejulikana,” mambo haya yote ya utatu, na ubatizo wa uongo, na kila kitu kilipaswa kudhihirishwa. Mungu na atusaidie kuona lililo Kweli! Na siyo kufikiri ati ni mtu fulani akijaribu kusema jambo fulani ku-…

173 Ninahisi hiyo roho ikichukizwa na jambo Hilo, mnaona. Mimi sizungumzi mimi mwenyewe, ndugu. Ninazungumza juu ya Malaika wa Bwana aliye kambini. Hiyo ni kweli kabisa.

Angalia, utatu! “Joka,” ni wangapi wanaojua lile joka? Ilikuwa ni Rumi. “Na yule joka akasimama mbele ya yule mwanamke amle mtoto wake mara tu atakapozaliwa.” Hiyo ni kweli? Nini maana ya “mnyama” katika Biblia? Nguvu. Vema. “Nabii wa uongo, nabii wa uongo,” wa uongo, aliyetiwa mafuta. Mnaona?

174 Ilianzia wapi? Huyu ni “nabii wa uongo,” umoja. “Nabii wa uongo,” papa wa kwanza; na kutoka hapo akatoka “yule—yule kahaba, na mama wa makahaba,” kitu hicho chote.

Utatu wa uongo ulikuwa unainuka; si katika siku za mwanzoni, haungedhihirishwa katika siku za mwanzoni, ulisonga mbele moja kwa moja pamoja nao. Lakini wakati ile Mihuri Saba ilipokuja, na kuzifungua hizo siri na kuzifunua; hapo ndipo “wale vyura, pepo watatu wachafu kama vyura, walipojitokeza kujidhihirisha,” fundisho la utatu dhidi ya ile Kweli. Mnaona? A -ha!

Mnaona mahali lilipotoka? Mnaona mahali linaporudi? Baraza la Ekumeni. Wote ni ndugu, hata hivyo; roho zile zile, jambo lile lile.

Basi angalia. Ni wadanganyifu sana, wanafanya miujiza! Na hawa ni pepo wanaokwenda kwenye miungu wote wa dunia, wakifanya miujiza, kuwadanganya katika siku ya mwisho, nao watafanikiwa katika kufanya jambo hilo. Mungu alisema nini juu ya huyo pepo mchafu?

Kasema, “Nitashuka niende niingie katika kinywa cha manabii hao na kuwafanya watabiri uongo, kumfanya Ahabu atoke aje pale akaangamizwe.”

175 Mungu alisema, “Nenda. Utafanikiwa. Utawafanya waamini jambo hilo. Hawako kwenye Neno hilo, kwanza.” Mnaona? “Nenda, kwa maana utamshawishi. Wewe ndiwe utakayefanya jambo hilo, utakapoingia katika hao manabii wa uongo, maana yeye anawategemea moja kwa moja. Wala hajui kitu juu ya Neno, wala hatajaribu kujifunza juu Yake. Hawezi kufanya hivyo, kwa sababu yeye ni mwiba, kwanza.” Mnaona? Mnaona? “Utafanikiwa.”

176 Angalia hapa hawa vyura wa uongo, wakiangalia nyuma, “Mbona, mnajua walichosema huko nyuma huko Nikea?”

Sijali walisema nini, huko Nikea. Ninasema waliyosema hapa kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu; kitakachotukia, si kilichokuwa; kitakachotukia, kwa maana Yeye ni “MIMI NIKO.” Mnaona?

“Uongo.” Angalia jambo hilo. A -ha! Angalia walikotoka.

177 Sasa sikilizeni kwa makini. Tunaona dhahiri, baada ya ile Mihuri Saba kufunguliwa, hiyo ni kufunua siri hiyo. Utatu huo ni nini? Mnaona? Ni wapi ulipowahi kuitwa utatu? Mnaona? Ni wapi katika Biblia ambapo hata lilinena neno utatu? Ni wapi kungeweza kuwa na Miungu watatu, hata tuabudu Miungu watatu na tusiwe wapagani?

Wanawezaje kutengana, wakati Yeye aliposema, “Mimi na Baba Yangu ni Mmoja”? “Msipoamini ya kwamba Mimi Ndiye, mtaangamia katika dhambi zenu, mnaona, kutokuamini kwenu.” Dhambi ni kutokuamini. “Utaangamia katika kutokuamini kwako.”

Loo, mnasema mimi ni nani, mlisema nimetoka wapi,
Loo, mnamjua Baba Yangu, ama mnaweza kujua Jina Lake?
MIMI NIKO Waridi la Uwandani, Nyota ya Asubuhi Ing'aayo.

Unaweza kuniambia Yeye ni nani?

MIMI NIKO aliyenena na Musa katika kijiti kilichowaka moto,
MIMI NIKO Mungu wa Ibrahimu, Nyota ya Asubuhi Inayong'aa.
MIMI NDIYE Ua la Uwandani, loo, ulisema nimetoka wapi;
Loo, unajua Baba Yangu, ama unaweza kulitangaza Jina Lake? (Amina!)
MIMI NIKO Alfa, Omega, Mwanzo kutoka Mwisho;
MIMI NIKO uumbaji wote, na Yesu ndilo Jina Lake.

178 Hiyo ni kweli. Hakuna utatu! La, bwana. Hilo ni jambo la uongo.

Ile Muhuri Saba, ikizifungua siri hizo ambazo zinapaswa “kumalizwa,” kunatokea. Muhuri unafunguliwa; unaandaa, unaonyesha, unafanya dhahiri Kweli zilizofichwa ambazo zile Muhuri zilikuwa zimeficha miaka hii yote, kupitia makanisa hayo yote na madhehebu.

“Huyo kahaba mkuu,” wa Ufunuo saba- … Yeye alikuwa nani? Lakini yeye ni “MAMA WA MAKAHABA,” pia. Mnaona?

179 “Sasa, uliwaita 'nderi,'” unasema, “Ndugu Branham.” Hiyo ni kweli.

Lakini, kumbukeni, nderi ni ndege. Yeye ametiwa mafuta apate kuruka, pia. “Roho hizo mbili ziwe karibu sana zingewapoteza walio Wateule …” Nderi ni mkubwa kama—kama tai. Yeye angeweza kuruka kama huyo tai; naye ana upako wa kuruka, ama kuhubiri, ama kutabiri, angalia, sawasawa na tai. Lakini

yeye hawezi kumfuata tai kwa urefu. La, la. Kama akijaribu kumfuata yule tai, upumbavu wake utadhihirishwa. Naam, bwana. Hawezi kumfuata yule tai.

Loo, anaweza kusema, "Ninaamini katika Yesu Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu. Ninaamini Mungu Baba, Mwenyezi, Muumba wa mbingu na nchi; Yesu Kristo Mwanawe, na kadhalika." Loo, hakika, wanaweza kufanya hivyo. Lakini vipi kuhusu Yeye kuwa yeye yule jana, leo, na hata milele? Mnaona?

180 Tai ni ndege aliyeumbwa maalum. Hakuna kitu kama yeye, duniani. Mnaona? Yeye—yeye … Kama mwewe akijaribu kumfuata, ama ndege mwingine ye yote, angevunjika -vunjika. Upumbavu wake ungefunuliwa, hakika kabisa. Yeye angelipuka wakati angejaribu kuweka Mvinyo mpya katika chupa ya kale. Mnaona, angelipuka. Angevunjika -vunjika. Yeye hajafanywa, haja-… Mwili wake haujaundwa pamoja kwa muundo wa kustahimili kule juu. Anapofikia katika mazingira yale makuu kule juu, kama yeye hakufanywa, kuagizwa, kuchaguliwa tangu zamani, kuzaliwa tai, atapasuka vipandevipande. Mnaona? Manyoya yangeruka yatoke kwenye mabawa yake, naye angeanguka ardhini. Hakika. Hawezi kumfuata yule tai, kwa urefu. Kama akijaribu kufanya hivyo, upumbavu wake utadhihirishwa. Hiyo ni kweli. Huwezi.

181 Kwa nini? Hawezi kuona kama tai. Inafaa nini kujaribu kuruka juu sana, na huwezi kuona mahali ulipo wakati uko juu? Na kama angejaribu, hata kujaribu kumwiga tai huyu, kule juu sana, yeye anakuwa kipofu sana hajui amefikia wapi. Hiyo ni kweli. Yeye anapiga makelele na kupaza sauti, na kufanya yasiyofaa; bali mwambie tu Neno, jamani, hapo upumbavu wake unajulikana.

Nena naye kuhusu ubatizo katika Jina la Yesu Kristo, ama, Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, yote—yote namna hiyo, na umwambie. "Mbona, loo, sasa ngoja kidogo!" Mnaona? Loo, naam, pale manyoya yake yanadondoka. Mnaona, yeye ameruka juu kabisa, na kutoa unabii, na kutoa pepo, na kunena kwa lugha, na kupiga makelele, na kufanya yasiyofaa, akipiga mbio huku na huko sakafuni. Bali usijaribu kumfuata Kule juu; mbona, yeye bila shaka atajulikana.

Hata hivyo, yeye amechaguliwa. Yeye ametiwa mafuta. Anaweza kuruka. Anaweza kujisawazisha, aende kule, bali si … umbali tu. Mnaona, anaweza kula mzoga uliooza, bali hawezi kula Nyama mpya inayotoka kwenye Kiti cha Enzi.

Yeye ni kipofu. Yeye amechochewa sana, bali hajui amechochewa juu ya kitu gani. Mnaona, Roho yule yule aliyeshuka juu yake, kama mvua, kumfanya ngano; kwanza yeye si ngano. Yeye analipuka. "Loo, siwezi kwenda … Loo, la, bwana! Ninajua Daktari Jones alisema …" Vema, endelea. Mnaona? Endelea, kama unataka.

182 La, angalia, yeye hajazaliwa, ama kujengwa, wala kuchaguliwa tangu zamani, kuwa ndege wa namna hiyo. Anaweza … Yeye ni…huenda akawa limau linalokua kwenye mchungwa, bali hakutoka kwenye mashina kamwe. Yeye ni kitu ambacho kimeongezwa. Na wakati wanapokuwa juu sana katika madhehebu yao hivi kwamba hawawezi kuona Neno la Mungu lililochaguliwa tangu asili likithibitishwa, basi upumbavu wao unajulikana. "Loo, upuzi huo, Duara juu ya kichwa, na kadhalika, loo, Hiyo ni upuzi." Mnaona? Unajulikana.

183 Yeye hajajengwa apate kuona umbali huo. Yeye anaweza tu kuona kadiri miwani yake ya kimadhehebu itakavyomruhusu kuangalia. Lakini, baada ya hayo, yeye ni kipofu kama popo. Hapo ndipo upumbavu wake unapojulikana. Mnaona? Hapo ndipo tai wa kweli anapoketi apate kula. Naam, bwana. Hapo ndipo tai wa kweli walioteuliwa wanapoona yeye ni nani. Wakati asipoweza kuchukua Neno hilo, wanajua papo hapo yeye ni nderi wa kimadhehebu.

Mbona, mbona hawezi kuruka? Maana, angalia kile alichokuwa akila. Amekuwa akila mizoga iliyooza ya kimadhehebu. Hilo halita—hilo halitafanya mwili wake kuwa wa kiroho, halitamweka katika afya ya kiroho, kwa maneno mengine, kumpeleka juu ya tofauti za kimadhehebu. Mnaona? Mnaona, yeye amelishwa tu vitu vilivyooza; mwili wake umetengenezwa kwa hiyo. Yeye hawezi kwenda huko juu ambapo hiyo Nyama safi humbeba huyo tai. Hawezi kufanya hivyo. Mnaona?

184 Hilo linatimiza Mathayo 24:24. Yeye anaruka, akiruka juu hewani, akipeperusha mabawa yake, bali hawezi kabisa kuwa juu vya kutosha. Mnaona? Hiyo ni kweli. Mnaona, yeye hawezi kwenda, hawezi kufikia juu vya kutosha kupata hiyo Mana mpya. Anaweza kula ile mana ya kale iliyo hapa ardhini, sungura wa kale waliokanyagwa na gari juma moja lililopita, na mwezi mmoja uliopita, ama miezi arobaini iliyopita, kuambukizwa. Anaweza kula hao, na kuwafurahia tu, kulia na kupiga mayowe, na kupiga makelele, na kuruka na kupuruka kama tai mwingine. Yeye ametiwa mafuta, kama ndege mwingine.

Naye ni mfano wa tai, ni kengewa. Tunajua jambo hilo. Hakika ndivyo alivyo, bali hawezi kumfuata tai huyo halisi. Mnaona? Hawezi kufanya hivyo. La, bwana. Mwili wake hakujengwa; amekuwa akila mzoga wa aina nyingine uliooza, mnaona, na haitakuwa…haitakuwa— haitakuwa Nyama mbichi, Mana mpya. Ingekuwa ni jambo ambalo Luther alisema, Wesley alisema, ama Daktari Fulani alisema. Haitatokana na yale Yesu aliyosema kwa ajili ya saa hii.

185 Hebu na twende sasa, karibu. Waliotiwa mafuta, "Makristo," katika siku za mwisho, bali "waalimu wa

uongo na nabii wa uongo." Angalia jinsi inavyoshangaza! Sasa nawatakeni mlinganishe hili; hatuna wakati wa kulisoma, Mathayo 24:24 na Timotheo wa Pili 3:8.

Mathayo 24:24 ilisema, katika siku za mwisho, mnaona, "Watatokea Makristo wa uongo," watu wa uongo, waliotiwa mafuta, "manabii wa uongo, nao wataonyesha ishara na maajabu," kama Yeye aliye—aliye wa kweli hasa, "nao karibu wata—nao karibu watawapoteza Walioteuliwa." Sasa angalia, huyo alikuwa ni Yesu akinena.

186 Huyu hapa Paulo anakuja, moja kwa moja nyuma Yake, akasema, "Naam, katika siku za mwisho, kutatokea watu wa kidini, mnaona, wenye mfano wa utauwa. Na kuchukua mateka wanawake wajinga, waliochukuliwa na kila namna ya tamaa za ulimwengu."

Nao wanashangaa, wanasema, "Kwa nini mnawachukia hao wanawake?" Loo, kwa wema … Hata hawalioni.

"Wanawachukua mateka wanawake wajinga, waliochukuliwa na kila namna ya tamaa," kutoka kwa mambo kama kwenye…ya… Mnaona, "Na kama vile Yane na Yambre …"

Mathayo 24:24, "Makristo wa uongo," wa uongo, waliotiwa mafuta, wakitenda ishara na maajabu wapate kuwapoteza walio Wateule.

"Sasa kama vile Yane na Yambre walivyompinga Musa, vivyo hivyo hawa waliokataliwa; waliokataliwa kwa mambo ya Imani." Si imani, "Imani!"

"Imani moja, Bwana mmoja, ubatizo mmoja …" Huwezi kuwa na "Imani moja" bila kuamini "Bwana mmoja." Huwezi kuwa na ubatizo mara mbili, wala hakuna mmoja kwa ajili ya Baba, na Mwana, Roho Mtakatifu. "Ubatizo mmoja," Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Mnaona, ubatizo wa uongo!

187 Angalia, linganisha hayo pamoja sasa unapofika nyumbani. Angalia Mathayo 24:24, Yesu akinena; Paulo, 2 Timotheo 3:8; wengine wengi. Na sasa linganisha jambo hilo.

Na halafu weka Andiko lingine, Luka 17:30, Malaki 4.

"Kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa," Neno lililotiwa mafuta la wakati huo, "vivyo hivyo na watu hawa," si mtu, "watu," waliotiwa mafuta, "wanapingana na ile Kweli."

"Katika siku ile ile atakapofunuliwa Mwana wa Adamu." Ufunuo 10:1 hadi 7, isome unapofika nyumbani, "Ujumbe wa malaika wa saba, kuifungua ile Mihuri." Ni kitu gani? Si yule malaika ni Mwana wa Adamu; bali huyo mjumbe anamfunua Mwana wa Adamu. Mnaweza kulitenganisha sasa? Hapo ndipo linapoonekana kuwa gumu sana kwenu, mnaona. Si Mwana wa Adamu, Mwenyewe; bali malaika wa saba, mjumbe wa saba, anawafunulia watu Mwana wa Adamu, kwa maana imeondoka kwenye kapi. Hawezi kulifanya madhehebu. Ni Punje, Yenyewe, tena.

"Na katika siku hiyo, Yane na Yambre watashindana," waliotiwa mafuta (wanaojifanya waamini na wasioamini, kanisa la kirasmi na la Kipentekoste) watashindana na ile Punje ya kweli, "bali waacheni; upumbavu wao utadhihirishwa, kama vile wao ulivyokuwa." Mnaona? Mnaelewa sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

188 Ufunuo 10, ulisema, "Katika siku za kupigwa kwa baragumu ya malaika wa saba." Sasa kumbukeni, ya saba, Wakati wa Kanisa la Laodikia. "Kupigwa kwa baragumu ya malaika huyo," wakati huo wa kanisa tayari umeunda madhehebu na ukawa wakati wa kanisa, hapo unapomalizika katika madhehebu yake ya Kipentekoste; wakati yule mjumbe wa huo…

Kila mjumbe alikuwa nini? Martin Luther alikuwa nini? Karipio kwa Mkatoliki. Wesley alikuwa nini? Karipio kwa hao Walutheri. Pentekoste ilikuwa nini? Karipio kwa hao wengine. Uhai umeenda wapi sasa? Mbali na madhehebu. Hakuna tena kapi; ni Punje. Ni kitu gani? Karipio kwa Wapentekoste, mnaona, kutimiza Maandiko ya wakati huu. Mnaona?

189 Angalia, siku ile ile ambapo mjumbe huyu … Si wakati anapoanza, bali anapoanza kutangaza Ujumbe wake. Mnaona? Mvuto wa Kwanza, uponyaji; Mvuto wa Pili, unabii; Mvuto wa Tatu, kule kufunguliwa kwa Neno, zile siri zilizofunuliwa. Hakuna tena, hakuna utaratibu wa juu zaidi wa kulifunua Neno, kuliko manabii. Lakini njia pekee ambayo nabii anaweza kuthibitishwa ni kwa Neno. Na, kumbukeni, ule Mvuto wa Tatu ulikuwa ni kufunguliwa kwa hiyo Mihuri Saba, kufunua Kweli iliyofichwa ambayo imetiwa muhuri katika Neno. Mnaona jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

Ni wakati huo, katika siku hiyo jambo hili litakapotukia, ambapo Yane na Yambre, waigaji, wataonekana tena. Kama tu walivyofanya wakati Musa alipotokea na Neno la asili, kulisema Hilo; wao wanatokea kuliiga Hilo. Sawa kabisa. Sasa mnaona Mathayo 24:24 ni nini? Mnaona, mliotiwa mafuta!

190 Sasa kuna mambo matatu tutakayosema kabla hatujafunga. Ni haya. Ninawatakeni msikilize kwa

makini sana sasa tunapofunga. Mambo matatu, kumbukeni, mambo matatu yametimizwa. Mambo matatu yako mbele yako sasa hivi.

Kwanza. Ulimwengu uko katika hali ya Sodoma. Yesu alisema lingetukia. Angalia huo upotovu; wanawake wetu wakijaribu kutenda kama wanaume; wanaume wetu wakijaribu kutenda kama wanawake, dondoadume; wameoza, wachafu, ni duni sana, wamepagawa na pepo, nao hawajui hilo. Biblia ilisema hilo lingetukia, na hapo ndipo lilipo.

Pili. Ni katika saa hiyo, kulingana na Maandiko hapa, ambapo Yane na Yambre wanaonekana. Pili.

Tatu. Ni kwenye wakati uo huo ambapo Mwana wa Adamu atafunuliwa.

191 Huyo hapo mwamini wako, anayejifanya mwaminio, na asiyeamini. Hilo hapo Neno lililo halisi limesimama wazi, limethibitishwa; huyo hapo anayejifanya anaamini akiliiga; na huyo hapo asiyeamini akilikataa jambo lote.

Lakini itakuwa Nuru yapata wakati wa jioni,
Njia ya kwenda Utukufuni hakika mtaipata. (Hiyo ni kweli?)
Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara ambazo Biblia yetu ilitabiri;
Nazo siku za Mataifa zimehesabiwa (Sodoma), zimekubwa na hofu;
Rudini, enyi mliotawanyika, nyumbani kwenu.
Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya wanadamu inavunjika, katika hofu hii;
Jazweni na Roho wa Mungu, zitengenezeni taa zenu na mzisafishe, (kusudi mpate kuona Neno la wakati huu,)
Angalieni juu, ukombozi wenu umekaribia!
Manabii wa uongo wanadanganya, (wao walisema wangekuwa hapa; watiwa mafuta),
Kwamba Yesu Kristo ni Mungu wetu.

Hiyo ni kusema, hawaamini jambo Hilo. Biblia ilisema kungekuwako na kitu hicho hapa. Hiki hapa!

Bali sisi tutatembea ambapo mitume wamekanyaga. (Nuru ile ile! "Na kuirudisha imani ya baba iwaelekee watoto wao.")
Siku ya ukombozi imekaribia, iko karibu sana,
Mioyo ya wanadamu inavunjika kwa sababu ya hofu, (dunia inadidimia);
Loo, jazweni na Roho wa Mungu, zitengenezeni taa zenu na mzisafishe.
Angalieni juu, ukombozi wenu umekaribia.

Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Hebu na tuinamishe vichwa vyetu basi.

192 Huko nje kwenye nchi ambako Ujumbe huu unaenda, kutoka Pwani ya Mashariki hata ya Magharibi, kutoka California hata New York, huko chini Kusini, huko juu Kaskazini, huko nje kwenye umisheni, na po pote unapokwenda, na katika Maskani haya. Sisi ni maskini. Hatuna mambo haya makubwa, makubwa, ya kupendeza, na televisheni. Tunajaribu tu kufanya vizuri tuwezavyo. "Lakini wote alionipa Baba watakuja."

193 Sasa, ninawatakeni mjue jambo hili ni hakika, nanyi mnaosikiliza kanda hii. Huenda mkafikiri leo kwamba nilikuwa nikinena habari zangu, kwa kuwa nilikuwa nikiubeba Ujumbe huu. Mimi sina uhusiano nao kamwe, si zaidi ya sauti. Na, sauti yangu, hata dhidi ya uamuzi wangu mzuri zaidi; Nilitaka kuwa mtegaji. Lakini ni mapenzi ya Baba yangu ambayo ninatangaza kufanya, na nimeazimia kufanya.

Sikuwa Mimi niliyeonekana kule chini mtoni; Nilikuwa nimesimama pale tu wakati Yeye alipotokea. Si mimi ninayefanya mambo haya na kuyatabiri mambo haya yanayotukia kikamilifu yanavyofanya; mimi ndiye tu ninayekuwa karibu wakati anapoyafanya. Mimi nilikuwa tu sauti aliyoitumia Yeye, kusema jambo Hilo. Mimi nilikuwa tu sauti aliyoitumia Yeye, kusema jambo Hilo. Haikuwa yale niliyojua; ni yale niliyojitolea kwake tu, Yeye alinena kupitia. Si mimi, haikuwa malaika wa saba, loo, la; ilikuwa ni dhihirisho la Mwana wa Adamu. Haikuwa malaika, ujumbe wake; ilikuwa ni ile siri ambayo Mungu aliifunua. Si mwanadamu; ni Mungu. Yule malaika hakuwa Mwana wa Adamu; alikuwa mjumbe kutoka kwa Mwana wa Adamu. Mwana wa Adamu ni Kristo; Yeye Ndiye mnayejilisha. Hamjilishi mwanadamu; mwanadamu, maneno yake yatashindwa. Bali mnakula Mwili-Neno lisiloshindwa la Mwana wa Adamu.

Kama hamjajilisha kikamilifu kwenye kila Neno, kujipa nguvu kuruka juu ya madhehebu haya yote na mambo ya ulimwengu, unaweza kufanya hivyo wakati huu, tunapoomba?

194 Baba mpendwa, hili ni jambo gumu. Si rahisi kwa mwanadamu anayepatikana na mauti kulifanya. Wewe unajua mambo yote. Nami ninakuomba, Mungu mpendwa, ya kwamba hilo halitaeleweka vibaya. Lakini, katika Nuru ya Neno Lako, jalia watu waenende.

Na, Baba Mungu, sijui Wateule ni akina nani; Wewe wajua. Sijui Kuja Kwako kutakuwa lini. Bali ninajua tu ya kwamba ulisema haya yatakapotukia, hawa waliotiwa mafuta wa uongo; si mara walipoanza.

Musa aliwaacha peke yao tu, kwa maana asingefanya kitu juu yake. Yeye angeweza tu kusema yale uliyokuwa ukisema. Ulimwambia aite viroboto; halafu wao wakawaita. Ulimwambia ageuze maji kuwa damu; kisha wakayageuza. Musa alitekeleza tu, Neno kwa Neno, kama ulivyosema Wewe, bali Wewe Ndiwe uliyedhihirisha huo upumbavu.

195 Sasa, Baba, Wewe ni Mungu, bado. Neno lile lile lilisema ya kwamba jambo hili lingetukia katika siku za mwisho. Watu wengi waaminifu, kama tulivyosema Jumapili iliyopita, wakiweka mikono yao kwenye Sanduku lile lililokuwa kwenye gari jipya, na si mabega ya Walawi, wameanguka wakafa, "wamekufa katika dhambi na makosa," wanabishana dhidi ya dhamira yao wenyewe.

Wahudumu wengi wanaoketi katika chumba chake cha kusomea, wanalisoma Neno hilo, na kugeuza karatasi upesi; wasije wakapasuka, kujua ya kwamba atachukiwa na watu, pamoja na kanisa lake na madhehebu yake. Mungu na atusaidie kamwe tusifanye hivyo!

196 Safisha mioyo yetu, Bwana, na uchafu wote wa ulimwengu. Bwana, ninasimama tayari kwa ajili ya utakaso. Ninasimama nikiwa tayari, pamoja na kanisa hili na watu wote wanaosikiliza, na yeyote atakayesikiliza kanda hii. Ninasimama, Bwana, na kuomba kusafishwa. Bwana, nipeleke kwenye kituo cha mfinyanzi kisha univunjevunje, nifinyange niwe mtumishi ambaye ungemtaka Wewe.

Kwa kuwa, Bwana Yesu, "Mimi ni mtu mwenye midomo michafu," kama alivyolia Isaya, "nikikaa pamoja na watu wenye midomo michafu; na ole wangu, kwa kuwa ninauona ufunuo wa Mungu ukidhihirishwa," kama vile Isaya alivyowaona Malaika Hekaluni. Nimeona wakati wa mwisho, Bwana, na ole wangu na jamaa yangu; ole wangu na watu wangu. Ee Mungu wa Milele, uturehemu. Ninajiombea mwenyewe na hawa watu. Na tusiangamie pamoja na wale wasioamini, bali jalia tuishi pamoja na waaminio.

197 Kila dhehebu, Bwana, kila mwanamume ama mwanamke … Siwezi kukuomba ulibariki dhehebu, wakati ninapojua Wewe unapinga jambo hilo. Lakini naweza tu kusema, Bwana, kama una kondoo Wako yeyote miongoni mwao, jalia wasikie kanda hii. Naomba waisikie, Bwana, na waielewe kwa ufahamu utakaowapa Wewe, nao na watoke waje wakupokee Wewe. Jalia wasidanganywe na upofu na mapokeo ya siku hii. Jalia wasijaribu kula kitu ambacho … ama ilikuwa ni mzoga katika siku nyingine. Hebu wachukue Neno.

Hivyo ndivyo Mafarisayo walivyokusulubisha Wewe, Bwana. Walikuwa wakichukua mzoga wa siku za Musa, na kujaribu kuufurahia; baada ya Wewe kutoa mfano, jangwani, wa mana mpya kila usiku, ikimaanisha kila kizazi. Hapo ndipo waliposhindwa. Uliwatia sumu. Uliwaua, kula chakula hicho kilichokuwa kimeambukizwa.

Na, kiroho, inafanya jambo lile lile leo; inawaua, kiroho, kwa madhehebu.

Tusaidie, Mungu mpendwa. Yote yako mikononi Mwako sasa. Katika Jina la Yesu Kristo.

198 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, tutaimba huo wakati mnapofanya uamuzi wenu. Je! Utaenda njia yote?

Naweza kumsikia Mwo-…(naye ni Neno) …-ngu akiita ...

"Loo, nilitangatanga wakati mrefu, lakini, kweli, sasa hivi namsikia,'Njoni Kwangu, ninyi nyote mnaoenda mkipapasa.' Sikilizeni, 'chukua msalaba wako, unifuate Mimi kila siku.' 'Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya; katika malisho ya majani mabichi hunilaza, Kando ya maji ya utulivu huniongoza.'"

Nako aniongozako mimi…

"Bwana, ninauona huo upumbavu wa utatu. Ninaona ulimwengu mzima ukipandwa ndani yake; magugu yakikua kila mahali. Bali utakakoniongoza sasa, Bwana, nitakuwa kama wale kwenye Matendo 19, 'Waliposikia Hili, walibatizwa tena katika Jina la Yesu Kristo.'"

… Fuata, ("Nimeenda sehemu ya njia, Bwana, vya kutosha kukupokea.")
Sasa nitaambatana Naye kote.

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha Ambako Ananiongoza — Mh.]

199 Mungu mpenzi, ninatumaini ya kwamba hilo linatoka moyoni mwangu. Natumaini ya kwamba unatoka katika moyo wa kila mtu anayeimba huo wakati huu, labda wengi watakaosikiliza kanda hii, ambao hawako ama wasioisikiliza sasa. Jalia tuwe tayari, Bwana, bila kujali gharama. Jalia tuwe tayari, Bwana, haidhuru itagharimu nini. Kasema, "Ni kama mtu anayetoka kwenda kulikabili jeshi lingine, askari, mfalme; kwanza yeye huketi na kuhesabu, iwapo yeye anaweza kufanya jambo hilo, kama anaweza kuyaacha mambo ya ulimwengu? Unaweza kuyaacha, ujiunge na jeshi la Neno la Mungu lilioandikwa; upige hatua na askari Wake, uruke pamoja na tai Wake?" Tujalie, Bwana, katika Jina la Yesu.

200 Mnaamini? Unamkubali? Vema. Tutawaona hapa tena, usiku wa leo, Bwana akipenda. Mnaamini jambo hilo kuwa ni Kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Ni dhahiri vya kutosha? ["Amina."]

Peleka Jina la Yesu,

Mtoto na huzuni na majonzi;
Litakufurahisha na kukufariji,
Lipeleke popo- …

Sasa, peaneni mikono na mtu aliye karibu nawe sasa.
Thamani, na tamu!
Tumaini la duniani, tumaini la duniani, furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Ee ni tamu iliyoje!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.
Tukiinama mbele ya Jina la Yesu,
Tukisujudu miguuni Pake
Mfalme wa wafalme Mbinguni tutamvalisha taji … (Yeye ni Mungu, basi)
Wakati safari yetu ikishakamilika,
Jina la thamani, Jina la thamani, Ee ni tamu ni tamu ilyoje! Ee ni tamu iliyoje!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Ee ni tamu iliyoje!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

201 Natumaini ya kwamba wahudumu wote walitambulishwa asubuhi ya leo, kutambuliwa.

Wakati mtu ameomba juma zima, akishangaa ni nini, akiona Maandiko haya, yamesimama moja kwa moja mbele yako. "Na ole wangu," Paulo alisema, "kama sihubiri Injili." Mwisho wa safari yake, yeye alisema, "Sikujiepusha na kuwatangazia Shauri lote la Mungu kama nilivyokabidhiwa kwangu."

202 Ninasahau wakati mwingine kutambua mambo, kuwasilisha, kuwaweka wakfu watoto wachanga.

Billy alisema, juzijuzi, mtu fulani alikuja, kasema, "Nimekuwa nikija hapa kwa miaka miwili, kumleta mtoto wangu awekwe wakfu."

Billy akasema, "Usifikirie vibaya juu ya jambo hilo. Nina mtoto mchanga, mwenye umri wa mwaka mmoja; bado hajawekwa wakfu, bado. Kwa hiyo nitangojea tu hata atakapokuwa mzee wa kutosha kwenda kule mwenyewe, nadhani."

Kwa hiyo tunamwona ndugu, dada, si—sivyo, mnaona, mimi … Jambo moja, tunapaswa kuwaweka wakfu watoto wetu.

Inatupasa kumbatiza kila mmoja. Kuna kidimbwi; haya hapa maji. Kama hujabatizwa, ni nini kinachokuzuia? Haya hapa maji. Njoo sasa hivi. Usingojee mpaka usiku wa leo; njoo sasa hivi. Kuna mtu anayesimama hapa atakayembatiza mtu ye yote aliyetubu na kukiri. Kama umebatizwa mara dazani, watakubatiza katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi. Mnaona? Sisi ndio hivyo.

203 Lakini, mnaona, Ujumbe uko moyoni mwangu. Sina budi kuutoa Huo. Hilo ndilo kusudi langu la pekee, haidhuru mke wangu anasema nini, watoto wangu wanasema nini, mchungaji wangu anasema nini, chochote kile asemacho. Ni Bwana wangu. Sina budi kuutoa Huo. Hilo ndilo kusudi langu pekee.

204 Na sasa, mara nyingi, nasahau kuwatambua wahudumu. Nadhani labda … ndugu yetu, Ndugu Neville, mtu wa thamani. Hawa ndugu wengine hapa, tuna furaha kuwa pamoja nanyi.

Si kwamba hatukubaliani nanyi, ndugu, kuwa tofauti. Wengi wenu hapa huenda ni wahubiri wa utatu. Hatutaki kuwakasirikia. Tunawapenda. Kama hatukuwapenda, kama sikuamini jambo hilo, nisingeondoka kwenye kanisa hili hata nishuke niende kule nikapige magoti yangu na kusema, "Mungu, nifanye sawa."

Sitaki roho hiyo ya kiburi, ya ubinafsi ichanganyikane na yangu. Ninataka roho yangu iwe nyeupe na safi, upendo wa ndugu, mtakatifu kwa Roho Mtakatifu. Sasa, kama mtu fulani akinifanyia jambo lolote baya, hilo ni sawa. Na hata ingawa naweza nikawa na haki ya kulipiza kisasi, sitaki jambo hilo maishani mwangu. La, na—nataka kuwa na upendo. Nataka kuwa tayari kusahihisha kwa upendo, kwa upendo ambao hujibu kabisa huko ng'ambo kwa ajili yake.

205 Simaanishi kuwa tofauti. Methodisti, Batisti, Katoliki, Presbiteri, hata uwe nani, sisemi mambo haya kusudi niwe tofauti, kuwa na kiburi kwenu. Kama nilifanya hivyo, mimi ni mnafiki na ninapaswa kuwa hapa chini kwenye madhabahu hii, nikimwomba Mungu.

Lakini ninasema jambo hilo, ni kwa sababu ya upendo, nami ninaona mnakoelekea. Sasa, sisemi jambo hili kwa nafsi yangu, na kusema ninadhania. Ninawapa BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni Kweli. Nami nawapenda kwa ajili ya mambo hayo. Mungu akubariki.

206 Sasa tunapoimba kifungu kingine cha wimbo huu, hebu, kabla hatujaenda. Tunataka muwe hapa usiku wa leo, mkiweza. Kama huwezi, Mungu awe pamoja nawe mpaka tutakapokutana. Tunaomba tu ya kwamba Mungu ata—atakubariki na kukupa kilicho bora sana katika nchi Yake, unaona.
Peleka Jina la …

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7